Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 21 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na nifafanue tu hapa kwa kuwa Wizara hii au Ofisi ya Makamu ina masuala ya Muungano na Masuala ya Mazingira. Kwa hiyo watakuwa wanakuja Wenyeviti wawili na pengine kwenye Wasemaji Wakuu wa Upinzani pia wawili. Kwa hiyo, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa niaba yake Mheshimiwa Paul Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukamilifu zaidi jina lake ni Mheshimiwa John Paul Lwanji. Sasa upande huo sasa mwakilishi wa Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Mazingira.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ilikuwa taarifa yetu hatujaimaliza kidogo, labda tutaiwasilisha baadaye.

**SPIKA:** Lakini basi iwahi kabla ya saa saa tano, saa 4.30

**MHE. ALI KHAMIS SEIF – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Sawa sawa.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. RIZIKI O. JUMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIBU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2011.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Randama ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 77

### Vituo vya Afya na Zahanati Kupatiwa umeme wa *Solar*

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi yetu kuna maeneo mengi ya vijijini na mijini ambayo hayajapatiwa umeme vikiwemo vituo vya afya na kusababisha matumizi ya taa na koroboi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka angalau umeme wa solar katika vituo vya afya na zahanati mbalimbali kama vile huko Puge-Bukere-Itobo na kwingineko nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekuwa na utaratibu wa kukarabati na kujenga vituo vya kutolea huduma za afya. Kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 – 2007/2008 kulikuwa na mradi maalum wa ukarabati wa vituo vya afya na zahati kwa kutumia fedha za Mfuko wa Pamoja *(Joint Rehabilitation Fund (JRF).* Kutoka katika mifuko mbalimbali ya wafadhili. Kutokana na mradi wa ukarabati wa vituo vya afya kufikia mwisho yaani mwaka 2009 Serikali inaendelea kukarabati, kupanua na kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali chini ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi yaani (MMAM).

Mheshimiwa Spika, Mpango wa MMAM ulianza rasmi mwaka 2007 na utaendelea mpaka mwaka 2017 na utatekelezwa katika awamu mbili za vipindi vya miaka mitano mitano. Mpango huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007. Lengo la Mpango huu ni kuboresha huduma za afya ya msingi katika kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mpango huu utahusisha ujenzi, ukarabati, upanuzi wa vituo vya kutolea huduma, pamoja na kuvipatia samani na vifaa.

Vile vile mpango unazingatia upatikanaji wa watumishi, kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto, kupunguza maambukizi na kuwapa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI, elimu ya afya na afya ya kinga.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa MMAM wananchi kupitia Kamati za Afya na Vituo vya afya huibua kazi kulingana na vipaumbele vyao kwa kumhusisha Mganga Mkuu na Mhandisi wa Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji.

Kwa hiyo, ni jukumu la wananchi kupitia Kamati zao husika kuweka kipaumbele kwa usimikikaji wa umeme jua *(solar power)* kama inavyofanyika katika maeneo mengine hapa nchini na Serikali kupitia Ofisi za Halmashauri zitakuwa watekelezaji wa shughuli hizo.

Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika Mkoa wa Tabora vipo jumla ya vituo 54 (Zahanati na Vituo vya Afya) ambavyo vimefungwa umeme wa jua kwa ajili ya kuendesha majokofu ya kutunzia dawa za chanjo na kuwasha chumba kimoja cha kuzalia wakima mama wajawazito.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia nampongeza Waziri wetu kwa majibu ambayo ameyajibu. Kwa kuwa wakina mama katika vijiji mbalimbali kwenye hizi zahanati na vituo vya afya hakuna umeme na hatimaye wanalazimika kutoa shilingi 500 kwa ajili ya kuweza kupatiwa mafuta ya taa na kuweza kujifungua. Ni lazima watoe shilingi 500 au 1,000.

Je, Serikali inaweza kusema ni jambo gani hilo? Je, ni halali kutoa ile shilingi 500 au ni utaratibu tu ambao umewekwa katika vituo hivyo kuwadhulumu wale akina mama?

Swali la pili, kwa kuwa sehemu nyingi hakuna umeme, na zahanati zetu hizi zinahitaji kupata umeme mpaka kule Urambo na Peramiho. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akajenga hoja katika Wizara yake ili Serikali iweze kutolea kodi kwenye suala la sola ili zahanati mbalimbali ziweze kupata umeme? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwa kazi yake nzuri anayoifanya kule Tabora kwa kununua taa kwa ajili ya zahanati mbalimbali na vituo vya Afya yeye mwenyewe kwa ajili ya akina mama kujifungulia. Taa hizo zimewekwa kwenye chumba kile tu ambacho akina mama wanajifungulia. Kwa hiyo, kwa hilo namshukuru sana. *(Makofi)*

Swali la pili, kuhusu shilingi 500 na 1,000. Sera yetu ya Taifa inasema kwamba akina mama wajawazito, watoto wenye umri wa mwaka mmoja mpaka mitano na wazee wa miaka 60 wanatibiwa bure. Kwa hizo shilingi 500 kwa kweli si halali na ni kinyume cha sheria na Sera zetu tunazojiwekea sisi wenyewe.

Kwa hiyo niwaagize tu kwamba vituo vya afya vyote na zahanati wakina mama kujifungua ni bure. Watoto wa mwaka mmoja mpaka mitano kutibiwa ni bure na wazee wa miaka 60 kutibiwa ni bure. Anaenda kinyume cha hapo ni kwamba anavunja sheria.

Kuhusu hoja ya kupunguza kodi kwenye vyombo au kwenye hizo *solar*, hili ni suala la Kiserikali. Naomba nilipokee tukalifanyie kazi tukalifanyie kazi pamoja na Waziri wa Fedha ili tuone namna bora ya kuweza kupunguza kodi katika vifaa hivyo muhimu.

**SPIKA:** Niliwaona kwa swali moja moja fupi sana la nyongeza, Mheshimiwa Sijapata halafu Mheshimiwa Msindai.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika nakushukru. Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, Jimbo la Kigoma Kaskazini kuna zahanati zingine ambazo zina sola lakini nashangaa kwa nini kituo cha afya Bitale ambacho sasa hivi kunapita barabara kubwa kabisa ya kutoka Mwandiga mpaka Manyovu ambayo iliyowekewa lami isiwekewe sola?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli sehemu nyingi kule Jimbo la Kigoma Kaskazini vituo vingi vimewekewa sola. Na ni kweli kituo cha Bitale hakijawekewa sola.

Mimi hili naomba nilichukuwe ili niwasiliane na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ili tuone ni namna gani bora ambayo tunaweza tukafanya ili kuhakikisha kwamba kituo hiki cha afya kinawekewa sola. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni mpango wa Serikali kujenga zahanati kila kijiji na kujenga kituo cha afya kila Kata na kwa kuwa Serikali inatoa *SDG* kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo vijijini. Waziri haoni kwamba sehemu ya fedha hizo zitumike kuweka sola ili kuokoa maisha ya wananchi wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, fedha zile za *Local Government Capital Development Grants*, ni fedha ambazo wananchi wenyewe wanaamua, hazina masharti yoyote. Kwa hiyo, ni vyema Halmashauri zenyewe zikajipanga, zikaweka katika vipaumbele.

Kwa taarifa niliyonayo kwamba fedha hizo robo tatu yake inaenda kwenye ujenzi wa vituo vya afya na zahanati na robo inaenda upande wa elimu.

Kwa hiyo, wakati wanaibua hiyo miradi ni vyema wakaweka hiyo *component* muhimu ya umeme wa sola. Kwa hiyo ni Halmashauri zenyewe na Halmashauri ya Iramba wanapata fedha hizo. Ningeshukuru kama Mheshimiwa Mbunge angeshirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuhakikisha kwamba kitu hicho muhimu kikawekwa kwenye vipaumbele vyao kwa hela zile za *Local Government Capital Development Grants.*

Na. 78

**Ukosefu wa jokofu la kuhifadhia maiti – Kituo cha Afya Kidodi na Hospitali ya St. Francis**

**MHE. CLENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kituo cha Afya Kidodi katika Tarafa ya Mikumi yenye wakazi wapato 72,250 na Hospitali ya *St. Kizito* inayohudumia wakazi zaidi ya 100,000 hazina joikofu hata moja la kuhifadhia maiti. Je, Serikali itawasaidiaje kupatikana kwa jokofu angalau moja katika kituo cha Afya Kidodi na moja katika Hospitali ya St. Kizito kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Kwanza niombe tu radhi kwamba Mheshimiwa Lyamba amefanya masahihisho baada ya sisi kujibu swali hilo. Na hospitali ya St. Francis iko katika Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, naomba nijibu kwa ujumla na hiyo St. Francis pamoja na St. Kizito.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) hupeleka fedha katika Halmashauri kwa ajili ya kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya. Jukumu la kuweka vipaumbele vya Bajeti limeachwa kwa wananchi wenyewe kupitia Bodi za Afya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vikao vilivyokuwa vinaendelea katika mikutano ya pamoja ya Halmashauri ya Bodi za Afya hususan katika Halmashauri za Wilaya za Kilosa na Kilombero kulitokeza wazo kuwa ni vyema katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika barabara kuu yaani *(high ways)* na idadi kubwa ya wananchi wanaohudumiwa katika maeneo husika pawepo na mpango wa kujenga majokofu ya kuhifadhi miili ya marehemu katika hospitali ya St. Kizito ambayo iko *high way* ya Mikumi, Gairo ambayo iko kwenye *high way* ya Morogoro-Dodoma na Magubike. Pia iko kwenye *high way* ya Morogoro-Dodoma na St. Francis ya Ifakara ambayo kwa sasa ina jokofu lenye kuhifadhi miili ya kati ya 4 – 8 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya St. Francis, sasa hivi inakarabatiwa na ukarabati wake utaweza kuifanya iweze kuhifadhi miili kati ya 20 mpaka 40. Hospitali ya St. Kizito kwa sasa kuna mpango wa kuweka jokofu kwa sababu kweli ni sehemu ambayo zinatokea ajali nyingi na mara nyingi maiti huhifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa badala ya palepale St. Kizito.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana na yenye matumaini kwa wananchi wa Mikumi, kwamba tutawekewa Jokofu katika Hospitali ya St. Kizito,

Je, kwa kuwa kituo cha afya cha Kidodi au neno lingine linalotumika ni Mhovu, nayo ipo katika *Highway* ya kutoka Mikumi hadi mji maarufu wa Mahenge, chenye umabli wa kilometa 75 kwenda Mahenge na kilometa 40 kwenda St. Kizito.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kuna umuhimu wa pekee kwa kuzingatia idadi ya watu wanaopata huduma katika kituo cha afya cha Kidodi, watu zaidi ya 72,000 kwamba napo pia panastahili kufikiwa kwa haraka kuwekwa jokofu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Lyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana kwa kushughulikia mambo mengi katika vituo vya afya vya Kidodi pamoja na kituo cha afya cha Mikumi pamoja na kituo cha afya cha Ulaya. Ni kweli kwamba Kidodi inahudumia wananchi wengi sana na iko barabarani.

Mheshimiwa Lyamba, anatambua jitihada za Serikali zilizofanyika kukarabati kituo kile cha afya.

Kwa hiyo, tutaendelea kukarabati na hilo la kuweka jokofu kwa kweli ni muhimu na tutalifanyia kazi. Nitawaomba ndugu zangu wa Kilosa katika fedha hizohizo za *Local Government Capital Developments Grants,* ambazo hazina masharti yeyote kuweka kwenye kipaumbele ili kituo cha afya cha Kidodi, kiweze kupatiwa jokofu.

Na. 79

**Wananchi wa Kiranjeranje kulipwa fidia za nyumba zao**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI K.n.y. MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kiranjeranje kwenye Wilaya ya Kilwa hawajalipwa fidia za nyumba zao katika barabara kuu ya Nangurukuru-Mbemkuru na kwa kuwa Wilaya ya Kilwa tayari imefanya tathmini ya gharama zipasazo. Hata hivyo miaka mitatu imeshapita bila fidia hizi kulipwa.

Je, lini wananchi hao watalipwa haki zao?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Mbwemkuru, jumla ya nyumba na mali za wananchi 100 zilizokuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ziliwekewa alamaya X na kutakiwa kubomolewa ili kupisha ujenzi wa barabara zikiwemo nyumba 23 za wananchi wa Kiranjeranje.

Baada ya zoezi la uthamini kukamilika wananchi wote wenye stahili walilipwa stahiki zao. Jumla ya shilingi milioni 104,093,651 zilitumika, kati ya hizo, shilingi 41,717,105 zililipwa kwa wananchi 23 wa Kiranjeranje. Baada ya malipo hayo, hapakuwepo na malalamiko yoyote yaliyopokelewa na Wakala wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu baada ya fidia kufanywa, Wizara ilipokea taarifa ya madai mapya ya fidia yenye thamani ya shilingi milioni 154,578 yaliyotokana na uthamini uliyofanywa kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Tathmini hiyo licha ya kutofuata utaratibu, haikuwa na vielelezo vya kuthibitisha uhalali wa madai hayo.

Kutokana na utata huo Wizara yangu kupitia Ofisi ya Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Lindi ilimwandikia Mkuu wa Mkoa kupitia barua Kumbukumbu Namba *RML/TanR/N.90/01/Vol.VII/06* ya tarehe 2 Aprili, 2008 ikieleza kutokubaliana na madai haya. Kutokana na maelezo hayo Serikali haidaiwi fidia yoyote baada ya kuwalipa wananchi wote waliostahili fidia kwenye ujenzi wa barabara hiyo.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana katika wilaya ya Kilwa. Pamoja na kwamba malipo yote yamefanyika, lakini haya malipo yaliyobaki ya milioni 154,578 limekuwa ni tatizo kiasi kwamba Rais, akipita pale, anasimamishwa kila mara. Mimi naiomba sana tafadhali Serikali, kwamba wafanye utaratibu wa kusaidiana, Wizara, Serikali pale Mkoani pamoja na wananchi kuliweka sawa suala hili kwa sababu linaleta utata sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona kama umepewa ushauri, si swali. Lakini pengine Mheshimiwa Waziri ungependa kusema chochote?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kutoa maelezo mafupi ya ushauri ambao nimepewa na Mheshimiwa Mikidadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ninauhamasisha Mkoa, kupitia *DC* na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, kufuata utaratibu wa kuwasilisha madai haya ili yaweze kufanyiwa kazi. Malipo yalifanywa mwezi Disemba 2005, madai mapya yamekuja Januari 2008, miaka mitatu baadaye, hayakuidhinishwa na *Chief Valuer* ambaye anahitajika kuidhinisha madai yoyote ya aina hii ya fidia na hayakuhusisha Wakala wa Barabara.

Kwa maana hiyo ni kwamba utaratibu haukufuatwa kabisa, kama kuna madai ya kweli yafuate utaratibu ili Serikali iweze kuyafanyia kazi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fidia imekuwa ni kero kwa wananchi wengi ambako miradi ya maendeleo inapita. Na kwa kuwa, mpaka sasa hivi Wizara imekabiliwa na madeni ya fidia ambayo hayajalipwa.

Je, Wizara inasema nini kuwalipa fidia wananchi wa Mpanda, ambao wameathirika na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege pale kashaolili?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kulipa madeni yote ya fidia ambayo yanahitajika kulipwa ndani ya mwaka 2010/2011 kwa mwaka mpya huu ambao unafuata. Jumla ya mahitaji ya fidia kwa mwaka unaofuata yanafikia bilioni 53 na tumejiopanga kuweza kuhakikisha kwamba pesa hizo zinapatikana na tulipe fidia katika miradi yote ile ambayo tumepanga kuitekeleza ili tusikwame katika kuitekeleza mirradi hiyo.

Na. 80

**Kukomesha Ukiukwaji wa Sheria Unaosababisha Ajali**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ajali nyingi zinapotokea majini huwa ni vigumu kupata idadi ya watu wanaopoteza maisha; na kwa kuwa, vyombo hivyo hujaza watu wengi na mizigo kinyume na sheria.

Je, Serikali inawachukulia hatua gani wamiliki wa vyombo hivyo wanaokiuka Sheria, pamoja na wadhibiti wa vyombo hivyo *(SUMATRA)*?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyombo vya majini nchini mwetu husajiliwa na kukaguliwa chini ya Sheria ya Usafiri wa Majini *(Merchant Shipping Act)* ya mwaka 2003 kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Hivyo, itokeapo ajali uchunguzi hufanywa chini ya mojawapo ya Sheria hizo kwa kuzingatia usajili wa chombo na hatua huchukuliwa kufuatana na matokeo ya uchunguzi au mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Uchunguzi wa ajali husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu 244 na 245 cha Sheria ya Usafiri majini ya 2003, ni kosa kwa mmiliki na nahodha wa chombo kuanza safari huku chombo

kikiwa kimezidisha abiria au mizigo. Hivyo, hatua za kisheria huchukuliwa pale chombo kinapokutwa kimezidisha abiria au mizigo.

Adhabu ya kosa la kuzidisha abiria ni faini ya dola za Kimarekani elfu mbili au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili, faini na kifungo.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine pia huchukuliwa pale itakapoonekana kuwa kwa namna moja au nyingine mkaguzi wa *SUMATRA* au Ofisa mwingine, nahodha au Ofisa mwingine wa meli amesababisha ajali kwa uzembe au kwa makusudi. Hatua hizo ni pamoja na kusimamishwa kazi ya ukaguzi au kufutiwa cheti cha unahodha au uofisa wa meli *(Certificate of Competence).*

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Juni 2006, *SUMATRA* imeweka utaratibu wa vyombo vya majini kuacha taarifa zake kabla ya kuanza safari. Taarifa hizo ni pamoja na idadi ya mizigo na abiria ambazo hulinganishwa na taarifa zilizopo kwenye cheti cha ubora cha chombo husika; chombo ambacho kimepakia kuzidi kiasi, hakiruhusiwi kuanza safari. Usimamizi huu hufanywa na *SUMATRA* kwa kushirikiana na wamiliki wa Bandari au mialo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Machi, 2006 kituo cha utafutaji na uokoaji cha cha Dar-es-Salaam kilizinduliwa na kuanza kazi rasmi. Pamoja na majukumu yake mengine kituo hiki pia hupokea taarifa zinazohusu usalama wa vyombo. *SUMATRA* kupitia vyombo mbalimbali imetangaza namba za mawasiliano ambazo mwananchi yeyote, popote alipo nchini anaweza kutoa taarifa za usalama kwa *SUMATRA* zikiwemo za chombo kupakia abiria au mizigo kuzidi kiasi ili hatua zichukuliwe mapema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba watumia vyombo vya majini na wananchi wote kwa ujumla kusaidia kutoa taarifa Polisi au *SUMATRA* kupitia kituo cha utafutaji na uokoaji cha Dar-es-Salaam pale wanapoona chombo kimepakia kuzidi kiasi au kwa namna yoyote ile kinahatarisha usalama wa chombo na maisha ya watu.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini njina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, mwaka 2008/2009 vyombo vingi vilipata ajali nja kuzama kwa ajili ya uchakavu na kuzidisha abiria na mizigo. Je, ni watu wanagapi waliokamatwa na kutozwa faini au kufungwa au kufukuzwa kazi? Na wale waliopoteza mali zao ni wote wamelipwa fidia?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa bahari zetu sasa zinaongezeka ,shughuli za biashara, uvuvi wa raia na uvuvi unaofanywa na wageni. Je, ni lini Serikali itakuwa na boti ya doria ili kulinda bahari zetu na kuokoa maisha ya watu pale ajali inapotokea?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kadika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza la watu wangapi ambao wamefikishwa mahakamani na kupigwa faini; bahati mbaya takwimu hizi sina, lakini nitamwomba Mheshimiwa Kadika, tuwasiliane ili niweze kuzikusanya na kuweza kumpatia.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili la ongezeko la shughuli za baharini na za uvuvi na ajali ambazo zinatokea, tumejipanga kwa ajili ya kuboresha hatua za kuweza kudhibiti usalama katika maji, baharini na katika maziwa yetu. Na mojawapo ni uanzishwaji wa kituo hiki cha utafutaji na uokoaji wa majini ambacho sasa hivi kimeshaanza kazi na kina uwezo wa kufanya mawasiliano katika maeneo yetu yote ya Baharini pamoja na Maziwa yote Tanzania.

Sasa hivi tunachojaribu kukiimarisha ni ushirikiano kati ya vyombo vya Serikali, na tumeweka Kanuni kwamba vyombo vyote vitakavyokuwa karibu na Chombo ambacho kimepata ajali, kinawajibika kutoa msaada mara moja na kwa kupitia kituo chetu hiki, kinafanya mawasiliano ya moja kwa moja na vyombo hivyo ili ikuweza kusaidia inapotokea ajali. Serikali itaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunapata boti zaidi za doria na zile ambazo zitahusika katika kusaidia uokoaji.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuanzishwa hicho kituo cha utafutaji na uokoaji tarehe 25 Machi, 2009. Lakini swali langu liko hapa. Kwa kuwa, ukanda wa bahari ni mrefu pamoja na maziwa yaliyopo huko juu. Na kwa kuwa, kituo kimoja cha uokoaji kilichoanzishwa Dar-es-Salaam, hakiwezi kutosha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vituo rasmi vya uokoaji pamoja na zana kamili za uokoaji ikiwemo Helkopta, katika visiwa vya Unguja, Pemba, Tanga, Mtwara na Ziwa Viktoria?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imelichukulia jambo hili kwa umuhimu sana, linahusiana na maisha ya wananchi wa Tanzania.

Kwa hivyo, kama ambavyo Mheshimiwa Mnyaa ameuliza, sasa hivi Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba inadhibiti usalama wa majini moja kwa kuwa na kituo hiki ambacho kiko Dar-es-Salaam, kilichoanza kazi rasmi tarehe 29 Machi, 2009 lakini pia tuna mkakati wa kuanzisha kituo kingine mjini Mwanza ambacho kitadhibiti eneo la ziwa Viktoria na ziwa Tanganyika, na hasa ziwa Viktoria.

Kituo kile ambacho kinafanya kazi Dar-es-Salaam, kina uwezo wa kudhibiti na kuratibu shughuli zote za uokoaji kwa eneo lote la mwambao wa bahari mpaka Pemba na zaidi ya Pemba na maeneo ya Mombasa, kwa hivyo kina uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, na huu ni ufadhili wa *IMO* ambayo imetusaidia sana Serikali ya Tanzania tumeshirikiana nao kwa ajili ya kujenga kituo hiki madhubuti. Kwa hivyo ukanda huu kuanzia Kaskazini mwa Msumbuji mpaka karibu na Mombasa, na kupita

Pemba kwa maana ya Mashariki, kote kunaratibiwa vizuri sana na kituo hiki kimoja ambacho kina uwezo mkubwa sana.

Na. 81

**Mradi wa Maji wa ADB - Longido**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa *ADB* Wilayani Longido umejengwa chini ya kiwango na usimamizi wake ni hafifu; na kwa kuwa, mradi huo unasimamiwa na Mhandisi wa Wilaya ya Monduli ambaye hana nafasi kubwa ya kutembelea Longido:-

Je, ni lini mradi huo utakabidhiwa kwa mhandisi wa Wilaya ya Longido?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Monduli ulitekelezwa katika vijiji 18 na miji midogo ya Monduli na Longido kwa ufadhili wa pamoja wa Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani *ADB*, kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 38.

Mradi ulianza kutekelezwa mwezi Novemba 2005 na kumailika mwezi Juni 2009. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, mradi ulitekelezwa katika Mji mdogo wa Monduli na vijiji 14 na katika Halmashauri ya Longido, mji uliohusika ni Namanga na vijiji vinne vgya Eworendeke, Orkejuloongishu, Ngoswaki na Sinoki.

Mheshimiwa Spika, wakati mradi unaanza Halmashauri ya Wilaya ilikuwa ni moja tu ya Monduli, lakini mwezi Julai 2007, Halmashauri ya Longido nayo ilianzishwa.

Hata hivyo kulingana na makubaliano ya uendeshaji wa mradi yaliyokuwa yamefikiwa kati ya Serikali ya Tanzania na *ADB*, pamoja na kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ya Longido, timu ya kuratibu mradi, yaani *Project Implementation Team*, ilibaki kuwa ni ileile ya Monduli kama ilivyokuwa imekubalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya mradi kukamilika vijiji vyote vinne katika Halmsahuri ya Longido, vilikabidhiwa *scheme* zao za maji, kwa sababu tayari vilikuwa vimesajiliwa kama vyomvo vya watumia maji, *Water User Associations (WUA).*

Mji mdogo wa Namanga, haukuwa na *WUA* iliyosajiliwa na hivyo *scheme* yake ya maji ilikabidhiwa kwa Mkurugenzi Mtendaji mpaka hapo watakaposajili chombo chao kisheria.

Kwa upande wa Halmashauri ya Monduli, mji wa Monduli na vijiji vyote kumi na vinne vyombo vyao vilikuwa vimesajiliwa na hivyo vilikawa na *scheme* zao za maji.

Mheshimiwa Spika, ningependa tena kukumbusha Halmashauri zote nchini kwamba uendeshaji na usimamiaji wa miradi ya maji unafanywa na vyombo vya watumia maji ambavyo vinasajiliwa kwa mujibu wa sheria ya maji na usafi wa mazingira Namba 11 ya mwaka 2009 na usajili wa vyombo hivi sasa unafanywa katika ngazi ya Halmashauri. Kwa hiyo, hakutakuwa na makabidhiano mengine kwa mhandisi wa maji wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Laizer kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji na kwa kuibua jambo hili ambalo bado Halmashauri nyingi zinahitaji kukumbushwa namna ya kuendesha na kusimamia miradi ya maji.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kilio changu hapa ni fedha mibilioni yaliyotumika na kazi haijamalizika. Je, Serikali wako tayari kwenda kuangalia miradi hiyo na kuona kwamba hakuna *value for money* iliyotumika na wananchi bado miradi yao haijakamilika? *(Makofi)*

Kwa kuwa mradi huo ulikuwa na magari manne, na Halmashauri zilipogawanywa tuliambiwa kwamba kila Halmashauri watachukua magari mawili. Lakini mpaka sasa Longido wamepewa gari moja tu. Je, Serikali inaweza sasa kugawa magari hayo manne, mawili yaende Longido na mawili yabaki Monduli?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri la msingi. Namshukuru vilevile Mheshimiwa Lekule Laizer kwa maswali yake, lakini kubwa zaidi kwa ufuatiliji wa masuala ya maji Longido kwa niaba ya wananchi wa Longido.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Monduli, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tafakari ya jinsi mahali tulipofika katika utekelezaji na maeneo yote ambayo hayajakamilika tutayachukua kama sehemu ya pili yaani awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu hasa katika eneo la Longido. Wizara yangu itatuma wataalam kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Longido ili kuweza kukamilisha utayarishaji wa mradi mpya ambao Serikali itatekeleza.

La pili kuhusu suala la magari, namwomba Mheshimiwa kwa kuwa mradi umekwisha na magari yameshatumika yale manne kwa kweli ni ya zamani na gari la zamani tukimpa kwa kweli ni mzigo tu kilichofanya Serikali ni kutoa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido gari jipya ambalo tayari tumeshawapatia. Si hivyo tu tumewapa

kompyuta, *printer, photocopier* na tunaendelea kuwasaidia hata ujenzi wa ofisi za maji katika Wilaya ya Longido.

Kwa hiyo, kwa kweli naomba awe na subira sisi tunaendelea kuwasaidia wananchiwa Longido.

Lakini niseme amelifuatilia sana hili suala Mheshimiwa kwa maana ya kwamba kulikuwa hakuna uwiano mzuri katika utekelezaji kati ya Longido na Monduli. Lakini nasema kama ilivyokawadia ya binadamu tunapata busara baada ya tukio ingekuwa tunaufanya mradi huo sasa labda tungeufanya vinginevyo lakini sasa tusahau yaliyopita tugange yanayokuja tutatekeleza mradi kwa ushirikiano.

Namshukuru yeye na uongozi na wananchi wa Longido hasa wakati nilipofanya ziara Longido kutembelea mradi wa *IGODIN* kwa mapokezi lakini vilevile kwa ushirikiano mkubwa walionipa ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wakati wa kipindi cha maswali naona bado watu wanakwenda sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa jamani huyu ndiyo kiongozi wa shughuli za Serikali, mkiwa mnabana sana, kuna Mbunge mmoja nimemwangalia amekaa dakika kumi na saba (17).

Sasa hapa sio mahala pa mikutano ya aina hiyo wala msichukue fursa hii pengine ni vigumu kumwona ofisini basi mnambana haelewi kabisa Mawaziri wamejibu nini katika maswali ya nyongeza.

Mimi ningependekeza badala ya kumbana Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa Maswali, yeye ni mwaminifu sana kukaa humu ndani, baada ya maswali wakati mjadala unaendelea ni vyepesi zaidi mtu kuweza kufuatilia, lakini maswali mengine haya huwa tunamtazamia Waziri Mkuu kuingilia kati akiona kwamba inabidi kufanya hivyo. Sasa kama mmebana toka saa tatu mpaka saa nne, inakuwa shida kidogo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Arfi, kama hayo ndiyo maelekezo ya Spika, kwa hiyo urudi kwenye kiti chako. *(Kicheko)*

Na. 82

**Kuwapatia Maji Wananchi wa Kijiji cha Mlela**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa kijiji cha Mlela Wilaya ya Kigoma Vijijini wana matatizo ya maji ambapo hutumia maji kutoka katika visima walivyochimba wenyewe; na kwa kuwa, chanzo cha maji kilichoko kijijini kwao maji yake huepelekewa wananchi wa kijiji cha jirani cha Kidahwe:-

(a) Je, kwanini Serikali isiwachimbie visima virefu na vifupi wananchi hao kwa kuwa chanzo chao cha maji kilipelekwa Kidahwe?

(b) Je, ikiwa chanzo hicho cha maji kinajitosheleza kwa nini wananchi wa Mlela nao wasitumie maji hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1979 Serikali ilikamilisha ujenzi wa mradi wa maji kwa ajili ya vijiji vya Mlela na Kidahwe kutoka kwenye chanzo cha mto Mkuti ni huko Kigoma. Katika ujenzi wa mradi huo aina mbili za teknolojia zilitumika kulingana na sura ya ardhi katika vijiji hivi. Kijiji cha Mlela kiko uwanda wa juu ya chanzo cha maji, wakati kijiji cha Kidahwe kiko chini. Hivyo, mashine moja ya kusukuma maji ilifungwa ili kuwezesha wananchi wa kijiji cha Mlela kupata maji kutoka kwenye chanzo hicho. Wakati wananchi wa Kidahwe nao walipelekewa maji kwa njia ya mtiririko kwa sababu sura ya nchi ilikuwa inaruhusu hivyo. *(Makofi)*

Kwa upande wa kijiji cha Mlela, mradi ulisimama baada ya miaka miwili tu, kutokana na wakazi wa Mlela na Kidahwe kushindwa kuchangia gharama za kuendesha. Mradi ulisimama baada ya miaka miwili tu kutokana na wakazi wa Mlela kushindwa kuchangia gharama za kuendesha mradi.

Mwaka 1981 mashine ya maji ilihifadhiwa kwenye ofisi ya Serikali ya kijiji cha Mlela. Hivi sasa mashine hiyo imechakaa na juhudi ya kuifufua haziwezi tena kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, baada ya melezo hayo mafupi napenda kujibu sasa swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, kwamba kuna uhaba maji katika kijiji cha Mlela unaosababishwa na kuharibika kwa mashine ya kusukuma maji kutoka katika *intake* iliyoko kwenye mto Mkuti. Sababu nyingine ni miundombinu ya maji iliyopo yenye tanki, mabomba na vichoteo iliyojengwa mwaka 1979 ambayo nayo imechakaa na haiwezi kukidhi mahitaji ya watu waliopo sasa.

Kwa kutambua tatizo hilo mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliboresha visima vifupi vitatu vya asili na kuviwekea pampu za mkono. Adiha, katika mwaka 2008/2009 Wizara iliipatia Halmshauri ya Wilaya Kigoma shilingi milioni 559,855,000 kwa ajili ya miradi inayoweza kutoa matokeo ya haraka ambapo

Halmashauri ilitumia sehemu ya fedha hiyo kwa kuboresha chemchem tano na kujenga vituo vya kuchotea maji.

Uchunguzi uliofanywa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Kigoma unaonyesha kwamba njia endelevu ya kuongeza upatikanaji wa maji katika kijiji cha Mlela ni kuchimba visima vingine vitano ambavyo gharama yake inakadiriwa kuwa shilingi milioni 25.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kutafuta fedha hizo katika mwaka 2010/2011 ikiwa pia ni pamoja na kutafuta vyanzo vingine hata nje ya Bajeti ya Serikali ili visima hivyo vifupi vitano vinavyotakiwa vichimbwe na kupunguza tatizo hilo la kijiji cha Mlela.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapunguzia gharama ya uendeshaji wa mradi w kazi wa kijiji cha Mlela, naimshauri Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kufanya mambo mawili yafuatayo:-

(i) Kufanya uchunguzi wa sehemu nyingine ya kuchukulia maji kwa njia ya mtiririko na makisio ya gharama ya mradi mzima.

(ii) Kufanya uchunguzi wa nishati mbadala inayoweza kutumika kuendesha pampu za maji.

Mheshimiwa Spika, nichukue tena fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, kwa kuwa mara kadhaa ameendelea kuleta tatizo hili Serikalini ili kulitafutia ufumbuzi suala la wananchi wa kijiji cha Mlela.

**MHE. SIJAPA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa hili swali lilikuja hapa Bungeni, tangu mwaka 2007 nakumbuka, na sasa hivi limerudi tena na kwa kuwa niliwahi kusema kuwa vile visima vitano walivyochimbiwa wale wananchi havikuwatosheleza kwa sababu idadi ya watu ni kubwa. Lakini papo hapo Serikali ikaahidi kuwa itachimba visima vingine vitano, nilidhania sasa imeshatekeleza. Sasa ni lini kwa muda mufaka kutoka 2010 mpaka 2011 ni lini sasa itajenga visima hivyo?

Na kwa kuwa sisi Wabunge wanawake tumekuwa tukifanya kazi sana katika majimbo ya wanaume. Kwa mfano mkoa wa Kigoma nimefanya kazi katika majimbo saba (7). Na kwa kuwa wanawake sasa inatakiwa twende majimboni na sisi tufanye kazi tukiwa tumetulia, Ndugu zangu nawaunga mkono wanawake wote twende majimbo tukafanye kazi. *(Kicheko)*

**SPIKA**: Hili la pili sio swali ni rai tu kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la Kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza moja la Mheshimiwa dada yangu Sijapata japokuwa ameshapata yeye bado anaendelea kujiita Sijapata Nkayamba, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa mwaka 2007 aliuliza na mie nilijibu hapa na mimi nimefuatilia kwa dhati kabisa na yeye anajua na mimi ni mdau nimezungumza na Halmashauri ya Wilaya yake kabisa kabisa kwamba mwaka 2010 na 2011 tutafute fedha na nimesema hapa kwamba hata nje ya Bajeti ya Serikali kama nilivyosema wakati nikijibu swali wiki ile iliyopita hatuwezi kutegemea tu Serikali kwa kila kitu ndiyo maana namhakikishia tutafute fedha, milioni 25 sio fedha nyingi sana. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba mwaka huu 2010/2011 Wizara yangu na Halmashauri tutatafuta hizo fedha na visima vitachimbwa, Mheshimiwa Sijapata amekwishapata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda umetubana kidogo Waheshimiwa nadhani itabidi tuendelee na swali linalofuata ni la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, linaulizwa na Mheshimiwa Castor Ligallama Mbunge wa Kilombero.

Na. 83

**Kutambulika kwa Mpango wa Itinerant Teaching Programme Access and Education Equality Improvement**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAM** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika wilaya ya Kilombero kuna kituo *(Lumemo Resource Centre*) kinachotoa elimu kwa walemavu chini ya mpango wa *Itinerant Teaching Programme Access Education Quality Improvement:-*

(a) Je, Serikali inautambua mpango huu?

(b) Kama unatambulika. Je, ni lini walimu hao watapewa pikipiki mpya ili waweze kutoa huduma kikamilifu hasa ukizingatia kuwa pikipiki walizonazo ni chakavu na hazifai kuwa barabarani *(not road worthy)?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM BAKARI MAHIZA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika katika Bunge hili la 20 salama salamin. Aidha kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama (Mb), lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Itinerant Teaching Programme* ni mpango wa utoaji elimu kwa watoto wasioona na wenye uoni hafifu katika shule za msingi za kawaida ambazo hazina vitengo vya elimu maalum.

Mpango huu hutekelezwa shuleni iwapo kuna watoto wasioona na wenye uoni hafifu katika mazingira shule ilipo. Mpango huu unaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Chama cha Kuhudumia Wasioona na Tanzania *(Society for the Blind (TSB)* na Shirika la *Sigh Stavers Tanzania (SST)* katika mikoa 10 ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida na Iringa.

Mheshimiwa Spika, mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Pwani Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Singida inahudumiwa na Chama cha Wasioona Tanzania na Mkoa wa Iringa unahudumiwa na Shirika la *Sight Savers Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Taasisi hizo inatoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na visaidizi kama vile vitabu, karatasi, mashine za kuandikia na fimbo nyeupe. Wizara pia hutoa walimu na wataalam kwa ajili ya mpango huu. Chama cha wasioona Tanzania na Shirika la *Sight Savers Tanzania* hutoa pikipiki na kuzifanyia matengenezo zinapoharibika. Chini ya mpango huu walimu wataalam hutembelea wanafunzi na walimu shuleni kwa ajili ya kutoa huduma na ushauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya mawasiliano na Chama cha Wasioona Tanzania kuhusu upatikanaji wa pikipiki mpya kwa walimu wanaotekeleza mpango huo, wakiwemo walimu wa wilaya ya Kilombero.

Chama cha Wasioona Tanzania kinatoa fedha za nauli kiasi cha shilingi 60,000/= kwa mwezi kwa walimu ili waweze kuzifikia shule zilizo katika mpango huo wakati kikiendelea na jitihada ya kutafuta pikipiki mpya. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri hasa kwa ahadi ya pikipiki kwa walimu walio katika kituo cha Lumemo kule Kilombero. Nina maswali mawili ya nyongeza kituo hicho licha ya pikikipi wana uhaba vilevile wa thamani *stationary,* pamoja na mashine zile za braille. Je, Waziri ataweza kushirikiana tena na Chama cha Wasioona Tanzania kuwapatia vifaa hivyo kituo hicho?

Kwa kuwa walimu awali walipata mafunzo yao nchini Malawi. Je, kuna mpango gani endelevu wa kupata walimu hawa hapa hapa nchini ili elimu hiyo iweze kutolewa kila Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM BAKARI MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, vituo hivi pamoja na kwamba vinaendeshwa kwa ushirikiano na asasi zisizo za kiserikali bado wajibu mkubwa upo chini ya Halmashauri na mahali vituo vilipo.

Kwa maana hiyo tunawaomba wakuu wa vituo hivyo waweze kuwasilisha maombi yao kwa Halmashauri zao ili waweze kupatiwa misaada mingine ya kitaalam na kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba jukumu jukumu la kupeleka visaidizi na vitendea kazi na vitu vingine vya kitaalam litaendelea kubakia kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na mimi namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tutalipatia kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anaulizia juu ya elimu endelevu kwa walimu hawa ambao wanatoa mafunzo haya, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunacho chuo maalum Patandi, kiko mkoa wa Arusha ambacho kinatoa mafunzo haya na pale inapobidi walimu hupelekwa hata nchi za nje kwa mfano Uganda, Kenya, Malawi, na Uingereza kwa ajili ya kupata mafunzo ya ziada na hili lipo linatekelezwa. *(Makofi)*

Na. 84

**Kupeleka Huduma ya Umeme Katika Vijiji vya Jimbo la Gairo**

**MHE. AHMED M. SHABIBY** aliuliza:-

Kwa kuwa, jimbo la Gairo lina vijiji vingi na vikubwa vyenye idadi kubwa ya watu na hivyo kustahili kupatiwa huduma ya umeme ambao unapita katika maeneo hayo kutokea mkoa wa Dodoma, ambako unasambazwa kwenye vijiji vyenye idadi ndogo ya watu.

(a)Je, Serikali itakubaliana nami kwamba huduma hiyo ya umeme kanda ya Kati inasambazwa kwa kufuata matakwa ya watu binafsi na si kwa umuhimu na wingi wa watu?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kata za Chakwale, Kibedya na Rubeho ambazo zipo umbali wa kilometa 10 toka umeme ulipo na Mheshimiwa Rais aliahidi zipatiwe umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 kwenda Gairo ni tawi la njia kuu ya kupeleka umeme wilaya ya Mpwapwa kutokea Dodoma. Njia hii ya umeme kutoka Dodoma kwenda Mpwapwa iliyojengwa mwaka 1996 kwa msongo wa kilovoti 11 iliongezwa nguvu mwaka 2002 na kuwa ya msongo wa kilovoti 33 ili

kuboresha hali ya upatikanaji umeme wilayani Mpwapwa kwa kuupatia mji huo umeme wa gridi badala ya umeme wa majenereta yaliyokuwa yakitumika Mpwapwa.

Mwaka 1999 hadi mwaka 2000 njia ya umeme kuelekea Gairo ilijengwa. Tawi hili la njia ya umeme kwenda Gairo lilitoka katika njia ya umeme iendayo Mpwapwa katika kijiji cha Mbande. Urefu wa njia hii ya umeme kuanzia kituo cha umeme cha Zuzu (Dodoma) hadi Gairo ni kilomita 140 na kati ya hizo, kilomita 133 ziko upande wa Dodoma na 7 ziko upande wa Morogoro (Gairo). Lengo la Serikali katika miradi ya umeme vijiji ni pamoja na kuvipatia huduma ya umeme vijiji vinavyopitiwa na njia ya umeme kama namna mojawapo ya kuleta maendeleo ya wananchi na ndivyo ilivyokuwa kwa vijiji vilivyopitiwa na njia hii ya umeme kwenda Gairo. Kuhusu umeme wa Kata ya Chakwale, Kijiji cha Chakwale kiko takribani kilomita 12 hivi kutoka barabara iendayo Dar es Salaam upande wa kushoto ukitokea Dodoma. Kwa mujibu wa upembuzi yakinifu uliofanywa na *TANESCO* ili umeme uweze kufika Chakwale kunahitajika kujengwa kilomita 16 za njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 kutoka Ibuti na kuchepukia Ingirori; kuweka *transforma* zipatazo 6 na ujenzi wa kilomita 12 za njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 kwenye vijiji vya Ingiroli, Kibedya A, Kibedya B hadi Chakwale pamoja na kijiji cha Mtumbatu. Gharama ya kazi hii inakadiriwa kuwa shilingi 1,056,767,316.00.

Mheshimiwa Spika, ili kufikisha umeme kijiji cha Rubeho unahitajika ujenzi wa kilomita 15 za njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 kutoka Gairo kupitia vijiji vya Malimbiku, Bombasita, Msingi Kati, Msingi Juu, Kwipipa, Rubeho A na Rubeho B. Kazi nyingine ni ufungaji wa transfoma zipatazo 7 na ujenzi wa kilomita 18 za njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi 978,900,000.

Baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatekeleza usambazaji wa huduma ya umeme kwa kulingana na mipango iliyojiwekea kama vile wa kupeleka umeme vijijini unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*), na ule wa jumla yaani *Power System Master Plan*. Nia ya Serikali ni kupeleka huduma ya umeme kwa wananchi wote bila upendeleo kwa kuanzia Makao Makuu ya Wilaya zote pamoja na vijiji vinavyopitiwa na njia hizo za umeme.

(b)Serikali imekwishafanya tathmini ya kupeleka umeme Kata ya Chakwale, Kibedya na Rubeho kama ilivyoelezwa hapo juu na taratibu za kupata fedha za utekelezaji toka Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) zinaendelea.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa vile hii ni ahadi ya Rais, na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini amejibu kwamba, tayari tathmini imeishafanyika na kiasi cha pesa kinachohitajika kimeishapatikana.

(i) Je, ni lini sasa atapeleka umeme katika Kata ya Chakwale na Rubeho?

(ii) Kwa vile mwaka huu ni wa Uchaguzi Mkuu na hii ni ahadi ya Rais kama hakuna uwezekano, Waziri atakubaliana na mimi sasa aende kwenye Jimbo la Gairo sehemu hizo ili akawaelezee wananchi wa sehemu walizoahidiwa na Rais?

**SPIKA:** Aah! majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, naona mwenzetu huyu amebanwa sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba hii miradi ya Mheshimiwa Shabiby kwenda Chakwale, ni miradi mikubwa kidogo na kama nilivyosema, jumla ya gharama zinazohitajika kutekeleza miradi hii ni shilingi bilioni 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba kutokana na jinsi ambavyo shughuli za kiuchumi zimekuwa zikipanuka pale Chakwale na Kibedya, watu wameongezeka sana lakini na uwezo wa kiuchumi wa Kata hizo umeongezeka sana na ndiyo maana nina amini kwamba hata Mheshimiwa Rais alipofika pale aliona umuhimu wa huduma ya umeme pale na kwamba itasaidia kuboresha maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema mradi huu kwa maombi aliyoomba Mheshimiwa Shabiby, kuna maeneo ninafahamu kama Ukwamani ambayo yanaanza sasa hivi, na nadhani kuelekea mwezi wa Nane, au wa Tisa yatakuwa tayari. Haya maeneo mengine yamefanyiwa tathmini na tunasubiri tukipitisha Bajeti hii na Bajeti ya *REA* ambayo ninatarajia tutaipitisha hapa hivi karibuni, ili tupate mwelekeo wa kujua miradi hii itakamilika lini.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ni kweli nina tambua kwamba, ahadi ilitolewa na huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu na suala hilo linatubana wote tuliomo humu ndani. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba, katika kipindi hiki ambacho tupo hapa Bungeni, na Chakwale hapo siyo mbali tunaweza tukatafuta muda tukaenda na Mheshimiwa Mbunge, siyo tu kuelezea kama mradi hautatekelezwa, lakini kuuelezea mradi kwa ujumla kwa wananchi wa Chakwale.

**SPIKA:** Waheshimiwa, ingawa muda wa maswali umepita kidogo, lakini mtakumbuka tulivyoanza kulikuwa na Hati za kuwasilishwa mezani zimetuchukulia muda. Kwa hiyo, ndiyo tunaufidia hivyo. Kwa hiyo, nina waruhusu Waheshimiwa Diana Chilolo na Fuya Kimbita waulize maswali mafupi, jamani siyo dibaji tena ndefu. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, matatizo ya umeme yanafanana karibu maeneo mengi hapa nchini, na kwa kuwa,

Serikali kupitia maswali yangu na jitihada za Wabunge wa majimbo Mheshimiwa Missanga na Mheshimiwa Chiligati, iliahidi kupeleka umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* kutoka Manyoni – Kilimatinde - Chikuyu na Kintinku na kupeleka umeme Sepuka, Singida Vijijini na kupeleka barua rasmi kabisa na Wabunge wakawasomea wananchi.

Je, Serikali itakuwa imetenga fedha hizo kupitia Bajeti hii tunayoijadili sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya umeme ya Tanzania hayafanani maeneo yote, lakini kwa hili la Singida kweli linafanana na hili la Chakwale, kwa sababu tayari umeme umefika pale Manyoni na kuna jitihada za makusudi za kuongeza uwezo wa upatikanaji wa umeme kwenye kanda nzima ile ya Kati ili hata usambazaji wa maeneo haya ambayo anayataja Mheshimiwa Mbunge, ambayo kusema kweli ni makubwa kama hili la Manyoni-Kilimatinde kwenda kule Chikuyu na Kintinku, nadhani ni kama kilomita sabini hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ni mradi mkubwa lakini na huu mradi wa Sepuka wa Mheshimiwa Missanga, naomba niseme kwamba ameufuatilia kwa karibu sana, nadhani unatokea pale barabarani, ni kama kilomita 12 au 13 hivi.

Mheshimiwa Spika, miradi yote hii miwili naomba nimwambie Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Chiligati, Mheshimiwa Missanga na Mheshimiwa Paul Lwanji ambao wanahusika na maeneo haya. Naomba tusubiri upatikanaji wa fedha kama tutakavyopitisha katika Bajeti ili tuone utekelezaji kwa mwaka huu utakwendaje.

Kusema kweli kama utekelezaji wa mradi huu umechelewa, ni kwa sababu ya pesa ambayo ilikadiriwa kupatikana *REA* na ambayo haikupatikana yote. *(Makofi)*

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Ningeomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba, kwa vile kule wilayani Hai hali hii pia inatukabili, na tunahitaji umeme katika maeneo ya Longoi *Secondary*, Mungushi na maeneo mengine ya Machame Kusini, na shida kubwa baada ya kufuatilia pale wilayani niliambiwa kuwa ni shida ya nguzo, nikaenda mkoani nikaambiwa tatizo la nguzo ni la nchi nzima.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia nini sasa, tutarajie kuzipata hizo nguzo ili ile miradi ya umeme iweze kutekelezwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Archt. Fuya G. Kimbita, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna tatizo la nguzo sasa hivi kwa maeneo mengi ya nchi hii kwa sababu ziko nguzo za aina mbili. Ziko zile nguzo ambazo ni ya *high tension.* Aina hii haina tatizo, miti hiyo iko mingi na imekomaa vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo sasa hivi ni kwenye hivi vinguzo vidogovidogo hivi ambavyo ndivyo vinabeba nyanya hizi za kilovolt 0.4 ambazo kwa sababu ya mipango mipana sana ya usambazaji, mahitaji yake yamekuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimeulizia *TANESCO* nadhani wiki iliyopita nikaambiwa tatizo lililokuwepo ni kwamba, hizi nguzo ndogo ndogo hazikomai vya kutosha kwa hiyo, zikiwekwa kwenye maeneo yake vinakaa mwaka mmoja, miwili zinaoza badala ya kukaa kama miaka 12 au 15. Kwa hiyo, kununua nguzo ukaiweke kwa miaka miwili wakati uhai wake ungekuwa miaka 12 ni hasara kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mipango mbalimbali inayofanywa ambayo mmoja wapo ni kuangalia pia uwezekano wa kuweka nguzo labda za simenti au nguzo za njia nyingine. Lakini, kwa ujumla katika mipango ambayo tumewahimiza *TANESCO* ni kuongea na hawa Wazabuni wa hizi nguzo ili waanze kuzitengeneza kwa muda mrefu kwa sababu nguzo inachukua kama miaka mitatu, minne kutoka kuipanda mpaka kukomaa.

Lakini pia, kufanya *treating* inayostahili, siyo ya kulipua lipua ili ukiiweka nguzo ikae japo miaka 10 unajua umemalizana na hilo tatizo badala ya kuanza kuweka nguzo kila baada ya mwaka mmoja au miwili.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo hili linashughulikiwa na *TANESCO* na mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuwa ni tatizo kubwa tutalitolea maelezo hapa wakati wa kutoa maelezo ya Makadirio ya Wizara yetu ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Na. 85

**Mahitaji ya Umeme Lupa**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Serikali kupitia Bajeti yake ya mwaka 2009/2010 imetenga fedha kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji vya Lupa, Sangambi na Mlimanjiwa Wilayani Chunya na Mkandarasi wa kujitegemea wa kufanya kazi hiyo tayari amepatikana:-

Je, ni kampuni gani imepewa zabuni hiyo na kazi itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vya Lupa, Sagambi na Mlimanjiwa Wilayani Chunya ni mojawapo ya miradi ambayo Wakala wa Nishati Vijijini ametenga fedha katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya utekelezaji.

Mradi huu utahusisha ujenzi wa kilomita 44 za njia ya umeme msongo wa kilovolt 33, kilomita 4 za njia ya umeme msongo wa kilovolt 0.4 pamoja na ufungaji wa vituo vya kupoza umeme vinne (4) vyenye ukubwa wa kVA 100 kila kituo.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wanakamilisha mkataba na mkandarasi aliyechaguliwa ambaye ni *Rousant International* kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu. Inategemewa kuwa ujenzi wa njia za umeme utaanza kabla ya mwisho wa mwezi Julai, 2010. Mradi unatarajia kuchukua kama miezi 12 kukamilika tangu kuanza ujenzi wake.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, uzoefu umeishaonesha kuwa miradi hii ya ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kV 33 ikiishakamilika *TANESCO* inahemewa na ongezeko kubwa sana la wananchi wanaohitaji umeme kutokana na uhaba unaojitokeza mara kwa mara wa *transformer* za kupoza umeme, vilevile nguzo za kutosha na nyaya za usambazaji kama ambavyo wananchi katika kata za Ipinda, Makwale na Matema Wilayani Kyela wanavyohangaika baada ya ujenzi wa njia ya kilovolt 33 kukamilika.

Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na ongezeko dhahiri litakalotokea la wataka umeme wa vijiji vya Upendo, Mtambe, Namamba na Kisalasi jimboni Lupa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Mwakyembe kwamba hilo swali lenyewe emelieleza na anaeleza haswa tatizo linalotukabili ambalo hapa katika suala la Wilaya ya Chunya limejitokeza pia, kwamba kupeleka tu umeme

hapa kwenye vijiji vya Lupa ni kilomiya 44 na hizo kilomita 44 hizo ni kV 33 halafu ukifika pale Lupa ule usambazaji tu pale ni kilomita nne na ni kV 0.4.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyosema wakati ninajibu swali la mwanzo, tatizo la usambazaji ni tatizo la nguzo, *transformer*, waya husika na pia ni tatizo la mita. Kwa hiyo, katika kuangalia uzoefu wa nchi zingine tumegundua kwamba wenzetu wanahimiza uwekezaji wa makusudi ili pale ambapo panaonekana kwamba, pana mahitaji makubwa ya vifaa kama hivi viwanda vidogovidogo hivi vijitokeze pale pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kwamba tumepata maombi ya wawekezaji mbalimbali wa kuja kuwekeza kwenye masuala ya mita, *cables* na vitu vingine kama hivyo na tunaamini kwamba uwekezaji huu ukifanywa hapa nchini inawezekana kabisa kwamba hata gharama hizo za usambazaji na pia upatikanaji wa vifaa ukawa na ubora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, Bukene kuna tatizo pia?

**MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU:** Be!

**SPIKA:** Bukene nako!

**MHE. TEDDY L. KASELLA – BANTU:** Ndiyo, na ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa tatizo la umeme wa kutoka Nzega kwenda Bukene linafanana sana na swali la msingi lililoanza hapo awali, na kwa kuwa watu wanaofanyakazi wako tayari kuweka vifaa vya umeme kwa ajili ya kazi ya kutandaza umeme kutoka Nzega – Itogo-Bukene na kwa kuwa vifaa viko tayari vimewekwa pale kwenye *godown* la Igembesabho na *engineer* yupo na hatua hizo zinaleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Bukene.

Ni lini basi kazi hii itakwisha ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Bukene wanawasha umeme katika jimbo hilo?

**SPIKA**: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali ambalo ni jepesi tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwamba, ameeleza kwamba kazi hiyo iliishaanza kwa sababu amezungumzia mradi huo mara nyingi tu hapa Bungeni na amekuja Wizara ya Nishati pale mara nyingi na *TANESCO* kufuatilia mradi huu. Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, huu mradi wa Nzega-Itobo na Bukene kama vifaa vimeishafika, mimi nina amini na mafundi wako wa palepale Tabora lakini pia kutokea ofisi kuu ya kanda

wakina Bwana Kingo na nani, kutoka kule Mwanza, nina amini kabisa kwamba wanalifuatilia kwa karibu.

Labda nimhakikishie Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwamba, nitawasiliana nao, nijue ile ratiba ya utekelezaji inakwendaje halafu nitakupatia jibu ili na wewe uwafikishie taarifa wananchi wa Bukene waweze kuutarajia umeme huo kwa wakati ambao tunatarajia utekelezaji utafikisha umeme huo Bukene.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita, na maswali sasa yamekwisha.

Matangazo, nikianza na wageni: Waheshimiwa Wabunge tangu jana tumempokea mgeni mashuhuri kutoka Jamhuri ya Rwanda, naye si mwingine ila ni Mheshimiwa Dr. Vincent Biruta, Rais wa Bunge la Rwanda. Wenzetu wana *Chambers* mbili, yaani Wawakilishi na pia *Upper Chamber.*

Kwa hiyo, yeye Dr. Biruta ni Rais wa ile *Upper Chamber* ambayo inaitwa *Senate* kule Rwanda na sasa nafurahi kuweza kumwomba asimame. *(Makofi)*

*Please, Dr. Biruta if you can stand up please. We feel very much honored for you having taken trouble to travel all the way to Dodoma This proves how close Rwanda and Tanzania are in every respect and this visit with your other Members of Parliament whom I will shortly introduce, we value and we hope that you will have a nice days in our country. (Applause)*

Yupo Mheshimiwa Fatma Ndangiza ambaye ni Balozi wa Rwanda hapa nchini, *welcome once again*. Aah kwako wewe niseme karibu tu, kwa sababu hata mume wako ni Mtanzania, kwa hiyo unakijua vizuri Kiswahili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wafuatao ni Mheshimiwa Dr. John Baptist Msemakweli - Mbunge. Jina hili utaona kama ni la Tanzania tu, Msemakweli, karibu sana Mheshimiwa. Yupo pia Mheshimiwa Gahondogo Athanasie, Mbunge, wenzetu Rwanda wanazingatia sana jinsia, huwezi ukawa na msafara ambao utakuwa na jinsia moja tu. Tunawashukuru na kuwapongeza sana kwa mafanikio waliyofikia katika masuala ya jinsia. Ni mafanikio makubwa. Mwisho Ndugu Nsazimana Alexis, Mtumishi wa Bunge ambaye ndiye Katibu wa Msafara, yule pale, karibu sana. (*Makofi*)

Jana baada ya kumpokea Mheshimiwa Dr. Biruta, wakati tunakula naye chakula cha jioni alitueleza kwamba, yeye alifika hapa wakati wa uzinduzi wa ukumbi huu mwaka 2006 lakini, jana alipokuwa anawasili kwa ndege kutoka Dar es Salaam alishangazwa sana na majengo ambayo baadaye alielezwa ndiyo Chuo Kikuu kipya cha Dodoma, ameshangaa sana, amesema ah, nyie Watanzania mnafanya mambo yenu kimyakimya lakini mambo makubwa kabisa. Kwa hiyo, nilitaka mjue hilo. (*Makofi*)

Karibu sana, tutakuwa naye leo na kesho, ataonana na viongozi mbalimbali na Kamati mbalimbali.

Wageni wa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, masuala ya Muungano, sijui naye anagombea Urais wa Zanzibar lakini nadhani ana wageni wake na Mheshimiwa Dr. Batlida Buriani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni wafuatao.

Yupo Ndugu Ruth Mollel, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, yule pale karibu sana mama Mollel. Yupo Raymond A. Moshy, Mkurugenzi wa Utawala wa Ofisi ya Makamu wa Rais, yupo Seif Msongole, Katibu wa Makamu wa Rais, yupo Ndugu Juma H. Mkima, Mhasibu Mkuu, karibu sana. Yupo Joan Mbuya, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, yule pale karibu mama, yupo Richard Muyungi, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira, yule pale, Baraka Rajab, Kaimu Mkurugenzi wa Masuala ya Muungano, ahsante sana. Ndugu, Bonaventura Baya, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC na Jerome Assey, Mshauri wa Makamu wa Rais, Uchumi - yule pale, karibuni sana! *(Makofi)*

Wapo wageni mahususi wa Mheshimiwa Waziri Dr. Batlida Buriani, ambao ni wanafunzi 70 wa kidato cha sita kutoka *Edmund Rice Secondary School*, Arusha na wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha *St. Johns* ambao ni wakazi wa Arusha wakifuatana na Walimu wao ambao ni Ndugu Zablon Mtani, naomba wasimame pamoja na wanafunzi, Ndugu Charles Benjamin apunge mkono, yule Mwalimu, yule pale na ndugu Tabu Mwalimu, apunge mkono tafadhali! Ahsante sana wageni wetu kutoka Arusha. Naona Mheshimiwa Waziri Buriani anapiga kasi, kwa kweli mambo mwaka huu .........! (*Kicheko*)

Ahsanteni sana vijana tunawatakia mafanikio katika mafunzo yenu. *(Makofi)*

Pamoja na hao wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri, Dr. Buriani ambao ni Viongozi wa akina mama wanaohamasisha matumizi ya Makaa ya Mawe kwa kupikia ambao ni Mama Hellena Mwambegele, huyu ni Mjasiriamali, maarufu sana, yuko wapi huyu, aah, yule pale mkono wa kulia, ahsante sana Mama Mwambegele!. (*Makofi*)

Mama Magreth Kibuzi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Dodoma, yule pale ahsante sana! Ndugu Deodatus Buhuma, Mweka Hazina, ahsante sana, Ndugu Bahati Gabriel na Ndugu Hakimu Abdul Aziz, wawili hao ni Wajumbe, karibuni sana!

Waheshimiwa Wabunge, halafu wapo wanafunzi 25 wa shule ya Sekondari ya *City* Dodoma, sijui kama walipata nafasi, shule ya *City* Dodoma, naomba kama mpo msimame, labda hapana! Wapo wanafunzi 20 na Walimu watano (5) kutoka shule ya Makongo *High school* ya Dar es Salaam, naomba wasimame pale walipo, aah wale pale. *(Makofi)*

Karibuni sana Wanafunzi na Walimu wa Shule maarufu sana ya *Makongo High*, imekuwa ni msaada sana kwa taifa kwa sababu baadhi ya wanamichezo wazuri sana wametoka hapo. Natumaini mtaendeleza juhudi hizo. Pia wapo na wanataaluma siyo michezo tu, tunawatakia mema katika masomo yenu.

Yupo Ndugu Martha Shindika, kutoka Sengerema, Mwanza ambaye hakutamkwa yeye ni mgeni wa nani. Mama Shindika, yule pale ahsante sana! Nadhani atakuwa ni mgeni wa Mheshimiwa Ngeleja tu maana yake ndiye Mbunge husika. Bahati mbaya Waziri yuko katika ziara huko alikotumwa, karibu sana mama! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kutambulisha wageni. Sasa ni Mgeni wa Mheshimiwa Shally Raymond, ni Bi. Masia ambaye ni Diwani wa Kata ya Mamsera kule Rombo, Diwani yule pale ahsante sana! Sijui kama Mheshimiwa Shally Raymond umewasiliana na Mheshimiwa Mramba, maana yake mambo haya Wanawake mmekuja juu sana nyie! *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, ni Ndugu Elias Kenyunko, anayetokea Serengeti jimboni kule. Lakini pia ni mwanafunzi wa mwaka wa pili, Chuo Kikuu cha Dodoma, karibu sana na tunakutakia mema katika mafunzo.

Mwisho, lakini siyo mwisho kwa umuhimu, ni wageni wa Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, ambaye pia ni Mbunge wa Urambo Magharibi na Mheshimiwa Spika wa Bungew hili. Wageni hawa ni Wajumbe wote wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Urambo, CCM wakiongozwa na Mheshimiwa Gulamsen Juma Dewji, Mwenyekiti, naomba Mwenyekiti kwanza asimame, ahsante karibu sana Mwenyekiti. (*Makofi*)

Ndugu Alphonce Kinamhala, Katibu wa CCM Urambo, Ndugu Anna Magowa, Mkuu wa Wilaya, Ndugu Adam Malunkwi, Mwenyekiti wa Halmashauri, Ndugu Emmanuel Gembe, ni Mjumbe lakini pia ni Katibu wa Uchumi wa Mkoa, siyo wa Wilaya, wa Mkoa wa Tabora, yule pale.

Ndugu Peter Busagwe, Katibu Mwenezi, Ndugu Weston Chokala, Katibu wa Uchumi, Wilaya ya Urambo, Ndugu Rosalia Shija, Katibu wa Wazazi, Ndugu Martha Susu, Mwenyekiti wa UWT Urambo, Bi. Tausi Sungura, Katibu wa UWT Urambo, Elias Kaseko, Mwenyekiti wa Wazazi, Abbas Nkoningo, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana, Mheshimiwa Mashaka Kayanda, Diwani ambaye pia ni Mjumbe, Mheshimiwa Mussa Ludete, Diwani na Mjumbe, ndg. Yasin Luswaga, Mjumbe, Mheshimiwa Abdallah Magohe, ambaye ni Diwani na Mjumbe na Ndugu Robert Mwijage ni Katibu Msaidizi

na Mhasibu wa Wilaya, karibuni sana! Sisi Wabunge wenu wawili tunafurahi sana kuwakaribisha hapa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuunda Wilaya mpya ya Kaliua na bado tuna maombi mengine tutazungumza zungumza nanyi, kwa sababu tunahitaji kuweka Wilaya yetu ikae sawa. Kwa hiyo, tutakutana hivi punde, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Basi Waheshimiwa kutokana na wageni wote hao nalazimika kuondoka kitini. Nimwombe Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kuja kuendelea na shughuli nyingine. (*Makofi*)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne. S. Makinda) Alikalia kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kazi. Ningependa kutoa salaam za Mheshimiwa Jenista Mhagama, tuliyekwenda kushiriki mazishi ya Mume wake, mazishi yalikwenda vizuri, sasa na yeye pia anafanya mambo ya kifamilia tu. Ahsanteni sana kwa salamu zenu, amezipokea kwa upendo mkubwa sana na Ofisi ya Bunge ilitoa msaada mkubwa na kumsaidia katika shughuli hii yote, ahsanteni sana! (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi Kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 - Ofisi ya Makamu wa Rais

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema kwa kutujalia uhai hadi kufikia siku ya leo. Aidha, mimi binafsi na kwa niaba ya Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kuwa na imani nasi na kutupa dhamana ya kuwa Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake yaliyowezesha Ofisi yetu kutekeleza vizuri majukumu yake. Pia, namshukuru Mheshimiwa Samwel John Sitta, Spika wa Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa kasi, umakini na kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. Napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyeketi wake Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa ushauri, maoni na ushirikiano walioutoa katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ofisi imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itazingatia yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) kwa ushirikiano na michango yao katika kuimarisha hoja hii. Pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri mwenzangu Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Waziri wa Nchi, Mazingira, kwa ushirikiano na utendaji wake thabiti na makini katika kutekeleza majukumu ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru watendaji wakuu na wafanyakazi wenzangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bi. Ruth Hiyob Mollel, Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), Wakuu wa Vitengo na Wafanyakazi wote kwa michango waliyoitoa katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi kwa mafanikio na ufanisi mkubwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Uzini kwa kuendelea kunipa heshima na dhamana ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka kumi na tano. Aidha, kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, , Waziri wa Nchi, Mazingira, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa kuendelea kumpa heshima na dhamana ya kuwa Mbunge wao (Viti Maalumu) kwa kipindi cha miaka kumi. Tunaahidi kuendelea kushirikiana nao katika kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na hivyo kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene (CCM) na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (*CUF*), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kujiunga na Bunge lako Tukufu. Aidha, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kuteuliwa kwao kunathibitisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa utendaji wao ulio makini. Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, kwa kushinda uchaguzi mdogo katika jimbo la Biharamulo Magharibi kwa tiketi ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Mheshimiwa Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefariki dunia tarehe 31/12/2009. Marehemu Mzee Kawawa atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa uongozi imara na shupavu tangu enzi za kupigania uhuru wa nchi yetu hadi baada ya kustaafu rasmi katika shughuli za Serikali na alikuwa mhimili muhimu katika kutoa ushauri na maelekezo katika Serikali na Chama Tawala. Vilevile, natoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng’itu (CCM) aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa. Vifo hivi vimeleta majonzi makubwa kwa Bunge na Taifa letu kwa ujumla. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. (Amin)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali na Utekelezaji wa Dhana ya Kilimo Kwanza kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa ujumla wake, mipango hiyo ina lengo la Kukuza Uchumi, kuhifadhi Mazingira na Kupunguza Umaskini na hivyo kuleta Maisha Bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wake kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005, Ahadi za Serikali Bungeni za mwaka 2009/2010 na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake Ibara 143 ukurasa 167 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaelekeza kwamba, nanukuu:-“Ushirikiano wa kiuchumi na kijamii umeanza kuimarika na mfano mzuri wa ushirikiano huo umedhihirika katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF* katika Jamhuri nzima, Bara na Zanzibar. Katika kipindi cha Ilani hii CCM itazielekeza Serikali zote mbili kuanzisha miradi ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii ya pamoja, Visiwani Zanzibar na kuwashirikisha wawekezaji binafsi. Maingiliano ya kiuchumi ni njia muhimu ya kuimarisha Muungano”.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kumekuwa na maendeleo katika sekta za kiuchumi na kijamii kwa pande zote za Muungano kwani wananchi wamenufaika sana na miradi ya maendeleo iliyoandaliwa na kutekelezwa na pande zote mbili. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2005 kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa jamii wa kutumia fursa zilizopo kutekeleza na kufuatilia miradi ambayo inachangia kuboresha hali ya maisha, kwa kuzingatia viashiria vya malengo ya maendeleo ya milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Utekelezaji wa *TASAF* II umekuwa na mafanikio makubwa kwani jamii imeweza kuelewa malengo ya miradi inayochangiwa na *TASAF* hivyo, kuwa na mwamko na ari ya kushiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya Pili ya TASAF inatekelezwa katika Halmashauri 121 Tanzania Bara na Halmashauri zote za Tanzania Zanzibar. Fedha za kutekeleza *TASAF* II ni jumla ya dola za Marekani milioni 178.5 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 249.9. Kati ya fedha hizo, dola za Marekani milioni 15 sawa na shilingi bilioni 21 ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dola za Marekani milioni 13.5 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 18.9, ni nguvu za wananchi na dola za Marekani milioni 150 sawa na shilingi bilioni 210, ni mchango kutoka Benki ya Dunia. Kuanzia mwaka 2006 hadi Machi, 2010, *TASAF* ilitoa shilingi 161,386,382,189.33/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii 7,645. Kati ya miradi hiyo, miradi 7032 inatekelezwa Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi 152,894,964,286/= na miradi 613 inatekelezwa Tanzania Zanzibar kwa gharama ya shilingi 8,491,417,902/=. Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Tanzania – *MACEMP*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kuboresha usimamizi wa mazingira ya pwani na maliasili ya bahari kwa nia ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Mradi huu ni wa miaka sita na unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jumla ya shilingi bilioni 66 kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa *(International Development Agency – IDA*) ambalo limetoa mkopo wenye masharti nafuu kwa mgawanyo wa asilimia 60 sawa na shilingi bilioni 40 kwa Tanzania Bara na asilimia 40 sawa na shilingi bilioni 26 kwa Tanzania Zanzibar. Aidha, Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility* – GEF) umetoa msaada wa shilingi bilioni 13 kwa mgawanyo wa asilimia 50 Tanzania Bara na asilimia 50 Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji – *PADEP*. Lengo kuu la mradi huu ni kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya Kilimo na Mifugo, kuongeza pato la Mkulima na uhakika wa Chakula katika kaya na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini kijijini. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia iliyotoa shilingi bilioni 70 kwa mradi wote. Kwa upande wa Tanzania Bara mradi huu unatekelezwa katika Wilaya 32 kwa gharama ya shilingi bilioni 64 na kwa upande wa Tanzania Zanzibar mradi unatekelezwa katika Wilaya tisa kwa gharama ya shilingi

bilioni sita. Mradi ulitarajiwa kukamilika Desemba, 2008 lakini umeongezwa muda hadi Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa miundombinu unaendelea kufanyika pande zote mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na uimarishaji na ukarabati wa njia ya umeme kutoka Dar-es-Salaam hadi Fumba - Unguja. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa barabara tano za Pemba chini ya ufadhili wa Mfuko Maalumu wa Serikali ya Marekani *(Millenium Challenge Account – MCA*) yanaendelea. Ujenzi wa miundombinu hiyo utagharimu shilingi bilioni 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufuatilia utekelezaji wa kila siku wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano ili kudumisha Muungano na ushirikiano wa Serikali zote mbili. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliratibu vikao vitano vya maandalizi ya kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya Muungano. Vikao hivi vilifanyika katika ngazi ya Mawaziri wa SMT na SMZ tarehe 3 Mei, 2010; Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ tarehe 12 Aprili, 2010. Vikao vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano vilifanyika tarehe 24 Oktoba, 2009, tarehe 27 Aprili, 2010 na tarehe 20 Mei, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Juni, 2010 kilifanyika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja tisa zilijadiliwa na kati ya hizo, hoja mbili zimefikiwa makubaliano na hati za makubaliano zilisainiwa na Mawaziri husika kutoka Serikali zote mbili katika kikao hicho kilichofanyika Zanzibar. Hoja hizo ni Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar na Utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na *International Maritime Organisation* (*IMO*). Aidha, hoja nyingine zimefikia hatua nzuri ya utekelezaji kama ifuatavyo:-.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni miongoni mwa mambo yaliyopatiwa ufumbuzi katika jitihada za kutatua kero za Muungano. Awali, Sheria Na. 1 ya mwaka 1998 ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu ilikuwa haitumiki. Marekebisho ya Sheria yalipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Februari, 2007, kifungu cha 5(a) cha Sheria hiyo kilirekebishwa ambapo Katibu Mkuu, Afisi ya Waziri Kiongozi na Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Tawala za Mikoa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wamejumuishwa katika Kamati ya utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi. Kwa sasa Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ni moja. Hata hivyo, Sheria hiyo bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi, hivyo Sekta husika

zimekubaliana kutumia utaratibu wa muda ili shughuli za mamlaka ziweze kuendelea hadi Sheria hiyo itakaporidhiwa na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya fedha yameendelea kushughulikiwa ipasavyo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kila mwaka. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kunufaika na asilimia 4.5 ya mikopo ya misaada ya kibajeti (*General Budget Support – GBS - C*) ambayo ilikuwa haipati kwa miaka iliyopita. Vile vile, suala la misamaha ya mikopo ya fedha kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (*International Monetary Fund* - IMF) limeshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata fedha za misamaha hiyo. Pia, suala la uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi limepatiwa ufumbuzi na sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa ndani ya nchi. Aidha, SMZ inaweza kukopa nje ya nchi chini ya udhamini wa SMT.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. Kulikuwa na tatizo la ukadiriaji vibaya wa thamani za bidhaa uliokuwa ukifanywa na baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kusababisha malalamiko kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara. Suala hili limepatiwa ufumbuzi. Bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za forodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zitahesabika kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika kuhakikisha kuwa tatizo hilo halijitokezi tena, Mamlaka ya Mapato Tanzania itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji watakaobainika kutumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani za bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya miradi ya Zanzibar kujumuishwa katika Miradi ya Kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliainisha miradi minane kwa ajili ya kuombewa ufadhili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi hiyo inaendelea kushughulikiwa kwani kati ya miradi hiyo, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar umepata mkopo wa shilingi bilioni 95 kutoka Benki ya *Exim* ya China. Aidha, Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba umeingizwa katika miradi ya kipaumbele ya Tanzania inayoombewa ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*). Miradi mingine iliyoainishwa iko katika hatua mbalimbali za kuombewa ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje. Kulikuwa na malalamiko kutoka Zanzibar kuwa haipati nafasi ya kutosha ya kuwa na mashirikiano ya kiuchumi na taasisi za Kimataifa. Suala hili limepatiwa ufumbuzi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashirikishwa katika masuala ya Kimataifa. Aidha, imeagizwa kuwa, ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yote ya Kimataifa uanzie katika hatua za awali na hii itekelezwe na Wizara zote. Hata hivyo, ili utekelezaji wa suala hili uende vizuri, Kamati ya wataalam imeundwa ili iweze kutayarisha mwongozo kuhusu ushirikishwaji wa SMZ katika masuala yote ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya uwiano wa nafasi za ajira kwa wananchi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano. Suala hili linaendelea kufanyiwa kazi. Kamati

ya wataalam inayojumuisha Makatibu Wakuu kutoka pande mbili za Muungano inapitia Sera na Sheria za ajira. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine yanayoendelea kushughulikiwa ni namna ya kugawana gharama na faida ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kuhusu Taarifa ya Tume ya Pamoja ya Fedha juu ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Masuala haya yamewasilishwa kwa Serikali zote mbili yakisubiri maelekezo kutoka ngazi za juu za uongozi ili kupatiwa ufumbuzi. Aidha, hoja za mgawanyo wa faida ya Benki Kuu na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kushughulikiwa. Napenda kuwaeleza Watanzania kwamba, ni vema wakaelewa kuwa Serikali zetu hazijakaa kimya kwani zipo hoja ambazo zinatakiwa zipate mijadala ya kina ili kufikia uamuzi kwa faida ya pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano vinapatiwa ufumbuzi, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano angalau mara tatu kwa mwaka. Vikao hivi vitatanguliwa na vikao vya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi imeratibu gawio la asilimia 4.5 litokanalo na misaada ya Wahisani na mikopo ya kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Bunge liliidhinisha shilingi 50,214,131,000/= kama mgao wa asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia tarehe 11 Juni, 2010 shilingi 51,237,000,000/= zilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni asilimia 102 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi cha gawio huongezeka au kupungua kutegemea na kiasi cha misaada na mikopo inayopatikana kwa mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yetu imefuatilia utekelezaji wa ahadi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika shughuli za maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kipindi hiki shilingi 1,600,000,000/= zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Amani hadi Mtoni huko Zanzibar; shilingi 3,250,000,000/= kwa ajili ya mradi wa umeme Pangani hadi Pemba na shilingi 200,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa jenereta wakati wa tatizo la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na.16 ya mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, inamtaja Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kuwa ndiye mratibu wa Mfuko huu kwa upande wa Zanzibar. Kwa mwaka huu wa fedha Ofisi ilipokea shilingi 1,230,032,000/= kwa ajili ya mikoa ya Zanzibar. Fedha hizo zimepelekwa Wizara ya Fedha na Uchumi ya SMZ ili zigawanywe kwa Majimbo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi, kijamii, na kisheria katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi imefanya jitihada za kuhakikisha kuwa, jamii inakuwa na uelewa wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Ofisi iliandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 10,000 za vipeperushi, nakala 10,000 za Jarida la Muungano Wetu, kalenda 2000 za mwaka 2010, *Wheel Covers* 500 na fulana 300 zenye ujumbe wa kudumisha Muungano. Aidha, semina moja kuhusu masuala ya Muungano kwa watumishi na viongozi wapatao 60 wa Serikali zote mbili iliandaliwa na kufanyika tarehe 11 hadi 12 Desemba, 2009, Bagamoyo. Pia, elimu ilitolewa kwa Umma katika maonesho ya Nane Nane ya mwaka 2009 yaliyofanyika Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano kupitia Redio, Televisheni, Magazeti, Majarida, vipeperushi, Semina, Maonyesho ya Kitaifa na machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kushughulikia masuala ya Muungano, Ofisi inaratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kisera, kubadilishana utaalam na wataalam, ushiriki katika masuala ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliratibu vikao tisa vya Wizara za SMT na SMZ katika Sekta za Mawasiliano na Uchukuzi, Miundombinu, Kilimo, Mifugo, Elimu, Fedha na Uchumi, Habari, Utamaduni na Michezo, Tawala za Mikoa, Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi iliratibu ziara za Mawaziri wa Serikali za pande zote mbili kutembelea shughuli za maendeleo katika kipindi hiki cha utekelezaji. Waziri wa Miundombinu alifanya ziara Chake Chake, Pemba tarehe 15 - 16 Novemba, 2009 kwa ajili ya kutembelea miradi ya Miundombinu; na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano alifanya ziara Unguja na Pemba kuanzia tarehe 14 - 20 Januari, 2010 kwa lengo la kutembelea Taasisi za Muungano pamoja na Miradi ya Pamoja kati ya SMT na SMZ. Aidha, Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi alifanya ziara Dar es Salaam kuanzia tarehe 12 - 13 Machi, 2010 kukagua miradi mbalimbali ya Maendeleo na Mkoani Iringa tarehe 17 -19 Machi, 2010 na kushiriki katika ufunguzi wa mashindano ya mpira wa miguu ya Kombe la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara, Idara, Taasisi na Asasi zisizo za Muungano za pande mbili zitakutana kujadili masuala ya kisekta kwa kubadilishana uzoefu, ujuzi, utaalam, mafunzo na ushiriki katika masuala ya kimataifa angalau mara mbili kwa mwaka ili kuongeza maelewano na mshikamano baina ya wananchi wa pande mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio tuliyoyapata katika kutekeleza masuala ya Muungano, zimejitokeza changamoto zikiwemo za kuelimisha umma kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Serikali inatambua kuwa zipo changamoto katika kumaliza vikwazo vinavyokwamisha shughuli za Muungano. Dhamira ya Serikali zetu mbili ni kuondoa mambo yanayoleta vikwazo kwa kuhakikisha yanatatuliwa ipasavyo ili Muungano uendelee kuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi endelevu ya mazingira. Maisha ya wananchi wote yana uhusiano wa karibu sana na mazingira; hatima ya maisha yetu na vizazi vijavyo yatategemea uhusiano mzuri kati yetu na mazingira. Kwa mantiki hii, katika kukabiliana na changamoto za mazingira, Serikali imeendelea kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005, Sera, Mikakati, Sheria na Kanuni zinazolenga kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali na maliasili katika shughuli zetu za kila siku, kwa lengo la kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu taifa letu limekumbwa na majanga na athari mbalimbali za mazingira katika maeneo mengi nchini. Mifano halisi ni mafuriko katika Wilaya za Kilosa na Mpwapwa, maporomoko ya udongo katika Wilaya ya Same na hali ya ukame iliyosababisha vifo vingi vya mifugo na uharibifu wa mazao katika mikoa ya Manyara na Arusha. Ofisi ya Makamu wa Rais inachukua fursa hii kuwapa pole wananchi wote waliokumbwa na majanga haya. Majanga haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira na yanazidi kutukumbusha umuhimu wa kuchukua hatua za dhati za kuhifadhi mazingira. Serikali itaendelea kutekeleza programu mbalimbali za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kukuza ubunifu wa kuhimili athari hizi; kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira na ile ya kupambana na changamoto za athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kushirikisha wadau wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake. Ibara ya 112 ukurasa wa 138-139 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaelekeza kwamba, nanukuu;-

(a) “Kuendeleza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa wao kuhusu hifadhi ya mazingira.”

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kukabiliana na uharibifu wa mazingira, Ofisi imeendelea kuratibu na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuandaa na kusambaza Kanuni, Miongozo na Mikakati inayolenga katika hifadhi na usimamizi wa mazingira. Mikakati hii imesaidia katika kukuza uelewa wa jamii na kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Elimu ya Mazingira kwa Umma wakati wa maadhimisho na maonesho yanayohusu Siku ya Mazingira Afrika,

Siku ya Wakulima (Nanenane), Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Ozoni Duniani na Siku ya Wanawake Duniani. Katika maadhimisho haya, elimu ya mazingira ilitolewa kwa kutumia vipeperushi nakala 10,000; shajara nakala 1,000; vitenge doti 5,000; fulana na kofia 20,000; mabango 50 na vitini nakala 10,000; vikundi 10 vya sanaa; vipindi maalum 30 vya luninga na 30 vya Redio; makala maalum 25 na mahojiano 15 na maonesho ya matumizi ya majiko banifu, nishati mbadala itokanayo na briketi (*briquettes*) za makaa ya mawe na makapi ya mazao (ndizi, kahawa, katani). Ofisi imetumia fursa hii kutoa elimu kwa umma kwa kuandaa na kusambaza shajara na vitini vyenye ujumbe mbalimbali kuhusu utunzaji wa mazingira.

Vile vile, elimu ya mazingira ilitolewa katika vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa 19, na semina elekezi mbili, kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya. Elimu ya mazingira ilitolewa pia kwa wadau mbalimbali wakati wa zoezi la ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji.

Warsha nne ziliendeshwa kwa Sekta Binafsi na Asasi zisizo za Kiserikali kuhusu miongozo na utekelezaji wa miradi ya kupunguza Gesi Joto na kuleta Maendeleo Endelevu (*Clean Development Mechanism - CDM*). Aidha, yalitolewa mafunzo ya udhibiti wa kemikali zinazomong’onyoa tabaka la hewa ya Ozoni kwa wadau 120 ambao ni mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi, maofisa forodha na waratibu wa mazingira.

(b) “Kuhamasisha na kuwezesha utumiaji wa matanuri ya kisasa ya kuchomea mkaa yenye sifa ya kupunguza upotevu wa miti”

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2009/2010 Ofisi kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matanuri ya kisasa yanayotumia kuni kidogo na yanayotumia nishati mbadala kama mabaki ya mbao na pumba za mpunga kwa lengo la kupunguza matumizi na upotevu wa miti. Katika kipindi hiki, vikundi vya wachoma mkaa vitatu katika Wilaya za Rufiji, Handeni, Kibaha, Monduli, Kisarawe, Morogoro, Muheza, Hai, Rombo na Mwanga vilipata mafunzo kuhusu teknolojia banifu za uchomaji mkaa zikiwemo *Half Orange* na *Casamanche*. Aidha, wakulima, taasisi zisizokuwa za Kiserikali na makampuni yameendelea kuhamasishwa kuanzisha mashamba ya miti kwa lengo la kupunguza matumizi ya misitu ya asili nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti kuhusu matumizi ya makaa ya mawe kwa kupikia zinaendelea kufanyika, chini ya uratibu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Tekinolojia (*Commission for Science and Technology* - COSTECH), ili kuhakikisha matumizi yake yanakuwa salama kwa mazingira na afya ya binadamu. Matokeo ya awali ya tafiti hizi yanaonesha kuwa makaa ya mawe huzalisha gesi zinazoweza kuathiri afya ya binadamu kwa mfano Salfa Dioksaidi (*Sulphur dioxide*). Hivyo, tafiti hizi zinalenga kutafuta njia ya kupunguza viwango vya gesi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamasisha matumizi ya majiko yenye kutumia mkaa/kuni kidogo. Ofisi kwa kushirikiana na makampuni binafsi na vikundi vya kijamii imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia majiko banifu kwa matumizi ya nyumbani. Uhamasishaji huu umefanyika katika maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa kama vile Siku ya Wakulima - Nanenane, Siku ya Mazingira ya Afrika na Siku ya Mazingira Duniani. Katika hatua ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, Ofisi kwa kushirikiana na *TaTEDO* ilisambaza majiko banifu 6,000 kwenye kaya katika mkoa wa Kilimanjaro. Mradi huu unalenga kupata ufadhili unaotokana na soko la biashara ya gesi ukaa.

Aidha, mradi wa kuhamasisha matumizi ya teknolojia banifu za nishati umesambaza majiko banifu takribani 32,000 kwenye mikoa ya Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora, Mwanza na Rukwa. Vile vile, Ofisi imeanza kuhamasisha matumizi ya gesi asilia katika taasisi, mashule na majumbani hususan katika maeneo ya mijini. Aidha, Ofisi imeanza mazungumzo na makampuni yanayouza majiko na gesi asilia ili waweze kuwakopesha watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga mwamko katika jamii wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na jinsi ya kukabiliana nayo. Elimu hii imetolewa kupitia warsha, vyombo vya habari, makala, maonesho na maadhimisho ya siku za Kitaifa zinazohusu mazingira. Aidha, warsha nane zilifanyika katika kanda saba Tanzania Bara na moja Zanzibar kuelimisha Maafisa Mazingira/Misitu/Maliasili wa Wilaya kuhusu Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji Miti na Uharibifu Misitu (MKUHUMI).

Vilevile, warsha moja ilifanyika kuelimisha Wakurugenzi na Makamishna wa Wizara za Nishati na Madini; Maliasili na Utalii; TAMISEMI; Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Maji na Umwagiliaji; Viwanda, Biashara na Masoko; na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu mpango huo. Aidha, Ofisi imeendelea kuhamasisha wananchi kupanda na kutunza miti na misitu, na kutumia majiko banifu kwa lengo la kupunguza kiwango cha hewa ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendeleza kampeni ya upandaji miti ambayo imekuwa ikifanywa kila mwaka na kuhakikisha kwamba miti inayopandwa inatunzwa ipasavyo na kuhimiza tabia ya kutokukata miti ovyo"Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya upandaji miti. Kwa mujibu wa taarifa ya kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 jumla ya miti 190,988,377 ilipandwa na miti 146,539,424 iliota sawa na asilimia 77 ya miti iliyopandwa. Jumla ya Wilaya 21 zimevuka lengo la kupanda miti 1,500,000, lililoainishwa kwenye Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa elimu kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa wananchi"Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia warsha, makala, vyombo vya habari na maonesho ya maadhimisho mbalimbali. Aidha, mafunzo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yalitolewa kwa Wataalam wa Mazingira katika Mikoa ya Arusha, Manyara na Kigoma. Lengo kuu la mafunzo haya lilikuwa ni kuainisha majukumu yao katika utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka ngumu ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, makala katika magazeti, majarida na kwenye maadhimisho ya sikukuu za Kitaifa na Kimataifa zinazohusu mazingira. Vipindi sitini kuhusu wajibu wa wadau katika udhibiti wa taka vilirushwa kupitia vituo vya televisheni vya *TBC, ITV* na *Star TV*. Ili kuwa na mpango endelevu wa usimamizi wa taka nchini, Ofisi imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka kwa kushirikiana na wadau na utekelezaji wake utaanza rasmi mwaka huu wa fedha. Vile vile, Ofisi imekamilisha makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuboresha usimamizi wa taka katika jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Hatua ya awali ya utayarishaji wa mpango mkakati wa Mazingira *(Environmental Management Master Plan*) umeanza na shughuli hii itakamilika katika kipindi cha miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vitakavyotumika taka ngumu kama malighafi. Ofisi kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya Kiserikali imeendelea kuhamasisha taasisi binafsi na viwanda kutumia taka ngumu kama malighafi. Aina ya taka ngumu zinazotumika ni pamoja na chupa za plastiki, karatasi, makopo na vyuma chakavu. Miongoni mwa viwanda vinavyotumia taka ngumu hizi ni pamoja na kiwanda cha chupa za plastiki cha Bakhressa, Morogoro *Plastics, Simba Plastics, TANPACK Tissues Limited* na *Aluminium Africa*. Aidha, viwanda vya sukari vya *TPC* Moshi na Mahonda Zanzibar, vimeanza utaratibu wa kutumia taka za miwa kwa ajili ya kuzalisha nishati. Kiwanda cha *TPC* Moshi kinazalisha Megawati 10 kwa ajili ya kuingiza katika gridi ya Taifa. Vile vile, kiwanda cha Katani *Limited* (Tanga) hutumia mabaki ya katani kuzalisha nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha 2009/2010 na malengo ya mwaka wa fedha 2010/2011. Serikali inatambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu katika kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005 na kufikia malengo ya Milenia na yale ya MKUKUTA. Ni dhahiri kwamba, kuna uhusiano mkubwa kati ya kiwango cha umaskini na uharibifu wa mazingira. Katika kukabiliana na changamoto za hifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi inaendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na Programu yake (*Environmental Management Act-Implementation Support Programme-EMA-ISP*). Katika kipindi hiki, Kanuni tatu za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ziliandaliwa, ambazo ni Kanuni za Usimamizi wa Mazingira dhidi ya Athari zitokanazo na Bioteknolojia ya Kisasa (*Biosafety Regulations*); Kanuni za Usimamizi wa Taka zenye Sumu (*Hazardous Waste Regulations*) na Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu (*Solid Waste Regulations*).

Aidha, Kanuni mbili zimejadiliwa na wadau na ziko katika hatua za mwisho za kukamilika. Kanuni hizo ni Kanuni za Wakaguzi wa Mazingira (*Environmental*

*Inspectors Regulations);* na Kanuni za Kudhibiti Viwango vya Kelele na Mitikisiko *(Noise Pollution and Vibrations Standards Regulations*). Kanuni nne ziko katika hatua za awali za maandalizi. Kanuni hizo ni Kanuni za Usimamizi wa Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu (*Persistent Organic Pollutants Regulations*); Kanuni za Usimamizi wa Majitaka (*Liquid Waste Management Regulations);* Kanuni za Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira (*Integrated Prevention and Control of Pollution Regulations);* na Kanuni za Mbinu za Kiuchumi za Kuhifadhi Mazingira *(Economic Instruments Regulations).*Hadi sasa kanuni 15 zimeandaliwa na zimesaidia sana katika kutekeleza sheria ya mazingira kwa ngazi mbalimbali.

Aidha, miongozo mitatu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliandaliwa. Miongozo hiyo ni Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Wizara, Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa (*Guidelines for Environmental Action Plan for MDAs and Local Government Authorities*); Mwongozo wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano na Mwongozo wa Kushughulikia Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuelimisha umma juu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Ofisi iliandaa na kusambaza kwa wadau nakala mia tano za kalenda na shajara elfu moja zenye ujumbe kuhusu hifadhi ya mazingira na majukumu ya wadau katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, vipindi thelathini vya luninga, thelathini vya redio na makala maalum ishirini na tano viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Ofisi imeendelea kutumia fursa ya maadhimisho na maonesho mbalimbali ya kitaifa katika kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Ofisi iliwasilisha Ripoti ya Kwanza ya Hali ya Mazingira katika Bunge lako Tukufu mwaka 2009. Katika kipindi hiki, Ofisi imekamilisha taratibu za kutafsiri Ripoti hii kwa lugha ya Kiswahili kwa kuandaa hadidu za rejea na kupata Wataalam. Tafsiri ya Ripoti hii itatoa fursa kwa wananchi wengi kuielewa na kuitumia katika kutekeleza mikakati na mipango ya hifadhi ya mazingira. Maandalizi ya ripoti ya Pili yameanza na itakamilishwa mwaka huu wa fedha.

Aidha, Ofisi imeteua Wakaguzi wa mazingira ishirini kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa mujibu Ibara ya 182 ya Sheria ya Mazingira. Wakaguzi hawa watadhibiti uchafuzi wa mazingira na kutoa adhabu za papo kwa papo kwa mujibu wa sheria. Mchakato wa uteuzi wa Wakaguzi wengine kutoka Taasisi na Wizara mbalimbali hadi katika ngazi ya Wilaya unakamilishwa. Serikali pia imeteua waratibu wa mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

Ofisi imefanya uperembaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji katika mikoa kumi na tatu na kuendesha semina kwa Waratibu. Ofisi inakamilisha taratibu za kuanzisha Mfuko wa Mazingira chini ya Ibara 213 ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kuongeza vyanzo vya fedha kwa ajili ya usimamizi wa mazingira. Aidha, mchakato wa uanzishaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira umeanza na tunatarajia Baraza hili litaanza kufanya kazi mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya Watendaji wa Serikali za Mitaa sitini walipewa mafunzo kuhusu kujumuisha masuala ya mazingira katika mipango ya Halmashauri zao. Mbinu hizo ni pamoja na jinsi ya kuendesha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira. Aidha, tafiti mbili zilifanyika kuhusu tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUKUTA na tathmini ya Sera mbalimbali zinavyojumuisha masuala ya mazingira katika maandalizi ya MKUKUTA II. Vile vile, elimu kwa umma kuhusu mazingira na umaskini ilitolewa kwa vipindi kumi vya redio, vipindi kumi vya luninga na kusambaza nakala elfu nne za Jarida la Umaskini na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinazohusu umaskini na mazingira zimeendelea kukusanywa na kusambazwa kupitia mtandao wa Tanzania *Socio-economic Database (TSED*). Mafunzo yalitolewa kwa wawakilishi themanini wa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) kutoka Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Mbeya, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, kuhusu uhusiano wa mazingira na umaskini pamoja na sera na sheria za mazingira, ardhi na maji. Katika kipindi hiki, mafunzo yalitolewa kwa Wanavijiji sitini wa maeneo kame katika Wilaya za Manyoni, Iramba na Monduli, kuhusu shughuli mbadala zinazoongeza kipato na zinazozingatia hifadhi ya mazingira kwa mfano, ufugaji wa kuku wa kienyeji, kutengeneza vikapu na mapambo na ufugaji wa nyuki.

Aidha, kufuatia ziara ya mafunzo katika maeneo kame ya Wilaya ya Meatu Mkoani Shinyanga, wanavijiji hawa wametenga maeneo ya hifadhi ya uoto wa asili (ngitiri), kiasi cha hekta 1,000 katika Wilaya ya Iramba na hekta 598 katika Wilaya ya Manyoni. Aidha, wawakilishi sita wa maeneo husika walishiriki katika maonesho ya biashara yaliyofanyika Dar es Salaam na Nairobi, Kenya ili kujifunza kwa vitendo. mbinu za kupata masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, chini ya Programu hii, kazi zifuatazo zitatekelezwa:- kuwezesha Wizara na Taasisi za Serikali kukusanya takwimu juu ya umaskini na mazingira; kuendelea kuandaa na kuchapisha nyaraka za kuelimisha umma kuhusu Sheria ya Mazingira, Sera ya Mazingira na Kanuni za Sheria ya Mazingira; kuendelea kutoa mafunzo kwa Watendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu kuhuisha masuala ya mazingira na umaskini katika mipango ya maendeleo; kutoa mafunzo kwa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) kuhusu masuala ya mazingira na umaskini na kuwezesha upatikanaji na upashanaji wa habari za mazingira kupitia Mtandao wa Habari za Mazingira wa Afrika (*Africa Environmental Information Network).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika kipindi hiki, Ofisi iliendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati katika mikoa 13. Mikoa hiyo ni Shinyanga, Kagera, Morogoro,

Singida, Arusha, Dodoma, Kigoma, Rukwa, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Pwani na Tanga.

Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati inaonesha kuongezeka kwa mwamko miongoni mwa wananchi katika shughuli za hifadhi ya mazingira hususan katika kutunza vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti, ikilinganishwa na miaka iliyopita. Kwa mfano, baadhi ya Wilaya zimeanza kuondoa miti isiyofaa na kupanda miti ifaayo kwenye vyanzo vya maji ikiwemo Wilaya za Rungwe na Ruangwa.

Aidha, Ofisi imeendelea kuhamasisha upandaji miti nchini kama ilivyoainishwa kwenye Kiambatisho Na.1. Nachukua fursa hii kuzipongeza wilaya zilizovuka lengo na natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazikuweza kufikia lengo hili ziongeze juhudi katika upandaji na utunzaji miti. Hata hivyo, idadi ya miti iliyopandwa imeshuka kwa asilimia 13 ikilinganishwa na miti iliyopandwa katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Hii ilichangiwa na tatizo la ukame katika maeneo mengi ya nchi hususan katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati huu katika mikoa yote ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti itaanza kutolewa rasmi katika mwaka wa fedha 2009/2010. Madhumuni ya Tuzo hii ni kuhamasisha jamii kushiriki na kuongeza juhudi katika kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti, ili kudhibiti kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini. Katika kipindi hiki, Ofisi imehamasisha jamii, Vikundi, Taasisi, Kampuni na Watendaji wa Wilaya na Mikoa ili kushiriki katika mashindano hayo.

Jumla ya mikoa kumi na sita imeshiriki kwa kuwasilisha washindi wa kila kundi kwa ngazi ya Mkoa ikijumuisha makundi ya Kaya, Kijiji, Kata, Shule, Vyuo, Taasisi, Vikundi na Kampuni, Wilaya na Mikoa. Mikoa iliyoshiriki ni Tabora, Shinyanga, Rukwa, Kagera, Manyara, Mwanza, Lindi, Pwani, Mtwara, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Singida, Mbeya, Iringa na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu, kuwa kwa mara ya kwanza Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti katika ngazi ya Kitaifa zilitolewa katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika kitaifa katika Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma. Tuzo zilizotolewa ni cheti, kombe, fedha na ngao.Washindi wa kitaifa wa tuzo hii walikuwa kama ifuatavyo: (a) kundi la kaya ni Bw. Musa Nyamve Sambe wa Kijiji cha Mwambegwa, Wilaya ya Meatu katika Mkoa wa Shinyanga, aliyepata cheti na Shilingi 2,000,000; (b)

kundi la kijiji ni Kijiji cha Kidabaga kilichopo Tarafa ya Kilolo, Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa kilichopata cheti, kombe na Shilingi 3,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, (c) kundi la Kata ni Kata ya Kigongo, iliyoko Tarafa ya Nyamirembe, Mkoa wa Kagera iliyopata cheti, kombe na Shilingi 3,000,000; (d) kundi la shule za msingi ni Shule ya Msingi ya Ruvu JKT, iliyoko Wilaya ya Kibaha katika Mkoa wa Pwani iliyopata cheti, kombe na Shilingi 3,000,000; (e) kundi la Shule za Sekondari ni Shule ya Sekondari ya Hedaru, iliyoko Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro iliyopata cheti, kombe na Shilingi 3,000,000; (f) kundi la vyuo vya mafunzo na utafiti ni Chuo Kikuu cha Mkwawa, Manispaa ya Iringa, Mkoa wa Iringa kilichopata cheti, kombe na Shilingi 3,000,000; (g) kundi la Taasisi za kijeshi ni Gereza la Karanga katika Mkoa wa Kilimanjaro lililopata cheti, kombe na Shilingi 5,000,000; (h) kundi la Taasisi za Uhamasishaji na Uwezeshaji (NGO's) ni shirika lisilo la kiserikali la Tanzania *Forestry Conservation Group*, lililoko Wilaya ya Korogwe katika Mkoa wa Tanga lililopata cheti, kombe na Shilingi 5,000,000; (i) kundi la Uhamasishaji na Uwekezaji (Kampuni) ni Shirika la Mtakatifu Benedictine Abbey Ndanda kutoka katika Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara waliopata cheti na kombe; (j) kundi la Wilaya ni Wilaya ya Chato, Mkoa wa Kagera iliyopata cheti, kombe na Shilingi 5,000,000; (k) kundi la mkoa bora ni mkoa wa Iringa uliopata cheti, kombe na Shilingi 7,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mshindi wa jumla Kitaifa ni Bw. Musa Nyamve Sambe wa Kijiji cha Mwambegwa, Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Shinyanga aliyetunukiwa cheti, ngao na fedha taslimu shilingi 10,000,000. Mshindi huyu alionesha ubunifu wa ziada katika kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti. Nachukua nafasi hii kuwapongeza washiriki wote waliojitokeza kushiriki katika mashindano haya. Kwa wale ambao hawakufanikiwa kushinda Tuzo hii mwaka huu, wasikate tamaa waendelee na juhudi ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti, ili waweze kuwa miongoni mwa washindi wa mashindano haya yatakapofanyika tena mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii, taasisi na watendaji katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mashindano haya. Ni matarajio yangu kuwa mikoa yote itakuwa inashiriki ktika mashindano haya yatakayokuwa yakifanyika kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kuhifadhi mazingira ya bahari, Uganda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu mwaka 2009/2010, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa uliandaliwa na unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Julai, 2010. Nakala 300 za Mkakati zimechapishwa na kusambazwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaanza utekelezaji, kuelimisha na kuhamasisha wadau pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika inayohusisha nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Katika mwaka wa fedha

2009/2010, shughuli zilizotekelezwa ni uanzishwaji wa vikundi vya uvuvi shirikishi (*Beach Management Units*) katika Vijiji kumi kwa Mikoa ya Kigoma na Rukwa kwa lengo la kuhamasisha uvuvi endelevu; uelimishwaji wa wananchi kuhusu hifadhi endelevu ya Bonde la Ziwa Tanganyika katika Wilaya za Sumbawanga vijijini, Nkasi, Mpanda, Manispaa ya Kigoma na Kigoma Vijijini; uanzishwaji wa Kamati kumi za Mazingira na kuhamasisha utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji sita vya mfano katika mikoa hiyo na uanzishwaji wa shughuli za upimaji wa mialo ya kisasa, pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani katika mikoa husika kuhusu uvuvi shirikishi. Aidha, mafunzo kuhusu uvuvi endelevu na usimamizi shirikishi wa Ziwa Tanganyika yalitolewa kwa Maafisa Uvuvi katika Wilaya za Nkasi, Mpanda, Sumbawanga na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika na shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa majitaka na taka ngumu; kufanya usanifu wa mfumo wa maji safi, majitaka na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji; kuimarisha Kamati za Mazingira katika Mikoa ya Kigoma na Rukwa; kuanzisha mashamba-darasa katika vijiji sita vya mfano; kuandaa miongozo na mpango mkakati wa usimamizi wa majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji; kujenga ofisi ndogo ya mradi Kipili katika Mkoa wa Rukwa; kujenga ofisi ya doria katika mwalo wa Kasanga katika Wilaya ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa shughuli za Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Nile zilifikia ukomo mwezi Septemba 2009. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba, shughuli za Bonde hili zinakuwa endelevu, shughuli hizo zimehuishwa katika mipango ya Wilaya husika na katika Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji; na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli zinazohusu hifadhi ya Bonde la Mto Nile zitatekelezwa kupitia Mikakati hii na mipango ya wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana niliuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu nia ya kuanzisha mradi wa hifadhi ya Bonde la Ziwa Nyasa utakaohusisha nchi za Tanzania, Malawi na Msumbiji. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi ilifanya tathmini ya hali ya mazingira katika wilaya zinazopakana na Ziwa Nyasa ambazo ni Mbinga, Ludewa, Makete, Njombe na Kyela ili kupata takwimu na taarifa za awali zitakazosaidia katika maandalizi ya andiko la mradi wa kikanda wa hifadhi ya Ziwa hilo. Taarifa ya tathmini hii ilijadiliwa katika kikao cha wadau kilichofanyika mkoani Mbeya mwezi Septemba 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wadau walioshiriki katika kikao hiki ni pamoja na Wakurugenzi Watendaji na Maafisa Kilimo, Uvuvi, Maliasili na Mazingira kutoka Halmashauri za Mbinga, Njombe, Ludewa, Makete na Kyela. Kikao hiki kilipendekeza maeneo ya kipaumbele ambayo yatazingatiwa katika uandaaji wa Mradi. Aidha, mapendekezo haya pamoja na yale ya nchi nyingine yalijadiliwa katika mkutano wa

kikanda uliofanyika Jijini Maputo, Msumbiji mwezi Aprili, 2010 ili kuainisha maeneo ya kipaumbele ya ujumla ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha maandalizi ya Programu na kuhamasisha na kuelimisha jamii katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya mazingira yanahitaji ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi wake. Katika mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi wa Mazingira ambayo inatekelezwa na Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*). Mashirika hayo ni pamoja na Jane *Goodall Institute*, *AFRICARE*, *African Wildlife Foundation* (*AWF*) na *World Wildlife Fund for Nature* (*WWF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Programu hii, mafanikio yafuatayo yalipatikana: Jumuiya za Maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori (*Wildlife Management Areas* – WMA), ziliendelea kuwezeshwa na *African Wildlife Foundation* kutengeneza mipango ya biashara na kupitia upya mikataba na wawekezaji. Kutokana na mapitio hayo, Jumuiya ya Burunge iliyoko katika Wilaya ya Babati iliongeza mapato yake kutoka wastani wa shilingi milioni 4.2 hadi milioni 21 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika utekelezaji wa Programu hii, Askari wa Wanyamapori na wajumbe sabini wa Jumuiya hiyo walipewa mafunzo maalum ya kuwawezesha kuboresha utendaji wa kazi. Vile vile, mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu ya jamii katika Wilaya ya Kondoa, hususan katika vijiji vya Kolo, Mnenia, Itundwi na Kandaga iliandaliwa. Katika kipindi hiki, juhudi zimefanyika pia kusaidia jamii ya wafugaji kutekeleza miradi ambayo itaongeza thamani kwa ufugaji. Hii ni pamoja na mafunzo ya unenepeshaji wa mifugo yaliyotolewa kwa wanavijiji 400, kupewa madume bora ya mbegu 11 na ujenzi wa machinjio ya kisasa. Aidha, vijiji tisa katika Wilaya za Monduli, Simanjiro na Karatu viliandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Mfumo Ikolojia wa Gombe inayotekelezwa na *Jane Goodall Institute* katika vijiji 24 vya Mkoa wa Kigoma. Katika kipindi hiki: hekta 6,768 zilitengwa na kuhifadhiwa; hekta 838 zimepandwa miti kwa ajili ya nishati kwa matumizi ya kaya; vijiji sita vilipimwa na kuandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi; kaya 520 zilianza kutumia majiko banifu; wakulima 348 walihudhuria mafunzo kuhusu njia bora za kilimo kinachozingatia hifadhi ya mazingira; vijana 314 walipatiwa mafunzo kuhusu hifadhi ya mazingira kwa lengo la kutoa elimu hiyo kwa vijana wengine *(Training of Trainers*); na klabu tano za uhamasishaji wa shughuli za hifadhi ya mazingira zilianzishwa. Aidha, mwezi Aprili, 2010, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitembelea miradi hii ili kutathmini utekelezaji wake. Katika kipindi cha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu hii na kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika uchimbaji madini. Madhumuni ya Tuzo hii ni kuhamasisha makampuni ya uchimbaji wa madini kuhifadhi mazingira. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi imeendelea kuhamasisha makampuni kushiriki katika mashindano ya Tuzo hii kwa kuandaa na kusambaza kwa wadau vipeperushi 5,000 kuhusu vigezo na mwongozo wa utoaji Tuzo. Aidha, Mchakato wa kumpata mshindi wa tuzo hii kwa mwaka 2009/2010 unaendelea na makampuni yote ya Uchimbaji yanashiriki. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa wadau na kuhamasisha ushiriki wao ili kuongeza ushindani na hivyo kuboresha hifadhi ya mazingira katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya Tabia nchi. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Kwa kuwa Programu hii ilikuwa na mipango ya muda mfupi, ilifanyiwa mapitio na kujumuisha mipango ya muda wa kati na muda mrefu. Aidha, katika kipindi hiki, Mkakati wa Kitaifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ulikamilishwa. Mkakati huu unaainisha changamoto zilizopo na shughuli za vipaumbele katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) unaolenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya misitu. Mpango huu unalenga pia kubaini njia bora ya kutoa motisha kwa wananchi na taasisi mbalimbali zinazotunza na kuhifadhi misitu na kuweka mfumo bora na madhubuti wa soko la biashara ya hewa ukaa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, miradi sita ilianza kutekelezwa Asasi Zisizo za Kiserikali katika maeneo mbalimbali nchini. Asasi hizo ni Tanzania *Forest Conservation Group* (*TFCG*), CARE Tanzania (upande wa Zanzibar), Tanzania *Traditional Energy Development and Environmental Organization* (*TaTEDO*), The Jane *Goodall Institute, African Wildlife Foundation* (*AWF*), na Mpingo *Conservation*. Aidha, Asasi za *Wildlife Conservation Society of Tanzania* (*WCST*) na *World Wildlife Fund for Nature* (WWF) Tanzania zinaendelea kukamilisha maandiko ya miradi yao. Aidha, tafiti za kina *(in-depth studies*) tano kuhusu masuala ya MKUHUMI zinaendelea kufanyika. Uzoefu utakaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi hii na tafiti hizi utachangia katika utayarishaji wa Mkakati wa taifa wa MKUHUMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata jumla ya Dola za Marekani milioni 2.9 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 4.06, kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Africa Adaptation Programme).* Mradi huu ni wa miaka miwili, na utaanza kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha. Mradi huu unalenga kuhuisha masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sera za sekta mbalimbali. Wizara na Taasisi zitakazohusika katika utekelezaji wa Mradi huu ni Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira - Zanzibar; Mamlaka ya Hali ya Hewa; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Taasisi ya Kutathmini Rasilimali (*Institute of Resource Assesment* - *IRA*) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, miradi ya majaribio itatekelezwa katika Wilaya za Igunga (Tabora), Mbinga (Ruvuma), Misenye (Kagera) na Kaskazini A (Kaskazini Unguja).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi imetengewa fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 3.5 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 4.9 kutoka katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika baadhi ya maeneo ya pwani ya nchi. Mradi huu umeanza kutekelezwa na unalenga katika masuala ya upandaji na hifadhi ya misitu ya mikoko katika Wilaya ya Rufiji, ukarabati wa ukuta wa ufukwe wa Pangani na uchimbaji wa visima vipya vya maji katika Halmashauri ya Bagamoyo baada ya baadhi ya visima vya zamani kuingiliwa na maji chumvi kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Nchi Katika Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark, ulioanza rasmi mwezi Agosti mwaka 2008. Katika kipindi hiki, kazi zilizotekelezwa ni: Kutathmini mwenendo wa hali ya mabadiliko ya tabianchi *(climate change scenarios)*; kuandaa taarifa ya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi iliyofanyika katika mikoa sita Tanzania Bara na mikoa yote ya Tanzania Visiwani; kuendelea na kuandaa kijitabu cha vibonzo na kusambaza vitini zaidi ya 30,000.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: kujenga uwezo kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa Watumishi wa Idara ya Mazingira, wataalam katika ngazi za Wilaya na Mikoa, sekta na taasisi za umma; kuimarisha mfumo wa utunzaji taarifa za mabadiliko ya tabianchi; kuendelea kutathmini mwenendo wa hali ya mabadiliko ya tabianchi (*climate change scenarios*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi nne duniani ambazo zitanufaika na msaada wa fedha kutoka Jumuiya ya Ulaya (*European Union – EU*) mwaka huu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (*Climate Change mitigation and adaptation)* kama ilivyoanishwa katika Mpango wa Jumuiya ya Ulaya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Global Climate Change Alliance* - GCCA). Mradi huu utatekelezwa kwa miezi 72 kwa gharama ya *Euro* milioni 2.2 sawa na shilingi bilioni 3.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya inaandaa Mwongozo kuhusu utekelezaji wa Mradi huu ambao unatarajiwa kutekelezwa katika vijiji kadhaa nchini. Shughuli zitakazofanyika katika vijiji vitakavyochaguliwa zitahusu Hifadhi ya mazingira kwa ujumla; kwa mfano, Mipango shirikishi ya matumizi Bora ya

ardhi, Usimamizi Shirikishi wa Misitu, kilimo na ufugaji endelevu, usimamizi wa matumizi ya maji, na elimu ya mazingira mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: kuendelea kujenga uwezo na kutekeleza Programu, kuandaa Mikakati na Miradi mbalimbali inayolenga katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi; kuendelea kuratibu utekelezaji wa MKUHUMI na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi. Kuanza utekelezaji wa miradi ya MKUHUMI katika Wilaya za mfano za Bagamoyo, Kilolo na Wilaya za Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kyoto unaolenga katika kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Ofisi imeidhinisha maombi ya miradi mitatu ya kupunguza gesijoto na kuleta maendeleo endelevu (*Clean Development Mechanism* - CDM). Miradi hiyo ni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya mabaki ya miti na pumba za mpunga katika kiwanda cha saruji Mbeya; mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya maji ya Mto Mwega (Mufindi) na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Ruhudji (Njombe). Miradi hii inalenga kuzalisha nishati jadidifu *(renewable energy)* na kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Serikali, wawekezaji na watekelezaji katika miradi hiyo watanufaika kutokana na malipo ya kupunguza gesijoto duniani kulingana na kiasi cha hewa ukaa watakayopunguza.

Aidha, Ofisi iliendelea kuelimisha na kujenga uwezo wa wadau kwa kuandaa na kutekeleza miradi ya *CDM*. Katika kipindi hiki, Ofisi kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania pamoja na Ubalozi wa Uingereza iliendesha mafunzo kwa sekta binafsi kuhusu jinsi ya kuandaa miradi ya *CDM*. Mafunzo haya yalifanyika Dar es Salaam mwezi Novemba, 2009 na Aprili, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuchambua na kuidhinisha miradi ya *CDM* yenye manufaa kwa Tanzania na itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuongeza uelewa katika uandaaji na utekelezaji wa miradi ya *CDM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Ofisi iliratibu mchakato wa utambuzi wa maeneo ya kipaumbele yatakayohusishwa katika mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhi mkoani Kilimanjaro chini ya Mpango Maalum wa Afrika wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*TerrAfrica*). Maeneo yalioainishwa ni Kilimo, Nishati na Maliasili. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne (2010-2014).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya *Global Mechanism* inayohusika na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame imeendesha warsha ya wadau. Warsha hii ililenga kuelimisha wadau kuhusu fursa za uanzishaji wa mfumo wa uwekezaji katika ardhi ya kilimo

(*Country Integrated Strategic Investment Framework – CSIF*) na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo endelevu ya ardhi (*Integrated Financing Strategy – IFS*). Warsha ilihusisha Wizara mbalimbali, Taasisi zisizokuwa za Serikali za kitaifa na kimataifa, Sekta binafsi, Waandishi wa Habari, Vyuo vya Elimu ya Juu na Wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli zifuatazo zitatekelezwa chini ya Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame: kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhi mkoani Kilimanjaro utakaogharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni tatu ambazo ni sawa na shilingi bilioni 4.2; kuhuisha Mpango Mkakati wa miaka kumi wa Mkataba huu katika Programu ya NAP; kuratibu mpango wa uanzishaji wa Mfumo wa Uwekezaji katika Ardhi ya Kilimo na Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya maendeleo endelevu ya ardhi; na kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Maliasili ya Misitu ya Miombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2009/2010, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Hifadhi ya Bioanuai. Katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo yenye lengo la kuhifadhi Bioanuai. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Hifadhi ya Ziwa Tanganyika; Mradi wa Hifadhi Endelevu ya Misitu ya Miombo Magharibi mwa Tanzania na Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Kuhifadhi Bioanuai na Misitu ya Pwani ya Tanzania na Zanzibar. Aidha, katika kipindi hiki, Ofisi imeandaa Ripoti ya Nne ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Mkataba huu. Ripoti hii imeainisha hali halisi ya bioanuai nchini, jitihada za Serikali na wadau wengine katika hifadhi ya bioanuai na uhuishaji wa masuala ya bioanuai katika sekta mbalimbali pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2010 umeteuliwa na Umoja wa Mataifa kuwa ni Mwaka wa Kimataifa wa Bioanuai. Kaulimbiu ya maadhimisho haya ni “Bioanuai ni Tegemeo la Uhai na Maisha Yetu” (*Biodiversity is Life. Biodiversity is Our Life).* Kaulimbiu hii inalenga kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuepuka uchomaji ovyo wa misitu na ukataji miti holela, kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kudhibiti shughuli za kiuchumi zisizo endelevu ili kuwa na hifadhi endelevu ya viumbe hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kusimamia miradi iliyo chini ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai kuna Mkataba mdogo wa Cartagena unaohusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari zitokanazo na biotekinolojia ya kisasa. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Cartagena. Katika utekelezaji wa Mkataba

huu, Kanuni za Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa (*Environmental Management (Biosafety) Regulations,* 2009) zimekamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mara ya kwanza, Ofisi inaratibu mchakato wa uchambuzi wa maombi ya majaribio ya kimaabara ya zao la muhogo ambalo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki ili kuhimili magonjwa. Ofisi ilitoa elimu kwa umma kupitia Redio na Luninga kuhusu masuala ya viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki (*Genetically Modified Organisms* - GMOs) kwa lengo la kukuza uelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi imeanza mchakato wa uanzishwaji wa mtandao wa vituo kumi vya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa kwa mimea, mazao na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki (*National Centres of Excellence for Biosafety*). Vile vile, mafunzo kuhusu udhibiti wa viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na taratibu za kupokea maombi ya uingizaji wa vinasaba vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki yaliendeshwa kwa wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Bioteknolojia ya Kisasa pamoja na Mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Cartagena. Shughuli zitakazotekelezwa ni kutoa mafunzo kwa sekta husika juu ya utambuzi, udhibiti, tathmini na masuala ya kisheria kuhusu bidhaa na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki; kuboresha maabara zilizoainishwa katika mtandao wa vituo kumi vya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na kutoa elimu ili kukuza uelewa wa wadau kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Mkataba huu ni kudhibiti matumizi ya kemikali hizi na kukuza matumizi ya kemikali na njia mbadala ambazo ni salama kwa mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Montreal kuhusu Kemikali Zinazomong’onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni angani. Aidha, Ofisi iliendesha mafunzo kwa Maafisa Forodha sitini jijini Dar es Salaam kuhusu majukumu yao katika utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Kemikali Zinazomo’ngonyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni. Vile vile, mafunzo kwa Mafundi Mchundo tisini wa majokofu na viyoyozi juu ya njia bora za kuhudumia vifaa hivyo na ubadilishaji wa teknolojia za mitambo ya kupoozea inayotumia gesi haribifu yalifanyika Zanzibar na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki, Vituo vitano vya Kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Mbeya, Mwanza; na Zanzibar, vimeanzishwa katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi (*VETA*) ambavyo vimeanza kurejeleza gesi haribifu ili zitumike tena. Aidha, Ofisi iliratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ozoni kwa kufanya maonesho ya namna bora ya kuhudumia vifaa vinavyotumia kemikali zenye madhara kwa Tabaka la Ozoni na kemikali mbadala tarehe 16 Septemba, 2009 jijini Dar es Salaam. Katika maonesho hayo, Ofisi kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi cha Chang’ombe iliwezesha ubadilishaji wa teknolojia wa kutumia gesi haribifu

kwenda gesi mbadala katika majokofu na viyoyozi. Jumla ya majokofu 500 na viyoyozi 300 vilikarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaandaa Mpango wa Kitaifa wa Kupunguza Matumizi ya kemikali aina ya *Hydrocholorofluorocarbons* (*HCFCs*) zinazotakiwa kuondoshwa kwenye soko ifikapo mwaka 2030 kwa mujibu wa ratiba ya Mkataba wa Montreal. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Forodha na Mafundi Mchundo; kuandaa na kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba; ubadilishaji wa teknolojia za mitambo ya kupoozea inayotumia gesi haribifu; kukusanya na kuwasilisha katika Sekretariati ya Mkataba takwimu za mwaka za uagizaji na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni na kuendelea kutoa elimu kwa wadau na umma juu ya umuhimu wa kulinda Tabaka la Hewa ya Ozoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkataba kuhusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi (Mkataba wa Basel) na Mkataba unaozuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika (Mkataba wa Bamako). Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliratibu utekelezaji wa Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na Mkataba wa Bamako unaozuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki, Ofisi, ilisambaza vipeperushi 3,000 kuhusu Mkataba wa Basel kwa wadau ili kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa Mkataba huu; warsha moja ilifanyika Dar es Salaam Septemba, 2009 ili kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka; muhtasari wa Mkakati umeandaliwa na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Zebaki umekamilika na elimu ilitolewa kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika migodi ya Bulyamkulu, Kahama, Geita na Tarime kwa ajili ya kukuza uelewa juu ya madhara yatokanayo na Zebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka na Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Zebaki; kuendelea kukusanya takwimu za usimamizi wa taka; kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Mikataba hii nchini na kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi wa taka za sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu (Mkataba wa Stockholm). Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockhom. Katika kipindi hiki, Ofisi imeandaa miradi miwili inayohusu kujenga uwezo wa Kitaifa kudhibiti kemikali hizi. Jumla ya Dola za Marekani 250,000 sawa na shilingi Milioni 350 zimepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa kujenga uwezo wa taasisi za Serikali kusimamia matumizi ya kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu. Taasisi hizo ni kutoka Wizara za: Kilimo, Chakula na Ushirika; Maliasili na Utalii; Afya na Ustawi wa Jamii; Viwanda, Biashara na Masoko na Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vipeperushi 4,000 kuhusu Mkataba na Mpango Kitaifa wa utekelezaji wa Mkataba huo viliandaliwa na kusambazwa kwa wadau. Vile vile miongozo miwili kuhusu usimamizi wa Kemikali zinazodumu muda mrefu katika mazingira na usimamizi wa maeneo yaliyochafuliwa na kemikali hizi inakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuratibu Mpango wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mkataba wa Stockholm ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo wa taasisi husika. Shughuli zitakazofanyika chini ya mradi huu ni pamoja na kukuza uelewa wa wadau kuhusu madhara na usimamizi wa kemikali zinazodumu muda mrefu katika mazingira. Wadau hawa ni pamoja na wataalam wa tiba, wahandisi na mafundi mchundo katika mashirika yanayosambaza umeme nchini ikiwa ni pamoja na *TANESCO* na *ZECO* (Zanzibar). Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wataalam wa viwandani kuhusu usimamizi bora wa kemikali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Mfuko huu unafadhili maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni Mabadiliko ya Tabianchi; Hifadhi ya Bioanuai; Hifadhi ya Ardhi; Hifadhi ya Maji ya Kimataifa; Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni na Kemikali Zinazodumu kwa Muda Mrefu katika Mazingira. Katika eneo la Hifadhi ya Bioanuai, jumla ya miradi minne mikubwa na ya kati ilipata ufadhili wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.7 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 17.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo ni *Sustainable Woodland Management in the* Miombo *Areas of Western* Tanzania, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2.2 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 3.1 unaotekelezwa katika Mkoa wa Tabora; *Strengthening Management Effectiveness in the National Parks System* unaotekelezwa Usangu, Rungwe, Kitulo, Livingstone, Mbuga za Taifa Saadani na Serengeti, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 5.9 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 8.3 *Strengthening the System of Managing Biodiversity* unaotekelezwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni nne ambazo ni sawa na shilingi bilioni 5.6 na *GEF Small Grants Program,* wenye thamani ya Dola za Marekani 600,000 ambazo ni sawa na shilingi milioni 840.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Mabadiliko ya Tabianchi, miradi mitatu ilipata ufadhili wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 5.3 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 7.4. Miradi hiyo ni *Sustainable Woodland Management* in the Miombo Areas, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni Moja na unatekelezwa na Taasisi ya Kutathmini Rasilimali (*IRA*) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; *Mini-Grids Based on Small Hydropower Sources to Augment Electrification*, wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.7 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 5.2; na Mradi wa *Promoting Energy Efficiency in Buildings in Eastern Africa,* wenye thamani ya Dola za Marekani 595,600 ambazo ni sawa na shilingi milioni 834, ambayo inatekelezwa na Wizara ya Nishati na Madini. Katika eneo la Hifadhi ya Ardhi, mradi wa *Reducing Land Degradation in the High land* of Kilimanjaro, wenye thamani ya Dola za Marekani

milioni 2.7 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 3.8, mradi unaotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika eneo la Maji ya Kimataifa, mradi wa *Coastal Tourism Project* wenye thamani ya Dola za Marekani 59,351 ambazo ni sawa na shilingi milioni 83.1 unatekelezwa katika Wilaya ya Mafia, Kinondoni na Bagamoyo. Jumla ya miradi midogo 14 ya mazingira yenye thamani ya shilingi 556,837,272/= ilipata ufadhili kutoka Mfuko huu. Vile vile, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *GEF* ulifanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Rukwa, Ruvuma na Tanga. Aidha, uhamasishaji na ushauri wa vikundi wa kuandaa miradi ya ufadhili wa *GEF* ulifanyika kupitia maadhimisho na maonesho ya kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkutano Mkuu wa *GEF* uliofanyika nchini Uruguay mwezi Mei 2010, Tanzania imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 26 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 36.5 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka ujao wa fedha. Fedha hizi ni ongezeko la asilimia 70 ya fedha ambazo mfuko huu ulitoa kwa Tanzania miaka minne iliyopita baada ya Tanzania kuonekana kufanya vizuri katika eneo la hifadhi ya mazingira chini ya ufadhili wa Taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zitatumika kufadhili miradi itakayohusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi, bioanuai na usimamizi endelevu wa matumizi ya ardhi. Aidha, kwa mara ya kwanza, chini ya Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*UNCCD*) Tanzania imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 5.61 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 7.9 ambazo zitatumika katika kuhifadhi ardhi na kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za *GEF* nchini kwa kuhamasisha na kushauri vikundi, kuandaa miradi kwa ajili ya ufadhili wa *GEF* na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi iliyopata ufadhili wa *GEF* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira Tanzania (*Cleaner Production Centre of Tanzania - CPCT*). Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliratibu utekelezaji wa mradi wa majaribio kuhusu elimu ya matumizi na uzalishaji endelevu (*sustainable consumption and production*) katika shule za msingi teule 41 za Jiji la Dar es Salaam. Mradi huu ulilenga kukuza uelewa kwa wanafunzi kuhusu usimamizi wa taka ngumu kama vile plastiki, karatasi na makopo (*solid waste management).*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Kituo kiliendesha warsha kuhusu uzalishaji bora kwa wadau 50 kutoka sekta za Viwanda, Kilimo, Utalii, Nishati, Maji, Misitu; Taasisi zisizo za Kiserikali; Vyuo Vikuu na vyombo vya habari mwezi Machi, 2010 Jijini Tanga. Katika kipindi hiki, Kituo kilikamilisha tathmini mbili zinazolenga kuimarisha hali ya usimamizi wa kemikali na taka za sumu nchini na uendeshwaji wa Vituo vya

Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira katika nchi 13 Barani Afrika. Tathmini hizi zinalenga kuboresha usimamizi wa taka za sumu nchini na katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Kituo kitatekeleza awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira wa Ziwa Viktoria unaolenga kuhuisha dhana ya matumizi na uzalishaji endelevu katika shughuli za kiuchumi katika Bonde la Ziwa Viktoria upande wa Tanzania. Aidha, Kituo kitaendelea kuhamasisha viwanda kuzingatia dhana ya uzalishaji bora na kufanya utafiti wa hali ya usimamizi wa taka za elektroniki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi iliendelea kuratibu maandalizi ya tathmini ya uchambuzi wa faida na hasara za kupiga marufuku mifuko ya plastiki nchini. Tathmini hiyo inafanywa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Chuo kikuu cha Dar es Salaam na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha, katika kipindi hicho, Ofisi itafanya Mapitio ya Kanuni za kupiga marufuku mifuko laini ya plastiki ya mwaka 2006 baada ya tathmini kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 5 Juni kila mwaka Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Kimataifa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu yalifanyika katika Jiji la Kigali, Rwanda na K itaifa yalifanyika katika Wilaya ya Bahi, Dodoma. Kauli-mbiu ya Siku ya Mazingira Duniani Kimataifa mwaka huu, ilikuwa “Viumbe ni Wengi. Dunia ni Moja na Mstakabali ni Mmoja” (*Many Species. One Planet. One Future*). Kauli-mbiu hii inalenga katika kuhamasisha jamii kuchukua hatua zinazolenga katika hifadhi ya viumbe hai na mifumo ya ikolojia kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kitaifa kauli-mbiu iliyoongoza maadhimisho haya ni “Tunza Mazingira kwa Hifadhi Endelevu ya Viumbe Hai”.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya ujumbe huu kitaifa ni kuelimisha na kuhamasisha wananchi wote juu ya utunzaji na hifadhi ya mazingira hususan kupanda na kutunza miti, kuhifadhi misitu na uoto wa asili. Mwaka huu maadhimisho yalifanyika kwa kuhusisha shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Upandaji na palizi ya miti, kutoa elimu kuhusu hifadhi ya mazingira kupitia vyombo vya habari, vikundi vya sanaa na maonesho, shughuli hizo zilifanyika kuanzia tarehe 1 Juni hadi siku ya kilele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wote walioshiriki katika maadhimisho haya. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Mkoa wa Dodoma hususan Wilaya ya Bahi, kwa kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo Kitaifa na kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Watanzania wote kwa ushiriki wao. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea na uratibu na uhamasishaji wa ushiriki wa wadau mbalimbali kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997, Mpango Mkakati wa Baraza (*NEMC Strategic Plan* 2010-2014), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, nyaraka na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Baraza lilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi na sehemu za uzalishaji ili kuhakikisha kuwa taratibu na kanuni za hifadhi ya mazingira zinafuatwa. Makampuni/Taasisi zilizokaguliwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na kupewa amri ya zuio kutokana na kufanya uzalishaji bila kuzingatia hifadhi ya mazingira ni pamoja na Bubu *Gao Footwear*, *BIDCO Oil & Soap Limited*, *Abla Hotel & Apartments, Murzah Oil Mills*, *Tridea Cosmetics, Karibu Textile Mills (KTM)* na kiwanda cha chuma cha A.M. Aidha, Baraza lilifanya ukaguzi katika machinjio ya Ukonga na Vingunguti Dar es Salaam. Pia ukaguzi ulifanyika katika mgodi wa North Mara, Tarime kutokana na malalamiko ya wananchi kuhusu uchafuzi wa mazingira uliokuwa ukifanywa na Mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lilibaini upungufu unaosababisha uchafuzi wa mazingira na lilitoa maelekezo ya marekebisho ya matatizo hayo. Aidha, Baraza lilifanya ufuatiliaji katika migodi ya Kahama, Geita, Bulyanhulu pamoja na viwanda vilivyo na mikakati ya kupunguza gesi za hewa ukaa katika uzalishaji wa nishati ambavyo ni pamoja na Kiwanda cha Sukari cha *TPC*-Moshi, *TANWAT* na *Sao hill* Iringa kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanatekeleza vyema mipango ya hifadhi ya mazingira katika uzalishaji wao.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea kuimarisha shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria, ili liweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ilivyoainishwa katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Wakaguzi wa Mazingira 21 pamoja na maafisa mazingira wengine 13 kutoka Baraza walipewa mafunzo kuhusu misingi ya ukaguzi wa mazingira. Aidha, mchakato wa uteuzi wa wakaguzi wa mazingira toka taasisi nyingine umeanza na Baraza limekamilisha maandalizi ya sifa na vigezo vitakavyotumiwa katika uteuzi wa wakaguzi hawa na kuwasilisha kwa mamlaka inayohusika. Uteuzi huo utakamilishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza kwa kushirikiana na uongozi wa polisi Mkoa wa Mbeya waliendesha msako wa kushtukiza katika jiji la Mbeya ili kutekeleza Kanuni iliyopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni 30 na

vifungashio vya maji na juisi bila kujali unene wake. Zoezi hili lilifanyika mwezi Machi, 2010 ili kubaini wauzaji wa mifuko hiyo iliyopigwa marufuku. Wafanyabiashara 10 walikamatwa, kufunguliwa mashtaka na kutozwa faini kati ya shilingi 50,000 hadi 80,000. Hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa watakaopatikana na mifuko iliyopigwa marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza kwa kushirikiana na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamefanya utafiti wa kubaini hasara na faida zitokanazo na kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, kwa lengo la kuishauri Serikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litakamilisha taarifa ya utafiti kwa kujumuisha maoni ya wadau na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu hatua inayostahili kuchukuliwa. Aidha, Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni iliyopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki chini ya microni 30, kwa kutoa elimu kwa umma, kuendesha misako na kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaokiuka matakwa ya Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza limeendelea kuratibu programu yenye lengo la kukusanya, kusafisha na kuteketeza mlundikano wa viuatilifu chakavu nchini ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa mlundikano wa viuatilifu haujirudii hapa nchini (*African Stockpiles Programme* - *ASP*). Katika mwaka wa fedha 2009/2010, zoezi la kuainisha maeneo yenye viuatilifu chakavu hapa nchini lilikamilika kwa kuainisha maeneo katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma) na visiwa vya Zanzibar. Aidha, zoezi la kuainisha vituo vya kukusanya viuatilifu hivyo limefanyika katika kanda ya Kati, Kaskazini, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Zanzibar. Zoezi la kuanza kukusanya viuatilifu hivyo litaanza baada ya mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili limekuwa na mafanikio kwani baada ya kufanya kampeni ya kuelimisha wadau na wananchi wa maeneo husika, mwitikio na ushirikiano kutoka kwa watu binafsi, Taasisi za Umma na Asasi Zisizo za Kiserikali ulikuwa ni mkubwa. Aidha, kiasi cha tani 1500 za viuatilifu chakavu viligundulika na kuainishwa katika kipindi cha mwaka mmoja (2009) kutoka lengo la viutalifu tani 1200 zilizokusudiwa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea na zoezi la ukusanyaji na usafirishaji wa viuatilifu hivi kwa ajili ya uteketezaji. Pia Baraza litajenga mfumo wa kuzuia mrundikano huo kujitokeza tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, miradi ya maendeleo 175 ya wawekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM. Kati ya miradi hiyo, miradi 121 imefanyiwa TAM na ripoti zake kufanyiwa mapitio kwa ajili ya kupata Hati za TAM (*EIA Certificates*). Jumla ya miradi 89 imepata Hati za TAM baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni za TAM. Kati ya Miradi iliyopewa Hati: 37 ni ya mawasiliano; 13 ya ujenzi na uendelezaji kwenye vivutio vya utalii; 11 ya miundombinu; Mitano ya uchimbaji madini; mitatu ya nishati; mitatu ya viwanda; na mitatu ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mafanikio makubwa kwani kumekuwepo na ongezeko la miradi iliyofanyiwa TAM na kupatiwa Hati kutoka miradi 160 mwaka 2008/2009, hadi miradi 220 mwaka 2009/2010, sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Ongezeko hili linaonesha kuwa, wawekezaji wengi wamepata mwamko wa kufuata na kutimiza matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, ambayo pamoja na mambo mengine inawataka wawekezaji kutimiza masharti ya TAM kabla na baada ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lilifanya ufuatiliaji kwa miradi ya madini ya North Mara, Bulyankulu, Buzwagi na Geita ili kubaini kama wawekezaji walikuwa wanatekeleza masharti ya Hati ya TAM. Wawekezaji walipewa maagizo ya kutekeleza ili kuhakikisha kuwa shughuli zao zinazingatia maendeleo endelevu. Miradi 174 katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; miradi 11 katika Kanda ya Kaskazini na miradi 20 katika Kanda ya Ziwa ilikaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na kuwepo kwa mitambo na mifumo hafifu ya kudhibiti taka zinazozalishwa, uhaba wa wataalam wa mazingira, baadhi ya viwanda kuwa karibu sana na makazi ya watu, makampuni kutenga fedha kidogo sana kwa ajili ya hifadhi ya mazingira na uelewa mdogo wa watendaji wa viwanda na makampuni kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 na masuala ya TAM. Kufuatia changamoto hizi, Baraza lilitoa ushauri wa kurekebisha mapungufu na kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza liliendesha mafunzo yenye lengo la kukuza weledi kwa wadau kuhusu umuhimu na hatua za kuzingatiwa katika masuala ya TAM. Mafunzo hayo yalitolewa kwa: wafanyakazi 10 wa Mamlaka ya udhibiti wa huduma ya Maji na Nishati (*Energy and Water Regulatory Authority-EWURA*) Makao Makuu Dar es Salaam mwaka *2009; wafanyakazi 35 wa Idara ya Maji* - Bonde la Mto Ruvuma, Novemba 2009 na wafanyakazi 60 kutoka mamlaka za maji mijini, mabonde na Wizara ya Maji, mwezi Aprili 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wafanyakazi 24 wa Baraza walipewa mafunzo kuhusu TAM inayohusu miradi ya utafiti na uchimbaji wa mafuta. Pia, Baraza lilifanya warsha kwa wadau toka sekta, taasisi na Mawakala wa Serikali wanaohusika na utoaji wa vibali vya aina mbalimbali kwa lengo la kukuza ushirikiano na kufahamishana wajibu wa kila mdau kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Sura 191. Warsha hii ilifanyika tarehe 12 Aprili, 2010 na kuhudhuriwa na washiriki 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki, Baraza lilipokea jumla ya maombi 141 kwa ajili ya usajili wa wataalam wa TAM na Ukaguzi wa mazingira (*Environmental Auditors).* Maombi haya yalifanyiwa tathmini ili kukamilisha usajili rasmi wa wataalam hawa. Wataalam 49 wa TAM na 22 wa ukaguzi wa mazingira wamesajiliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali tarehe 26 Machi, 2010. Pia, maombi ya makampuni 24 yanayotoa utaalam elekezi wa TAM na Ukaguzi wa mazingira yalipokelewa kwa ajili ya usajili. Makampuni 12 yalisajiliwa kwa ajili ya kufanya TAM na 10 yalisajiliwa kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea kufanya mapitio ya taarifa za TAM, kusajili wataalam wa TAM na Ukaguzi wa Mazingira na kukagua miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye Hati za TAM na mipango ya hifadhi ya mazingira (*Environmental Management Plans*). Vile vile, Baraza litaendelea kuwajengea wadau uwezo kuhusu masuala ya TAM ili kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inazingatia matakwa ya TAM ili iwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya mazingira ni muhimu sana ili jamii iweze kushiriki katika kufanya maamuzi sahihi yanayohusu matumizi endelevu ya maliasili na mazingira kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza liliandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau: vipeperushi 30,000 kuhusu mazingira na kilimo; nakala 3,000 za Jarida la NEMC la mwezi Julai – Desemba 2009; nakala 2,000 za kalenda ya mwaka 2010 na shajara 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lilishiriki katika wiki ya maadhimisho ya siku ya Nane Nane mwaka 2009 ili kukuza weledi kuhusu mahusiano kati ya kilimo na hifadhi ya mazingira yaliyofanyika Mkoani Dodoma, Mbeya na Mwanza. Aidha, jumla ya vibwagizo 60 na vipindi 45 viliandaliwa na kurushwa katika luninga mbalimbali nchini. Vibwagizo hivyo na vipindi vya luninga vilihusu wajibu wa wadau katika udhibiti wa taka na mada za elimu ya mazingira. Vile vile, makala 15 za luninga kuhusu uhusiano kati ya umaskini na mazingira ziliandaliwa katika Wilaya ya Iramba na Bagamoyo na makala kuhusu hifadhi ya Korongo la Mto Kihansi na kuoneshwa kwenye luninga na redio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza liliendelea kutoa elimu kwa wadau ili waweze kuelewa masuala mbalimbali ya mazingira pamoja na majukumu na wajibu wao katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Sura 191. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya warsha kwa wadau 50 kutoka *Tanzania Investment Centre* (TIC), *Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture* (TCCIA), *Confederation of Tanzania Industries* (CTI) na *Tanzania Communication Reguratory Authority* (TCRA), mwezi Februari, 2010 huko Bagamoyo. Pia, Maafisa Mazingira 16 toka Kanda ya Kaskazini (Manyara na Arusha) walihudhuria mafunzo kama hayo Wilayani Karatu mwezi Desemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Machi, 2010 Baraza kwa kushirikiana na uongozi wa vijana Mkoani Tanga liliandaa na kuendesha warsha kwa viongozi 85 wa vikundi vya vijana kutoka Mkoa wa Tanga ili kukuza weledi kuhusu hifadhi ya Mazingira. Vile vile, warsha nyingine ilifanyika kwa sekta ya elimu iliyohusisha wakuza mitaala, Baraza la Mitihani na Wakaguzi wa shule kutoka kanda saba za elimu ilifanyika Dodoma mwezi Mei, 2010 kwa lengo la kuhuisha masuala ya mazingira katika mitaala na ukaguzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Jumla ya washiriki 58 walihudhuria warsha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zote za kutoa elimu, vitendo vya uchafuzi wa mazingira kama utupaji taka ovyo, utiririshaji wa maji machafu, matumizi na uchomaji mifuko ya plastiki na ukataji miti kiholela bado ni changamoto kwa baadhi ya maeneo. Napenda kutoa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika shughuli za

hifadhi ya mazingira kwani suala la hifadhi ya mazingira ni letu sote na athari za uharibifu wa mazingira hazina mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza litaongeza kasi ya kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu ya wadau katika uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi. Aidha, Baraza litaongeza kasi ya kutumia vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa Umma kutokana na vyombo hivi kuwa na mtandao mkubwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza lilifanya tathmini ya hali ya maeneo oevu katika kanda ya Kaskazini ikijumuisha Mikoa ya Tanga (Pangani, Korogwe na Handeni), Kilimanjaro (Moshi, Same na Mwanga), Arusha (Monduli na Karatu) pamoja na Mkoa wa Manyara (Babati na Hanang). Matokeo ya tathmini hii yanaonesha kuwa maeneo oevu yanazidi kupungua hivyo kuna umuhimu wa kuandaa mipango ya matumizi endelevu. Baraza litaendelea kushirikiana na halmashauri husika katika kuandaa mipango ya matumizi ya maeneo haya.

Aidha, Baraza liliendesha warsha kwa Maafisa Mazingira wa Wilaya, Manispaa, Miji, Majiji na Mikoa katika Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha na Tanga) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukusanya taarifa ya hali ya milima na mifumo ikolojia yake. Zoezi la tathmini litafanyika kwa ushirikiano na Maafisa Mazingira wa Mikoa hiyo katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza kwa kushirikiana na *Natural Forest Resource Management and Agroforestry Centre* - *NAFRAC*, walifanya uperembaji ili kutathmini hali ya mazingira na mafanikio ya mfumo wa ngitiri katika Mkoa wa Shinyanga. Vile vile, Baraza lilifanya ufuatiliaji na kutathmini hali ya mazingira katika Wilaya za Ngara, Biharamulo na Bukombe ambako kuna uharibifu mkubwa wa mazingira utokanao na msongamano wa mifugo kutoka nchi za jirani, uchimbaji usio endelevu wa madini ya dhahabu na utengenezaji wa mkaa kwa ajili ya Miji ya Shinyanga, Kahama na Mwanza. Ushauri ulitolewa kwa Halmashauri husika kuhuisha udhibiti wa uharibifu huo katika mipango yao ya maendeleo.

Aidha, Baraza liliandaa kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Utafiti wa Mazingira (*ERAC*), ili kupitia Rasimu ya Mwongozo wa Utafiti wa Mazingira. Mwongozo huu utatumiwa na Baraza kutathmini mapendekezo ya miradi ya utafiti katika utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utafiti wa Masuala ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (*NERA*), na kuwajengea uwezo maafisa mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya, ili waweze kutekeleza Ajenda ya Taifa kuhusu utafiti katika mazingira. Aidha, Baraza litaendelea kukusanya taarifa za hali ya mifumo ikolojia na kuwa na mipango ya usimamizi wa maeneo maalum ya kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Baraza liliendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa

kupitia Miradi ya: *Marine and Coastal Environment Management* Project (*MACEMP*), Tanzania Coastal *Management Partneship* (*TCMP-SUCCESS*), *Regional Programme for* the Sustainable Management of the Coastal *Zones of the Indian Ocean Countires (ReCoMaP) pamoja na Aghulus and Somali Current Large Marine Ecosystems* (*ASCLME*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Baraza liliwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango kazi ya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani katika Halmashauri zote 14 za pwani. Vile vile, kwa kushirikiana na vikundi kazi vya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani, Baraza lilifanya mapitio ya Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani, ili kuhuisha masuala muhimu yaliyoibuka karibuni kama vile mabadiliko ya tabianchi, uvunaji gesi asilia na mafuta pamoja miradi ya kilimo cha mimea kwa ajili ya nishati (*biofuel development).* Mkakati huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2010. Aidha, Baraza lilikamilisha Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira ya Pwani. Taarifa hii iko katika hatua za mwisho za uchapishaji na itatumika katika maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza kwa kupitia programu ya *ReCoMaP* limefadhili jumla ya miradi 16 inayosimamiwa na Asasi za kijamii na zisizo za kiserikali. Miradi hii yenye thamani ya *Euro* milioni 1.4 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 2.4, inalenga kuhifadhi rasilimali za pwani na bahari, kuzuia mmomonyoko wa fukwe, kuongeza kipato miongoni mwa jamii kwa kuhamasisha ufugaji wa samaki aina ya chaza wa lulu (*pearl oysters)*, nyuki, kilimo cha uyoga, mwani na ile inayolenga kuhifadhi maeneo tengefu ya viumbe baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *TCMP- SUCCESS* uliokuwa ukilenga kusimamia na kuhifadhi mazingira ya pwani na bahari chini ya usimamizi wa Baraza kwa ufadhili wa USAID tangu Oktoba, 2005 ulimalizika rasmi Desemba, 2009 na hivyo kuanzishwa kwa mradi mpya wa miaka minne wa *TCMP*-PWANI ulioanza kutekelezwa kuanzia Januari, 2010 na unatarajia kumalizika Desemba, 2013. Mradi huu unaofadhiliwa na USAID kwa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 3.8 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 5.3, unatekelezwa chini ya usimamizi wa Baraza na utaendeleza kazi zilizoanzishwa na *TCMP- SUCCESS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza kwa kupitia mradi wa *TCMP* – PWANI litaendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kusaidia uhifadhi wa Mazingira ya Pwani na Bahari na mifumo ikolojia yake katika eneo pana (*Land – Seascape)* la Bagamoyo na Pangani ikiwemo Hifadhi ya Saadani na eneo la Ghuba ya Menai, Zanzibar.

(ii) Kuendeleza juhudi za hifadhi ya maeneo yaliyotengwa ya Matumbawe (Bagamoyo) na yale ya Chaza na uzalishaji wa lulu (Ghuba ya Menai) ili kuinua hali ya uchumi kwa wanavijiji wanaozunguka maeneo hayo.

(iii) Kukuza na kuendeleza utalii wa Pomboo (*Dolphin tourism*) katika maeneo ya Ghuba ya Menai, na Utalii ikolojia/utamaduni katika maeneo ya Bagamoyo na Pangani.

(iv) Kujenga uwezo wa Wilaya na wa wananchi katika Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani na Bahari katika eneo pana (*Land- Seascape*) la Pangani na Bagamoyo pamoja na Ghuba ya Menai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza liliendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Kihansi ikiwa ni pamoja na mipango ya kurudisha baadhi ya vyura wanaohifadhiwa nchini Marekani. Kamati ya Kitaifa ya kuangalia na kusimamia zoezi la urejeshwaji wa vyura ambayo inahusisha wajumbe toka taasisi na idara mbalimbali za serikali, Vyuo Vikuu na taasisi za utafiti iliundwa mwezi Julai, 2009 na inaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ya Kuhifadhi Wanyamapori (*Wildlife Conservation Society)*, imeendelea kusaidia utekelezaji wa mpango wa mazalia ya vyura katika bustani za Bronx na Toledo zilizopo Marekani. Takwimu zinaonesha kuwa mpaka mwezi Mei, 2010 kulikuwepo na vyura zaidi ya 5,500 katika bustani hizo za Marekani. Vile vile, Baraza liliendesha warsha ya wadau wa hifadhi ya viumbe iliyofanyika tarehe 25 – 27 Februari, 2010 Dar es Salaam. Warsha hiyo ilihudhuriwa na wataalam 56 toka ndani na nje ya nchi kwa lengo la kupitia mwongozo wa urejeshaji vyura na kupanga tarehe ya kuanza zoezi la urejeshaji vyura ambalo linatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2010 kwa kurejesha takriban vyura 1,000 kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea kutekeleza mradi huu kwa kufanya utafiti na ufuatiliaji wa mifumo ikolojia ya Bonde la Kihansi kwa lengo la kubaini mazingira stahili kwa ajili ya kurejesha vyura katika mazingira ya asili. Vile vile, Baraza kwa kupitia mradi litajenga uwezo wa Wilaya zinazozunguka Bonde la Mto Kihansi pamoja na Watendaji wa Wilaya, Kamati za Vijiji na viongozi wa kidini katika masuala ya hifadhi ya mazingira na mbinu za kuboresha maisha ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza liliendelea kudumisha nidhamu na uwajibikaji wa watumishi katika kutoa huduma. Kanuni za utumishi, fedha na manunuzi zilizingatiwa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, katika kuongeza ufanisi kwa watumishi, watumishi nane wa Baraza wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi 24 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kujenga uwezo katika masuala ya utawala na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza lilikamilisha ukarabati wa majengo yaliyopo katika kiwanja chake kilichopo *Regent Estate* eneo la Mikocheni na tayari wafanyakazi wa Baraza wamehamia katika Ofisi hizo. Haya ni mafanikio makubwa kwani wafanyakazi wote wa Baraza watakuwa katika jengo moja, hali ambayo itaongeza ufanisi wa kazi na tija. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika utendaji na pia ujenzi wa jengo la kudumu unatarajiwa kuanza eneo la Mikocheni, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mazingira ni suala la mtambuka lenye changamoto nyingi zinazogusa sekta mbalimbali. Kati ya changamoto kubwa zilizopo ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira; udhibiti wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku umekuwa mgumu kutokana na mifuko hiyo kuingizwa nchini kwa njia zisizo rasmi kutoka nchi za jirani; kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati na mwitikio mdogo wa wadau katika hifadhi na utunzaji wa mazingira. Aidha changamoto za mabadiliko ya tabianchi hasa athari zake katika sekta mbalimbali zinarudisha nyuma juhudi za serikali za kupambana na umasikini na kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yanayoathirika zaidi ni maeneo ya pwani kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari; sekta ya kilimo kutokana na mafuriko na ukame wa mara kwa mara na sekta ya afya hasa kutokana kwa kuongezeka kwa magonjwa kama malaria katika nyanda za juu. Sekta nyingine ni miundombinu, nishati, misitu, mifugo, uvuvi na utalii. Aidha upotevu wa Bioanuai utokanao na ukataji miti na uharibifu wa mazingira ya bahari kwa uvuvi usio endelevu ni kati ya changamoto kubwa zinazotukabili sasa. Ushirikishwaji wa watendaji wote, Taasisi mbalimbali na wananchi kwa ujumla ni muhimu ili mipango ya kuhifadhi mazingira iendane na hali halisi ya mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha 2010/2011, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea na juhudi za kukabiliana na changamoto hizi pamoja na changamoto nyingine ambazo nimezianisha katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ilipata kibali cha kuajiri watumishi wapya 34 ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi. Aidha, watumishi 23 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo kwa kuzingatia Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Umma, watumishi kumi na mmoja wameajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni na watumishi sita walithibitishwa kazini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi inakusudia kuendelea kuwajengea uwezo, kuwapa motisha na kuwajengea ari watumishi ili kuhakikisha kuwa Wateja na Wadau wetu wanapata huduma zinazokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya utawala bora. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, kila mtumishi anapangiwa kazi za kutosha kulingana na majukumu ya Ofisi. Aidha, Ofisi iliendelea kushirikisha Watumishi katika kufanya maamuzi mbalimbali kwa kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi ambavyo vilijadili na kupitisha maamuzi mbalimbali yanayohusu wafanyakazi na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa ujumla. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itahakikisha kuwa kila mtumishi anaelewa majukumu na wajibu wake na kwamba anawajibika kikamilifu na kazi aliyopangiwa ili kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi imeweza kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa watumishi wapatao 88 kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali kwa kuzingatia kada na majukumu yao kazini. Kati ya hao, 22 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu, 32 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 34 walihudhuria mafunzo ya awali katika Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuwaendeleza watumishi kitaaluma ili wawe na uwezo wa kutosha katika maeneo yao ya kufanyia kazi na kutoa huduma kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Watumishi waliwezeshwa kufanya mazoezi ya viungo. Aidha, Wafanyakazi 60 walishiriki kikamilifu katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Morogoro. Lengo ni kuhakikisha kuwa, watumishi wanakuwa na afya bora na wanajenga mahusiano mazuri baina yao na watumishi wengine nje ya Ofisi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuwahamasisha watumishi wote kushiriki katika mazoezi ya viungo angalau siku moja kila mwezi ili kuimarisha afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendelea na ujenzi wa Jengo la Ofisi kwa Awamu ya Pili katika Kiwanja Na.10, Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais katika eneo la Tunguu – Zanzibar umefikia hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2010. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuwa na mazingira bora ya kazi kwa lengo la kuhimiza utendaji mzuri wa kazi wenye matokeo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Kuthibiti UKIMWI ikiwa ni kuunga mkono juhudi za kitaifa za kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, tunakabiliwa na changamoto ya muitikio wa watumishi kupima afya zao. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kuhamasisha watumishi kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari ili hatimaye waweze kuchukua hatua za kujikinga. Aidha, kwa wale wenye maambukizi ya VVU watapewa ushauri nasaha na matunzo ili kuhakikisha kuwa rasilimaliwatu tuliyonayo inaendelea kutoa huduma zilizo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi iliendelea kutekeleza Mpango wa Maboresho Serikalini. Maboresho hayo ni maandalizi ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati; maandalizi ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja; uanzishaji wa Miundo ya Utumishi ya fani ya mazingira; ushirikishwaji wa Sekta Binafsi kwa njia ya Mkataba katika utoaji huduma; kuweka Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji (*File Tracking System*); matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara; mapitio na maandalizi ya Mpango wa Mafunzo na uanzishaji wa Tovuti ya Ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya uwekaji wa mifumo hii, umefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi itaendelea kukamilisha usimikaji wa mifumo ya Mpango wa Maboresho Serikalini ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za watumishi na huduma zinazotolewa na kunyambulisha maeneo ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele na hivyo, kutumia rasilimali chache zilizopo katika kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Ofisi hii yamechangiwa pia na wahisani mbalimbali, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia. Napenda kuzitaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo: Serikali ya Norway, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Serikali ya Uholanzi, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo (*UNDP*), Jumuiya ya Ulaya (*EU*), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*UNEP*), Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*GEF*), Benki ya Dunia, *International Development Agency* (*IDA*), *Danish International Development Agency* (*DANIDA*), *SADC-REEP*, *Wildlife Conservation Society* (*WCS*), *World Wildlife Fund for Nature* (*WWF*) , Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), *Crop Life International* (CLI), *African Development Bank* (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani, Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba washirika wetu wa maendeleo waendelee kutusaidia katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini na juhudi zetu za kuboresha maisha ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 4,542,109,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 26: Makamu wa Rais. Kiasi hicho kinajumuisha fedha kwa ajili ya Mishahara ya watumishi, shilingi 542,953,000/= na Shilingi 3,999,156,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, naomba Bunge lako Tukufu sasa, liidhinishe makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa

Rais, Fungu 31, ya shilingi 65,011,444,000/=. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 904,088,000/= Mishahara ya Watumishi, Shilingi 40,638,341,000/= fedha za matumizi mengine na Shilingi 23,469,015,000 Fedha za Matumizi ya Maendeleo. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha fedha za ndani Shilingi 6,067,014,000/= na fedha za nje ni Shilingi 17,402,001,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ambayo ilihusika na Wizara hii, nilikuwa na matangazo ya kazi ambayo hayakutangazwa. Sasa napenda kuwatangazia Wabunge kwamba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa John Samwel Malecela anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama kwamba wanaomba wale Wajumbe wa Kamati hiyo saa tano na dakika arobaini wakutane kwenye *Speaker's Boardroom* kwa sababu wanakutana na huyu mgeni, *President* wa *Senate* ya Rwanda. Kwa hiyo kama kuna Wajumbe hawa wanatakiwa kukutana na mgeni huyo na wao ndiyo wamepewa nafasi ya kuongea na mgeni. Naomba msikose kwenda.

Nina tangazo lingine, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Ramadhan Maneno naye pia anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na Kikao leo tarehe 21 saa saba mchana kwenye ukumbi namba 227, Jengo la Utawala. Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA* Tanzania *Branch* anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo saa saba mchana baada ya kuahirisha Bunge kwenye ukumbi namba 133 na wahusika kwa majina ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Zainabu Vullu, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Omar Shekha, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Fatuma Maghimbi, Mheshimiwa Deveto Likokola na Mheshimiwa Mussa Zungu.

Tangazo lingine, hili linahusu Wabunge wote nadhani litarudiwa tena kesho kwamba Mheshimiwa Rais atafanya shughuli ya kutunuku nishani katika Uwanja wa Nyerere, Dodoma tarehe 23 Juni, 2010. Sasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atawatunuku Nishani baadhi ya watumishi, Nishani ya Utumishi wa Mrefu na Maadili mema. Tukio hili ni moja ya sherehe za maadhimisho ya wiki ya utumishi zinazofanyika jijini Mwanza. Waheshimiwa Wabunge wamealikwa kuhudhuria sherehe hizo hapa Dodoma. Kwa mujibu wa ratiba shughuli zitaanza saa kumi jioni, hivyo Wabunge wanatakiwa kuwasili katika eneo hilo saa tisa mchana.

Baada ya sherehe hiyo Wabunge wamealikwa kujumuika na Mheshimiwa Rais Ikulu Ndogo Dodoma Mjini kwenye tafrija ya kuwapongeza watumishi waliotunukiwa nishani. Hivyo, Wabunge wanatakiwa kuwasili Ikulu saa 12 jioni. Kwenye nishani saa tisa, kwenye hiyo shughuli jioni. Kwa hiyo Wabunge wote wamepewa kadi za mwaliko wa tafrija hiyo wanakumbushwa kwenda na kadi.

Kwa hiyo kuna matukio mawili, la kwanza itafanyika Uwanja wa Nyerere, jioni Ikulu ndogo saa kumi na mbili. Kwa hiyo mambo yote hayo mmekaribishwa. Suala la Bunge litafanyaje tutawaarifu baadae. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati au Makamu aliyeshughulikia Wizara hii, Mheshimiwa Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI –(K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati lakini awali ya yote nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wake wa kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya Urais leo. Hakika ni siku nyingine ya historia nchini. Rais wetu amefanya mambo mengi mema na ni kiongozi safi na makini katika kutekeleza ahadi na ilani ya chama. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais atarajie ushindi wa kishindo kutoka kwetu na kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114 (11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti, kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano inahusisha Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26 – Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika kutekeleza majukumu yake, Tarehe 01 Juni, 2010, Kamati ilikutana katika Ukumbi wa Karimjee, Mjini, Dar es Salaam, ili kupokea na Kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2009/2010 na kupitia Mpango na Makadirio Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika Kikao hicho Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, aliiambia Kamati kuhusu Majukumu, Dira na Dhima ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Mheshimiwa Waziri, pia alieleza mambo yaliyotekelezwa kwa Mwaka 2009/2010, Fungu 26 na Fungu 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2009/2010 katika Taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilikumbushwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2009/2010 Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 4,492,974,000/= kwa Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu

31 iliidhinishiwa Jumla ya Shilingi 63,397,505,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 15,870,888,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na maelezo kuhusu mwenendo huo wa bajeti, Kamati ilielezwa kuhusu kazi mbalimbali zilizofanyika kwa Fungu 26 na Fungu 31. Shughuli hizo zilihusu Masuala ya Muungano. Katika utekelezaji huo yapo mambo makuu manne yaliyojitokeza kama mafanikio. Mambo hayo ni:-

(i) Kuratibu vikao vya kutatua kero za Muungano na hatimaye kupatikana ufumbuzi wake;

(ii) Kuongezeka kwa uelewa kwa Umma kuhusu Muungano;

(iii) Kuimarika kwa ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii baina ya Pande mbili za Muungano; na

(iv) Kufikia hatua nzuri katika ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Zanzibar.

Ufafanuzi wa kina kuhusu mafanikio hayo ulitolewa na Mheshimiwa Waziri alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa kazi, Fungu 26 na 31, kwa Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, utukelezaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo saba ambayo yalihusu:-

(i) Fedha za kutosha kwa ajili ya Makamu wa Rais, kufanya ziara Mikoani;

(ii) Kazi ya muda mrefu kuhusu kushughulikia masuala ya kuchangia na kugawana Mapato na Matumizi ya Fedha za Muungano;

(iii) Kuweka utaratibu ulio wazi kwa maandishi baada ya makubaliano kuhusu ushirikiano wa Wizara;

(iv) Suala la gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(v) Sheria za Kodi ya Makampuni katika pande mbili za Muungano; na

(vi) Sura na Muundo wa Muungano katika Taasisi zote za Kimuungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu Maoni na Ushauri huo, yamo katika Maoni ya Kamati yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2009. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa mfano, kuhusu masuala ya kuchangia na kugawana Mapato na Matumizi ya Fedha za Muungano, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuwa Tume ya

pamoja ya Fedha, imekamilisha mchakato wa kitaalam wa kuchambua na kupendekeza vigezo vya mgawanyo wa mapato na uchangiaji wa gharama za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilijulishwa kuwa katika kutekeleza ushauri wa Kamati, Ofisi ya Makamu wa Rais, imekuwa ikitoa mwongozo na ratiba ya vikao vya ushirikiano kwa Wizara na Taasisi zisizo za Muungano za pande zote mbili kwa lengo la kuhimiza vikao vya pamoja vya kisekta. Hata hivyo, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuonyesha kuwa kwa Mwaka 2009/2010, vilitarajiwa kufanyika vikao 52, Taarifa ya Utekelezaji ilidhihirisha kuwa ni vikao nane tu ndio vilifanyika. Hii ni sawa na 15.4 ya lengo ambacho ni kiwango kidogo sana cha utekelezaji. Kamati inashauri kuwa Serikali ijipange vyema ili kutekeleza sehemu ya ushauri ambayo utekelezaji wake haujakamilika

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011 . Kabla ya kuomba kiasi cha Fedha, mtoa hoja alitueleza malengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, katika masuala ya Muungano. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri yalionyesha kuwa Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ufafanuzi wa kina kuhusu majukumu hayo umetolewa tena leo na Mtoa Hoja kabla ya Maoni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukamilisha na kuendelea na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yanayohusu Muungano, Mtoa hoja aliiambia Kamati kuwa Ofisi hii inataraji kukusanya maduhuli jumla ya Shilingi 39,386,775/= kutokana na Vyanzo mbalimbali. Kuhusu Makadirio ya Matumizi, Mheshimiwa Waziri aliomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 41,542,429,000/= kwa Matumizi ya Kawaida, na Shilingi 24,817,765,000/= Matumizi kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia dira, dhima na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kama alivyoeleza Mtoa hoja, Kamati ina Maoni na Ushauri wa kufanyiwa kazi katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

(i) Juhudi iongezwe ili ufanisi wa vikao vya pamoja upatikane. Aidha, Viongozi na Watendaji ambao ni muhimu katika Vikao hivyo, wahimizwe kuhudhuria ipasavyo.

(ii) Mapendekezo ya Tume ya pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofikishwa rasmi kwa Serikali zote mbili yafanyiwe kazi haraka tena kwa umakini mkubwa ili kukamilisha kazi hiyo ya muda mrefu.

(iii) Jitihada zaidi inahitajika katika kuimarisha utaratibu uliopo wa vikao vya pamoja vya Kisekta ili kuendelea kubadilishana uzoefu, ujuzi, utaalamu, sera na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya

Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa mwaka 2009/2010 na Maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Ushirikiano mkubwa alioutoa kwa Kamati wakati tulipokuwa tukichambua Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais , Bi Ruth Mollel pamoja na watendaji wengine wa Ofisi hiyo kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Kamati. Kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Kwa heshima kubwa nawatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti; Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mjumbe; Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mjumbe; Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mjumbe; Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mjumbe; Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mjumbe; Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mjumbe; Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mjumbe; Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mjumbe; Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mjumbe; Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mjumbe; Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, Mjumbe na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mjumbe.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dr. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein na Elihaika Mtui, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa kuendelea kuniamini na pia kwa familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuendelea kunitia moyo katika kazi hii ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, jumla ya shilingi 69,553,553,000/- kwa mafungu yote 26 na 31 Kati ya fedha hizo Shilingi 46,084,538,000/= zinaombwa kugharamia Matumizi ya Kawaida, na Shilingi 23,469,015,000/= kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kwanza kwa niaba ya wananchi wa Wilaya za Njombe, Makete na Ludewa niishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kutugawia

Mkoa mpya, Mkoa wa Njombe. Wananchi hao wamefurahi na wanashangilia sana kupata Mkoa mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nitumie fursa hii iliyo adimu kuwashukuru wananchi na wapiga kura wa Ludewa kwa kushirikiana na Mbunge wao kuleta mabadiliko na mageuzi makubwa katika Wilaya ya Ludewa lakini vilevile niwashukuru wananchi hao kwa kuchapa kazi kwa hali ya juu sana kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Wanasema kushukuru kunaambatana na kuomba, nina imani kabisa wananchi wale wana imani kubwa na Mbunge wao na wataendelea kuungana naye katika mchakato unaotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwasilishe taarifa ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Watendaji Wakuu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakiongozwa na Mhe. Waziri katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na kupitia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa mwaka 2009/2010 na pia kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Aidha, katika majadiliano Kamati ilifahamishwa dira na mwelekeo wa Ofisi pamoja na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina idara nne, vitengo vinne pamoja na Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais. Idara hizo ni:-

- Idara ya Mazingira;
- Idara ya Muungano;
- Idara ya Utawala na Rasilimali Watu; na
- Idara ya Sera na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vitengo vya Ofisi ya Makamu wa Rais ni Uhasibu na Fedha, Ukaguzi wa Ndani, Manunuzi pamoja na Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ina Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kujadili viambatisho vifuatavyo:-

- Taarifa ya Upandaji Miti Kitaifa Mwaka 2008/ 2009;

- Kanuni za Miongozo ya Sheria ya Mazingira;

- Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji Miti na Uharibifu Misitu (MKUHUMI);

- Miradi iliyopewa Hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) 2009/2010; na

- Taarifa ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhusu utekelezaji wa kazi 2009/2010 na kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili bajeti ya Ofisi hii, Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2010/2011, yamezingatia vipaumbele vya sekta ya Mazingira na vile vya Kitaifa ikiwemo Kilimo Kwanza; suala zima la kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010 Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali yaliyohusu sekta ya Mazingira. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika. Baadhi ya utekelezaji huo ni kama ifuatavyo:-

- Kanuni za Miongozo ya Sheria ya Mazingira;

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais imeajiri watumishi tisa wenye shahada katika fani mbalimbali zinazohusiana na hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira;

(ii) limu kwa umma imeendelea kutolewa kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali kwa kutumia njia mbalimbali kama vile programu za mazingira, maadhimisho na maonesho yanayohusu siku ya mazingira Afrika na siku ya Mazingira Duniani na pia kwa kupitia vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa;

(iii)Ofisi imefanya tafsiri ya muhtasari wa ripoti ya hali ya mazingira ya mwaka 2008 kwa lugha ya kiswahili na kusambaza nakala 1000 kwa wadau nchini. Aidha, hadidu za rejea kwa ajili ya kutafsiri ripoti kuu ya hali ya mazingira katika lugha ya kiswahili zimeshaandaliwa na tafsiri ya ripoti hii inatarajiwa kukamilika na kusambazwa katika Mwaka wa Fedha 2010/2011;

(iv)Baraza limeendelea kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira kwa miradi mbalimbali inayoanzishwa nchini. Pia hatua zimechukuliwa kwa wawekezaji wanaokiuka masharti ya TAM kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira, kwa mfano, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilitoa amri ya kurejeshwa mazingira (*Environmental Restoration Order)* kwa mgodi wa dhahabu wa North Mara na kutekeleza yote yaliyoamuliwa ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za mgodi. Aidha, tayari mgodi umeshawasilisha kwa Baraza maombi ya kuruhusiwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mtambo wa kutibu maji (*water treatment plant*) kama hatua mojawapo ya kutekeleza mpango wake wa usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imeendelea kutoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ambayo juhudi zaidi zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu mapato na matumizi kwa kipindi cha 2009/2010. Kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 Ofisi ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 4,100,000/= kama mapato ya Serikali yanayotokana na makato mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Mei 2010 makusanyo halisi ya mapato yalifikia Shilingi 34,989,260/=. Ongezeko la mapato haya yametokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni, marejesho ya masurufu na fedha za umma (*recovery of public money*) pamoja na mapato mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iliidhinishiwa na Bunge, kiasi cha Shilingi 63,397,505,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Fungu 31. Hadi kufikia tarehe 25 Mei 2010, Ofisi imepokea jumla ya shilingi 55,924,502,490/= sawa na asilimia 88 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Fungu hili.

MheshimiwaNaibu Spika, aidha, kwa upande wa fedha za Maendeleo, jumla ya shilingi 15,870,888,000/= ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 31- Mazingira ili kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2010 jumla ya shilingi 5,991,710,770/= tu sawa na asilimia 38 ya bajeti iliyoidhinishwa, zilikuwa zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2009/2010. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Ofisi ilipata mafanikio katika kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Hifadhi ya Mazingira kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi imeweza kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kukamilisha Kanuni tatu za Sheria hii ambazo ni Kanuni za Usimamizi wa Mazingira dhidi ya Athari zitokanazo na Baioteknolojia ya kisasa (*Biosafety Regulations*); Kanuni za Usimamizi wa Taka zenye Sumu (*Hazardous Waste Regulations*) na Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu (*Solid Waste Regulations*);

(ii) Ofisi imefanikiwa kutoa elimu ya hifadhi ya Mazingira kwa umma ambapo wananchi wamehamasika katika kutoa taarifa kuhusu uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kutokana na shughuli za viwanda, kilimo na uchimbaji wa madini;

(iii) Ofisi imefanikiwa kuratibu upatikanaji wa miradi mbalimbali chini ya Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira kwa Ushirikiano na Mataifa mengine, Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa unaofadhiliwa na Benki ya Dunia; Mradi wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Japan na Mradi wa kujenga ukuta wa Pangani ili kuhimili mafuriko yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unafadhiliwa chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na uko katika hatua za maandalizi;

(iv) Mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji umeanzishwa ambapo Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi imeandaliwa katika Wilaya takribani 60 nchini kusaidia kupunguza uharibifu wa ardhi nchini;

(v) Chini ya Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Fund*) miradi mikubwa minne yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 13 imepatiwa fedha kwa ajili ya hifadhi ya bioanuai; miradi mitatu yenye thamani ya dola za marekani milioni tano imepatiwa fedha kwa ajili ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na miradi midogo 14 ya vikundi vya wananchi ya kuhifadhi mazingira imepatiwa fedha;

(vi) Ukaguzi wa mara kwa mara wa viwanda na migodi ya dhahabu umefanyika ili kuimarisha shughuli za Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira na kutoa maelekezo inapobidi;

(vii) Miradi mbalimbali imeendelea kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ambapo jumla ya miradi 175 ya maendeleo ya wawekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanya TAM. Kati ya miradi hiyo, miradi 121 imefanyiwa TAM na ripoti zake kufanyiwa mapitio kwa ajili ya kupata hati za TAM;

(viii) Baraza limeendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa kutumia njia mbalimbali kama vile vipeperushi, vijarida, mabango, maonesho, luninga, radio na magazeti;

(ix) Baraza limekamilisha ukarabati wa majengo yaliyopo katika kiwanja cha baraza kilichopo *Regent Estate* katika eneo la Mikocheni na tayari wafanyakazi wa Baraza wamehamia katika Ofisi hizo; na

(x) Wataalam 49 wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na 22 wa ukaguzi wa mazingira wamesajiliwa kwenye Gazeti la Serikali (Machi 26, 2010).

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto: pamoja na mafaniko yaliyopatikana, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti usiokidhi mahitaji halisi ya shughuli za usimamizi na hifadhi ya mazingira nchini;

(ii) Udhibiti wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku umekuwa mgumu kutokana na mifuko hiyo kuingizwa nchini kwa njia za magendo kutoka nchi jirani;

(iii) Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati;

(iv) Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala mbalimbali ya mazingira;

(v) Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa kuhusu hifadhi na utunzaji wa mazingira; na

(vi) Kutotolewa fedha za wafadhili kama walivyoahidi katika bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilipata maelezo mbalimbali kutoka kwa wataalam kuhusu hatua zinazochukuliwa na Ofisi katika kukabiliana na changamoto hizo kama vile:- kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira; kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili kwa njia ya kuandaa miradi na kuboresha ukusanyaji wa takwimu za mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Ni dhahiri kabisa utunzaji wa Mazingira ni muhimu sana katika kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu hasa katika sura nne zifuatazo:-

(i) Mazingira yanaipatia nchi yetu mahitaji yote muhimu kwa ajili ya uchumi na ustawi wa jamii;

(ii) Mazingira ndio makazi ya viumbe vyote;

(iii) Mazingira ni chombo kinachopokea taka zinazozalishwa na binadamu; na

(iv) Mazingira ni msingi wa jawabu la kupunguza unyonge na umaskini.

Sekta hii ya Mazingira inahitaji msukumo wa viongozi wa ngazi zote na wananchi kwa ujumla. Kwa kuzingatia haya Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, hazijakamilika hivyo kusababisha Sheria hii kutokutumika kikamilifu. Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kuwezesha ukamilishwaji

wa Kanuni hizo ili kuhakikisha utaratibu, usimamizi na utekelezaji wa shughuli za mazingira unazingatia sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi wenye elimu ya usimamizi na utunzaji wa mazingira hasa katika Halmashauri za Miji na Wilaya. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi hao ili kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ambazo ni pamoja na uharibifu wa ardhi; upungufu wa misitu na miti; utowekaji wa mapori na upunguaji wa maliasili iliyomo na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utunzaji wa mazingira bado halipewi kipaumbele hususan katika Serikali za Mitaa. Kamati inashauri Baraza la Taifa la Hifadhi na usimamizi wa Mazingira lifanye kazi kwa karibu na watendaji wa Serikali za Mitaa ili kuboresha utunzaji wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta mbalimbali hasa zile zinazotoa nishati ya umeme na mamlaka za maji zimekuwa zikifaidika na utunzaji bora wa mazingira unaosimamiwa na Idara ya Mazingira pamoja na Baraza. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha sekta hizi zinashiriki katika kuchangia gharama za utunzaji na usimamizi wa mazingira nchini kama Sheria ya Mazingira inavyotaka ili kupunguza gharama kubwa zinazoikabili Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi katika kutoa elimu ya mazingira kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa katika utunzaji wa mazingira na pia wananchi watafaidika na mazao yatokanayo na misitu. Elimu hii itolewe kwa kutumia njia nyepesi hasa mikutano ya vijiji, radio, machapisho, vipeperushi na maonyesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi hawana uelewa kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na njia mbalimbali za kukabiliana na athari hizo. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu kwa umma kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi ili kujikinga na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko na maporomoko ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kuwa bunifu katika kuandaa mikakati mbalimbali ya kusimamia mazingira. Hata hivyo, Kamati inasisitiza mradi wa kusimamia Hifadhi ya Mabonde ujumuishe mabonde mengine nchini kwani mpaka sasa ni mabonde ya Ziwa Nyasa na Tanganyika tu yaliyo chini ya mradi huu. Aidha, mpango mkakati wa usimamizi wa taka ufanyike angalau katika mikoa yote yenye hadhi ya jiji tofauti na sasa ambapo ni miji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha tu iliyopo chini ya mkakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kutoa ushirikiano kwa Mamlaka mbalimbali nchini kama vile Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) mapema iwezekenavyo kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotarajiwa kuanzishwa hususan miradi ya afya na elimu, ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kufikiwa na huduma hizo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iliyowasilishwa na Serikali kwa mwaka ujao wa fedha (2010/2011) haitoshi ukilinganisha na kazi ya usimamizi na utunzaji wa mazingira unaoikabili Ofisi hii. Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iongezewa bajeti kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha ili Ofisi iweze kutekeleza kazi zake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya fedha kwa mwaka 2010/2011. Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka 2010/2011. Jumla ya Sh.65,011,444,000/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Fungu 31 - Ofisi ya Makamu Rais**.** Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa ajili ya Fungu 31- Mazingira ni shilingi 41,542,429,000/=, na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 23,469,015,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti; Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mjumbe; Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mjumbe; Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mjumbe; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mjumbe; Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mjumbe; Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mjumbena Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mjumbe; Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Said Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mjumbe; Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mjumbe; Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mjumbe; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe; MheshimiwaAziza S.Ally, Mjumbe; MheshimiwaLucy T. Mayenga, Mjumbe na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kwa niaba ya wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Katibu Mkuu wake Ndugu Ruth Mollel, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Ofisi hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Ofisi hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za Ujenzi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii, michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Yona kirumbi na Grace Bidya kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, na kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana kwa niaba ya Mwenyekiti sasa tunaingia Kambi ya Upinzani. Atakayeitwa kwanza ni Mheshimiwa Riziki Omar Juma, yeye atawasilisha sehemu ya Muungano, Mheshimiwa Karibu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Masuala ya Muungano) kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge toleo la Mwaka 2007, Kanuni ya 99 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia sote kuwa hapa kwenye kikao cha mwisho cha bajeti katika

awamu hii. Aidha, natoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa mtazamo wa Kambi hii. Pia naushukuru uongozi mzima wa chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*) pamoja na viongozi na wanachama wa Wilaya ya Wete kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kufanikisha kazi zangu. Mwenyezi Mungu awazidishie imani na upendo juu yangu. Amin.

Aidha, nawashukuru viongozi wangu wa Kambi chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa imani na ushirikiano wao kwangu, bila kuwasahau waheshimiwa wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wa hali ya juu katika kutimiza majukumu yangu na ya Kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda nitumie nafasi hii kumshukuru mume wangu na watoto wangu kwa kunivumilia katika kipindi chote cha miaka mitano kwa kuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, majumuisho ya miaka mitano Wakati tunamaliza Bunge hili, ni muhimu kujitathmini ikiwa miaka yetu mitano ya kuwamo humu ilikuwa na maana yoyote kwenye mustakabali wa Muungano wetu, hasa panapohusika jukumu letu sisi kama Kambi ya Upinzani. Kwa heshima, naomba nilikumbushe Taifa kupitia chombo chako hiki kitukufu kwamba jambo la msingi ambalo tulilipigania na kulisimamia ni kuwa na Muungano wenye ridhaa ya pande zote husika na wenye uadilifu. Tulipigania Tanzania Moja yenye Tanganyika Imara na Zanzibar Madhubuti. Kwetu, tuliamini na tunaendelea kuamini kuwa Tanzania ya aina hiyo inawezekana, ingawa kwa masikitiko tunakiri kwamba wenzetu walioshikilia madaraka hawajapata kuamini kuwa na Tanzania ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wa Kambi ya Upinzani, tulijaribu kutumia nafasi yetu na uwezo wetu kupigania umoja wa kweli na sio utengano, imani siyo unafiki na juu ya yote tulitaka kuona uwazi unatawala Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka yote hii mitano, Serikali hii imekuwa ikifikiri na ikitenda mambo yake bila ya kutilia maanani pande nyingine husika za Muungano huu. Katika hili, tathmini yetu inahitimisha kwamba miaka hii mitano imekuwa awamu nyingine ya kuudhoofisha Muungano wetu, kwani kwa mara nyingine suala la msingi halikuzingatiwa. Ni Mkataba wa Muungano, ambayo ni hati ya Kimataifa iliyosainiwa na wawakilishi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano na ambao hauwezi kubadilishwa kwa namna yoyote ile bila ya pande hizo kuamua hivyo katika misingi ya usawa na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka raia wa Jamhuri hii ya Muungano, watambue kwamba katika miaka hii mitano, sisi wa Kambi ya Upinzani, tulipigania kuona kwamba Mkataba huu unaheshimiwa kikamilifu. Tulithibitisha kwa hoja na mifano ya wazi

kwamba Serikali katika vipindi mbalimbali vya historia ya Muungano huu, imeukiuka, imeuvunja na kuudharau kabisa Mkataba huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani ukiwauliza Serikali watakupa mifano ya kero ambazo zimetatuliwa katika kipindi hiki, watakuambia kwamba mwezi uliopita paliwekwa saini baina ya Serikali mbili kwamba masuala ya Uvuvi wa Bahari Kuu na Tume ya Haki za Binaadamu yametatuliwa na kuondoshwa katika Orodha ya Kero hizo. Ukweli ni kuwa, hata mifano hii yenyewe inaonesha namna ambavyo moyo wenyewe wa Muungano unavyovunjwa. Kwa sababu kwanza, kutokana na mifano hii, tafsiri halisi inayopatika ya kutatua kero za Muungano, ni kuyafanya mambo yasiyo ya Muungano yawe ya Muungano. Kwa maneno mengine, ni kuendelea kudhoofisha mamlaka na madaraka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili**,** ikumbukwe kwa miaka yote hii minne si kwamba juu ya meza palikuwa na kero hizo mbili tu za Muungano. Zipo nyingi tu, zikiwemo, Mafuta na Gesi Asili, Kuongezeka na Tafsiri ya Mambo ya Muungano, Ajira za Wazanzibari katika Taasisi za Muungano; Uwezo wa Zanzibar Kukopa Nje; Gawio la Zanzibar katika Mali za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB); Utozwaji Kodi mara mbili kwa Wafanyabiashara wa Zanzibar; Utaratibu wa Zanzibar kuwa na Ushirikiano wa Kimataifa na Nchi za Nje na Mashirika ya kimataifa kwa lengo la kunufaika na fursa za kichumi na Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya na hatimaye Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tutakubiliana na kujiaminisha kuwa kinachofanywa na Serikali, ni kutatua kero za Muungano, hivi Serikali ya CCM ituambie inahitaji miaka mingapi mengine kutatua kero zilizokwisha orodheshwa ikiwa kasi yake ya utatuzi ni wastani wa kero moja tu kwa miaka miwili mizima?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu, ni ule ukweli tuliousema mwaka jana hapa, kwamba Kamati ya Makamu wa Rais haina uhalali wa kisheria. Katiba yetu haisemi popote kwamba chombo hiki kipo na kwamba kina nguvu gani. Ni chombo cha ushauri tu ambacho ufanyaji kazi na mafanikio yake yanategemea zaidi dhamira njema na kama tulivyosema kwenye hotuba yetu ya mwaka juzi, dhamira hiyo njema haionekani kuwepo, hasa hasa kwa upande wa Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo sababu katika hotuba yake ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka huu, Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Uchumi wa SMZ alisema wazi kwamba SMT bado haijawa tayari kuzungumzia masuala ya gawio la SMZ kwenye EACB, faida ya Zanzibar kwenye mtaji ulioanzisha Benki Kuu ya Tanzania, haki ya Zanzibar kupata zaidi ya asilimia 4.5% ya gawio la misaada ya nje na mengine mengi yenye manufaa ya moja kwa moja ya kiuchumi kwa Zanzibar na Serikali ya Muungano. Tunachokisisitiza hapa ni kwamba msingi wa Muungano unapaswa kuwa ni haki sawa kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa sababu hizo tatu, Kambi ya Upinzani haiwezi kuwa sehemu ya wawakilishi wa wananchi wanaoongeza matatizo ya wananchi hao badala ya kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tulijaribu kuonesha hofu yetu kuu tuliyonayo kwamba Serikali ya Muungano inajifanya kutia pamba masikioni na kudharau kabisa historia na uhalisia wa Muungano wenyewe, kwamba ni matokeo ya madola mawili huru kukasimu baadhi ya mamlaka yao katika mamlaka ya pamoja, huku madola hayo yakibakia na sehemu nyingine za mamlaka yake. Hili la Tanganyika na Zanzibar kukasimu baadhi tu ya madaraka yao kwa Muungano, tulilisema na kulirudia kwa kujiamini, maana hivyo ndivyo ilivyo unapoangalia Mkataba wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka pia raia wa Jamhuri hii ya Muungano watambue kwamba katika kipindi hiki tulipigania kuona kwamba hoja ya Muundo mpya wa Muungano wenye Serikali Tatu yaani ile ya Tanganyika, ya Zanzibar na ya Muungano, inarudi Bungeni na inakuwa sehemu ya kumbukumbu za chombo hiki Kitukufu. Tulilikumbushia na tulilitukuza kundi la Wabunge 55 wa Bunge hili Tukufu ambao katika miaka ya 1990 waliwahi kupitisha hoja ya haja ya kuwepo kwa Serikali ya Tanganyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hebu sikiliza, hakuna mahali Bunge lilipitisha hoja ya Wabunge 55, hakuna.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA, MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Raia wa Jamhuri hii ya Muungano wafahamu kwamba katika kipindi walichotuweka humu Bungeni, tuliuweka wazi upungufu uliomo katika Katiba ya 1977 hasa sehemu inayohusu Muungano, miongoni mwa upungufu tuliouweka wazi, ni ule wa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo tulisema wazi kwamba Mabadiliko ya 11 ya Katiba yaliyomwondoshea nafasi hiyo Rais wa Zanzibar yalikuwa batili kwa dhati yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba mabadiliko yale yalifanywa kwa hofu ya Serikali ya Muungano kukiogopa kivuli chake chenyewe vinginevyo, hapakuwa na hoja wala haja ya kuuvunja Mkataba wa Muungano kwa kisingizio cha kuwa eti ingewezekana pande hizi mbili za Muungano zikawa na Marais kutoka vyama tafauti, baada ya kurudi tena kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Kwa hivyo, tulidai na bado tunadai kwamba Rais wa Zanzibar arudi katika nafasi yake ya kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kama yalivyo matakwa ya Mkataba wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka raia wa Jamhuri hii ya Muungano wazingatie kwamba tuliihoji nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano tukieleza namna ambavyo nafasi hiyo isivyokuwa ya Muungano, kama vile tulivyohoji

matumizi ya jina la 'Tanzania Bara' badala ya Tanganyika ndani ya Muungano, Akaunti ya Pamoja ya Fedha, Mahakama ya Katiba na nafasi na uwezo wa Jaji Mkuu na Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kote huko hoja yetu ilikuwa rahisi kufahamika na ya wazi, mambo mengi yamevungwavungwa ndani ya kijaluba kimoja hata sasa ni shida kusema, kipi ni cha Muungano na kipi si cha Muungano. Imekuwa haitegemei tena Makubaliano ya wenye Muungano huo kama yanavyoelezwa kwenye Mkataba, bali kinategemea watunga mikakati wa Serikali ya Muungano wamelalia na kuamkia ubavu gani. Huko, kwa hakika, ni kwenda kinyume kabisa na ari hasa ya Muungano. Ndio maana hakuna la ajabu kwamba hakuna jirani hata mmoja wa Jamhuri hii ambaye amewahi kutamani kujiunga nasi kwa miaka yote hii 46, maana Muungano wetu unawatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tungetaka raia wenzetu wa Jamhuri hii ya Muungano waelewe kwamba tulihoji uhalali wa kisheria na wa kisiasa wa vikao vya pamoja kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wa Zanzibar vinavyoratibiwa chini ya Ofisi wa Makamu wa Rais. Hoja yetu ilijengeka juu ya dhana halisi ya Muungano wenyewe. Kwamba, kwanza, huu ni Muungano wa Madola mawili huru ya Tanganyika na Zanzibar na pili**,** ingawa Ofisi ya Waziri Kiongozi inaweza kuwa inawakilisha upande wa Zanzibar kama mshirika wa Muungano, Ofisi ya Waziri Mkuu haiwezi kuwa inawakilisha upande wa Tanganyika, ambaye ni mshirika mwingine wa Muungano; maana hii tunavyoambiwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo Zanzibar ni mshirika wake. Kwa ufupi ni kusema wanaokutana kuzungumza sio hasa waliopaswa kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie nukta hii kwa kuwathibitishia Watanzania wenzetu kwamba sisi wa Kambi ya Upinzani tulitimiza wajibu wetu. Tulihoji pa kuhoji, tulikosoa pa kukosoa na tulielekeza pa kuelekeza. Bila ya shaka, lilipotokea la kusifu na kuunga mkono, tulifanya hivyo, lakini lazima tukiri kwamba hayo yalikuwa ni machache sana, maana katika suala la Muungano huu, Serikali imeharibu mengi kuliko kutengeneza. Sisi tulitimiza wajibu wetu kwa kadiri ya nguvu na mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtikisiko wa Muungano mwaka 2005 – 2010, katika hotuba maarufu ya Rais Jakaya Kikwete hapa Bungeni ya Disemba 30, 2005, alizungumzia dhamira yake ya kuulinda, kuudumisha na kuuimarisha Muungano. Miaka miwili baada ya hotuba hiyo, Muungano ukaanza kukumbwa na dharuba ya kwanza ikitokea ndani ya Chama na Serikali yake mwenyewe. Ilikuwa ni pale Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alipotamka humu Bungeni kwamba Zanzibar si nchi. Pili ni pale Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lilipoamua kuzungumzia kwa uwazi suala la nishati za mafuta na gesi asilia na kutaka liondolewe kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano. Mambo haya mawili ndiyo migogoro mikuu ya waziwazi iliyoutikisa Muungano wetu ndani ya awamu hii. Yote mawili yalizua miito ya ukinzani kutoka pande husika na kila upande uliamini kwamba unasimamia jambo la haki na, au, la kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri ni kuwa msimamo wetu katika masuala kama haya huwa unajulikana wazi na hata unaweza kutabirika. Kwa sababu ya Sera ya Mfumo wa Shirikisho la Serikali Tatu tunayoisimamia, Kambi yetu imekuwa kila siku ikizitambua hadhi mbili za Zanzibar kama nchi na kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Tunaitambua Tanganyika katika upeo huo huo na kwa sababu ya sera ya kiuchumi tunayoitetea, tunaamini pia kwamba nchi yenye sifa hizo ya Zanzibar, ina jukumu la kusimamia rasilimali zake yenyewe kwa mustakbali wa watu wake na vizazi vyao. Juu ya yote, tunataka kuona kuwa mjadala mpana, wa kiadilifu na wa wazi na wenye dhamira ya kujenga unaendelezwa kuhusu masuala haya, kusudi hatimaye papatikane Muafaka wa Kitaifa kuhusu Muungano mzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yetu kwamba, tutakuwa tunajidanganya wenyewe tukidhani kwamba mambo haya mawili yamepitwa na wakati. Ni makosa zaidi kuamini kuwa yalipozuka yalizuka kwa bahati mbaya na kwamba yalikuwa masuala ya jazba. Kwa kuwa yenyewe hayakuzungumzwa yakamalizwa, tukae tukijua kwamba tunamaliza miaka yetu mitano ya kuwepo kwenye nafasi tulizo nazo, tukiwa tumeuacha mgogoro mmoja mkubwa sana kuwahi kutokea kwenye Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano na Wazanzibari, kwa siku nyingi huko nyuma, ufahamu wa wengi ulikuwa ni kwamba muingiliano wa kisiasa baina ya Tanganyika na Zanzibar ulianza baada ya Muungano huu, Aprili 1964. Lakini kutokana na rekodi za kihistoria ambazo sasa zimekuwa zikikusanywa na kuwekwa wazi na wanahistoria, ufahamu huu unatanuka na leo inajulikana kwamba muingiliano huo ulianza kabla ya Muungano wenyewe na kwamba ambacho kimekuwa kikitokezea ndani ya miongo hii minne na nusu ya sasa ni muendelezo tu wa kile kilichoanzishwa hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna maandiko kama vile kitabu cha ”Kumbukumbu za Masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo”, ”*The Partner-ship*” cha Mzee Aboud Jumbe, ”*Pan Africanism or Pragmatism*” cha Profesa Issa Shivji na cha karibuni zaidi ni ”Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru!” cha Dkt. Harith Ghassany. Maandiko yote haya yanataja kwa namna moja ama nyingine, namna siasa au viongozi wa siasa wa upande mmoja wa Muungano walivyowahi kuwa na athari kwenye upande mwengine.

Mheshimiwa Spika, athari njema na mbaya za muingiliano huu zinaweza kuorodheshwa kwa kadiri muorodheshaji anavyodhamiria. Si lengo la hotuba yetu ya leo kuzizungumzia kwa undani athari hizo, lakini itoshe kusema kwamba kila upande kati ya pande mbili hizi za Muungano, yaani Tanganyika na Zanzibar, una nafasi ya kuzisawiri au kuziathiri, kuzitengeneza au kuziharibu, siasa za upande mwingine. Kwa hivyo, linabakia kuwa jukumu la kila upande kuuangalia upande mwingine wa pili kwa jicho la urafiki, udugu, huruma na upendo kwamba wetu ni Muungano wa washirika na wala sio Muungano wa Wapinzani. Ni Muungano wa marafiki uliotokana na ridhaa zao wenyewe na wala si Muungano wa wababe wa kivita ambapo mmoja alimshinda mwenzake na kumuweka chini ya himaya yake kwa lengo la kumdhibiti asije akanyanyuka tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunatambua kwamba kwetu ni kuungana sio kutawaliana, kwa hivyo, hatuna na wala hatutakiwi tuwe na ushindani na ukinzani wa kudhibitiana na kuwekana katika wakati mgumu. Sote, Tanganyika na Zanzibar, tunapigania hatima ya pamoja, ambayo ni kuliona eneo hili la Afrika ya Mashariki likipiga hatua za kimaendeleo ya kiuchumi, ya kisiasa na ya kijamii ambayo yatakuwa kioo cha kuwavutia wengine wa Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tungependa kuweka msimamo wetu juu ya nafasi ya Zanzibar iliyo kwenye Muungano ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mambo matatu ndiyo yanayoleta utata, kwanza**,** maeneo yaliyoorodheshwa kuwa ya mahusiano kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni 17, ambapo kati ya hayo ni manne tu ndiyo mambo ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa yale yaliyobaki 13, Zanzibar ina mamlaka yake kamili juu ya mambo hiyo kwa mujibu wa Makubaliano ya Muungano na hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 102.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili**,** uhusiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaingia katika kigawe (*category*) cha mahusiano ya Kimataifa, ambalo lenyewe si jambo la Muungano. Tatu**,** hata itokezee kwamba Jumuiya hii inaingia katika kigawe cha Mambo ya Nje, ambalo ni jambo la Muungano, basi bado Serikali ya Muungano haina uhalali wa kuiwakilisha Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, angalau katika yale mambo ambayo si ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu kubwa inayojengeka sasa kwa Zanzibar ni kwamba, mwenendo wa kulazimishana unaonekana kuchukuliwa kwenye kasi ya kuelekea Shirikisho utaishia kwenye kuzusha mfumo wa Serikali Moja kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maana ikiwa tutaendelea hivi na kukichukua kila cha Zanzibar na kukiwakilisha chini ya mwamvuli wa Muungano, mwisho wa siku hapatabakia na chochote cha Zanzibar. Jumuiya hii ya Afrika Mashariki inathibitisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Kituo cha Katiba cha Afrika Mashariki chenye makao makuu yake mjini Kampala, Uganda iliyochapishwa mwezi wa Aprili mwaka huu, inaonya kwamba nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanapaswa kujifunza makosa makubwa yanayofanyika ndani ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa kweli wanataka Jumuiya hii idumu na iimarike.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa makosa yanayotajwa na ripoti hiyo ni ukweli kwamba hisia na mawazo ya upande mmoja wa Muungano hazipewi nafasi katika kuuendesha na kuutawala Muungano wenyewe. Tabia hii ya kuyachukulia mambo kifichoficho au kwa kuyavungavunga ni mbaya sana kwenye ushirikiano wa pande zaidi ya moja. Unapokosekana uwazi wa kutosha katika mahusiano, shaka na dhana mbaya ndio huchukua nafasi badala ya nia njema na kuaminiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuipa nafasi Zanzibar kama Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni tatizo lingine linalosubiri kuchipuka kwenye Siasa za Nje na Mashirikiano ya Kimataifa za Tanzania. Kwa upande mmoja, Wazanzibari wanataka kuiona nafasi yao wenyewe ndani ya Jumuiya ili waweze kusimamia vema maslahi yao kwa yale mambo yasiyo ya Muungano. Kwa upande mwingine, siasa za Muungano kuelekea Zanzibar zinazosimamiwa na Serikali ya Muungano haziruhusu kuiona Zanzibar inajenga ushirikiano wake yenyewe nje ya mipaka ya Tanzania hata kwa yale mambo yasiyo ya Muungano huku ikieleweka kwamba hata unapoangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ushirikiano wa Kimataifa si jambo la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu ambayo inajengeka kwa mkabala huu wa Serikali ya Muungano kuelekea Zanzibar, inaweza kuwaathiri washirika wengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao wanaweza nao kuhofia jaala za mamlaka yao kama wataingia kwenye ushirikiano wa ndani zaidi na nchi ambayo inaweza kujifanya Kaka mkubwa na kuwachukulia majirani zake kama watoto wadogo ambao hawawezi kujisimamia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaweza kufahamika kwamba kuna hofu pia kwa upande wa Serikali ya Muungano, ambao unaona hatua yoyote ile ya Zanzibar kutumia haki yake ya kuingia kwenye Ushirikiano wa Kimataifa kutaathiri mamlaka ya Serikali yenyewe ya Muungano na hivyo kuhatarisha au kuuvunja kabisa Muungano wenyewe. Ndiyo hoja iliyotumiwa wakati ule Zanzibar ilipolazimishwa kujitoa kwenye Jumuiya ya Nchi za Kiislam (*OIC*), hoja ambayo imeshafafanuliwa kwamba ilikuwa potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa hofu hii isiyo na msingi kwa upande wa Serikali ya Muungano, kunaathiri sana mfumo wa Muungano, maana ule msingi wa ukweli na ridhaa ya hiyari wa Muungano unakosekana. Msingi huo ni mapenzi na kuaminiana. Tunapofika mahali sisi wenyewe tukiwa kwenye Muungano hatuaminiani na badala yake tunategana mitego na kuviziana, tujuwe kwamba tumefika katika kilele cha udhaifu wa Muungano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maridhiano ya Wazanzibari, mwaka uliomalizika wa 2009 ulimalizika kwa matumaini mapya na mwaka huu wa 2010 ukaanza kwa matarajio ya milango ya kheri kufunguka Zanzibar. Hii ni baada ya viongozi wakubwa wa vyama viwili vya siasa vyenye ushawishi wa siasa za nchi hii kuamua kukutana na kuanzisha mazungumzo ambayo sasa yamezaa kile kinachoitwa Maridhiano. Sisi wa Kambi ya Upinzani tunawapongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*), Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuongozwa kwao na maslahi makubwa na mapana ya kinchi na kizalendo na kuamua kuweka nyuma hisia na maslahi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu wa Muungano, tunachukua fursa hii na kwa namna ya pekee, kumshukuru sana sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, ambaye akiwa kama Kiongozi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

ameonesha uelewa wa hali ya juu na akaziunga mkono jitihada za viongozi wenzake wa Zanzibar. Tunaamini kauli zake za mara kwa mara za kutia moyo ambazo amekuwa akizitoa kuhusiana na Maridhiano ya Wazanzibari, zinatoka moyoni mwake na kwamba kutokana na kuziunga mkono kwake kwa kila hali, basi nchi hii itajikwamua kutoka jinamizi la miaka zaidi ya hamsini la mgogoro wa kisiasa Zanzibar. Tunaamini Rais Kikwete anaongozwa na hekima yenye kuiona Zanzibar iliyoungana na iliyotulia kuwa ina maslahi zaidi kwa Muungano kuliko Zanzibar iliyogawika na kuchafuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nichukue nafasi hii kupitia Bunge hili Tukufu, kuwaomba Watanzania wenzangu popote walipo na katika Chama chochote cha Siasa walicho, waisaidie Zanzibar iondokane na balaa na badala yake, kwa kutumia Maridhiano haya, iinuke na istawi vyema. Nina hakika kwamba Zanzibar ya aina hiyo ndiyo inayotakiwa na kila mwenye nia njema na Muungano wetu. Nitumie fursa hii basi kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar waongozwe na hekima, busara na moyo wa umoja na upendo wakati watakapokuwa wanapiga kura ya maoni tarehe 31 Julai, 2010 kuhusu Maridhiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maridhiano ya Wazanzibari yametupa fundisho moja kubwa sana, kwamba penye nia na dhamira ya kweli na kutanguliza maslahi ya Taifa mbele, hakuna lisilowezekana. Hakuna asiyejua miongoni mwetu kiwango cha uhasama na kutoaminiana kilichokuwepo kati ya viongozi na wanachama wa CCM na CUF. Leo tumeweza kuibadilisha hali hiyo na kila mwenye kuitakia kheri Zanzibar na Tanzania hawezi kufanya juhudi za dhahiri au za chini chini za kutaka kuturejesha kule tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi, tutumie mfano huu na kwa misingi hiyo hiyo niliyoitaja hapo juu, ili sasa baada ya kuwa na Maridhiano ya Wazanzibari, tuwe pia na Maridhiano ya Muungano yatakayoupa Muungano wetu haiba na sura mpya katika hali ya umoja wa dhati na upendo wa kweli uliojengeka juu ya udugu wa asili wa watu wa pande mbili hizi za Muungano. Hili linawezekana ikiwa tutakuwa tayari kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kama nilivyotangulia kusema, hiki ni kikao cha mwisho cha Bajeti kwa kipindi hiki cha Bunge, huenda tukarudi tena hapa mwakani, huenda tusirudi. Turudi ama tusirudi, ni muhimu sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wakati aliotupa wa kuwatumikia Watanzania wenzetu katika kiwango hiki cha kuwawakilisha katika chombo kinachohusika na maamuzi ya kuiendesha nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kukumbusha kwamba Muungano huu ni kitu kizuri ambacho kinastahiki kuendelea kuwepo na kudumishwa, lakini kuulinda na kuuimarisha Muungano hakumaanishi kuongeza orodha ya Mambo ya Muungano na kupunguza mamlaka ya upande husika bali kunahitaji kuheshimiana na kuheshimu mamlaka ya kila upande. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu mambo ya mazingira, Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF, MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Sekta hii muhimu ya Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kwa ushauri wao na hususan kwangu tokea mwanzo mwa kipindi hiki cha Kikao cha Bajeti hadi sasa ninapowasilisha hotuba hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vile vile ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wanachama wenzangu wa Chama cha *CUF* katika Jimbo langu la Mkoani kwa kunipa ushindi mkubwa katika kura za maoni na kuwa mshindi wa kwanza. Nipo pamoja nao na sitawaangusha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa wanakuonea wivu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF, MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA**: Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, natoa shukrani na pongezi kwako wewe Naibu Spika, Spika na Wenyeviti wote, kwa kazi kubwa ya kuliongoza vyema Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira yana uhusiano mkubwa wa maisha ya binadamu, misitu na wanyama. Kwa hivyo uharibifu wa mazingira kwa njia yoyote ile una uhusiano mkubwa na maisha ya viumbe vyote hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya kilimo inachukua asilimia 45.6% ya pato la Taifa na asilimia 50% ya pato la fedha za kigeni. Sehemu kubwa ya kilimo hicho kinafanywa na wakulima wadogo wadogo wapatao 4.8 millioni ambao wamesambaa katika nchi nzima. Wakulima karibu wote hawana utaalamu wa kilimo bora, hawajui kama utumiaji wa mbolea za chumvi kwa wingi na kwa muda mrefu kuwa ni hatari kwa udongo. Hivyo basi, gharama ya kuirudisha ardhi katika hali yake ya asili itahitajika kutumia rasilimali nyingi sana. Matatizo hayo ya matumizi ya muda mrefu ya mbolea za chumvi kwenye eneo moja yameanza kujitokeza hasa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambapo wakulima bila ya kutumia mbolea hawawezi kupata mazao (mavuno) kulingana na eneo lililolimwa. Katika kuendeleza dhana ya kuhifadhi mazingira, Kambi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo la umuhimu mkubwa kwa Serikali kuhamasisha wakulima wetu hasa wale ambao ni watumiaji wakubwa wa mbolea za chumvi chumvi kubadilisha utaratibu huo na kuanza kutumia mbolea zetu za asili zisizo cha chumvi chumvi kwa lengo la kuirejesha ardhi katika hali yake ya uasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inasema kuwa bila uhifadhi wa udongo hakuna uhifadhi wa mazingira, kwa maana kwamba udongo ndiyo rasilimali mama katika kadhia nzima ya mazingira. Ipo haja Serikali kuliona hilo na watueleze watachukua hatua gani kulirekebisha tatizo hili ambalo kwa sasa wakulima wa Songea na Mbeya linawaathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu asilimia 92% ya nishati ya kupikia hapa nchini inatokana na kuni na mkaa na asilimia 80% ya nishati ya kuni na mkaa inatumika vijijini. Kwa kutegemea nishati hiyo, kwa kiasi kikubwa inaleta uharibifu mkubwa wa mazingira ambapo matokeo yake miti inakatwa kwa wingi na kusababisha ukosefu wa mvua na mmongonyoko wa ardhi. Bila ya kuwa na nishati mbadala ya kupikia ukiachana na kuni na mkaa suala la uhifadhi wa mazingira litakuwa la ndoto. Je, Serikali imejipanga vipi katika kupata nishati mbadala?

Mheshimiwa Naibu Spika, maji Baridi na Mazingira *(Fresh Water And Environment),* kiasi cha asilimia 50% ya maji kwenye mito ya Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji, Mbwemkuru na Ruvuma, inamwaga maji yake kwenye Bahari ya Hindi. Asilimia 50 iliyobaki ya maji ya juu ya ardhi yanamwaga maji hayo katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira katika maziwa na mito hiyo. Uchafuzi huo unaonekana kwa kupungua kina cha maziwa na mito hayo kutokana na mmongonyoko wa ardhi, ukataji wa misitu, uvuvi usio endelevu kwa kutumia zana zisizofaa na katika maeneo ya miji na ya viwanda, uchafuzi unafanyika katika maji kuwa na kemikali na uchafu kutoka kwenye makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ni la kwanza kwa urefu duniani lina km. 683 na ni la pili duniani kwa ujazo wa maji baridi, lina $km^3$ 18,900 linahifadhi asilimia 17% ya maji baridi duniani. Tanzania inamiliki asilimia 41% ya Ziwa hilo, hivyo ni hazina kubwa, ipo haja kulindwa kwa nguvu zote. Hivi sasa kumeanzishwa ujenzi wa nyumba mita chache kutoka kwenye Ziwa lenyewe. Hivi sasa itaonekana hakuna athari ya ujenzi huo kwa sababu ujenzi wa nyumba ni chache lakini hali itabadilika kadri ujenzi utakapoendelea. Je, Serikali inasemaje kuhusu ujenzi huu? Je, Sheria inayohusiana na masafa maalum ya kujenga kwenye vyanzo vya maji haipo tena? Kambi ya Upinzani inataka maelezo kutokana na suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya bahari na mazingira, Tanzania ina ukanda wa bahari wenye urefu 800 km kutoka mpaka wa Msumbiji, Kusini mwa Tanzania na Kenya, kaskazini mwa Tanzania. Karibu ukanda wote huo unaonekana una mikoko ambayo ndio mazalia ya viumbe mbalimbali. Pia katika bahari, yanaonekana matumbawe ambayo ndio mazalia na malisho ya aina nyingi za samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu mkubwa wa mazingira ya bahari unaonekana katika ukataji wa mikoko, mmomonyoko wa fukwe za bahari, uchafuzi wa maji kutokana na maji machafu kuelekezwa baharini. Serikali ina mpango gani wa kuepuka uchafuzi wa mazingira katika eneo la bahari?

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa madini na mazingira, nchi yetu hivi sasa kuna uchimbaji mkubwa na mdogo wa madini katika maeneo mbalimbali. Tanzani ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa dhahabu katika Bara la Afrika ukiachana na Afrika ya Kusini. Uchimbaji mdogo na mkubwa, una athari kubwa kwa mazingira kama hatua za kupunguza athari hizo hazitachukuliwa. Uchimbaji mdogo, kuna kusambaa kwa zabaki (*mercury*) katika maji kwani zabaki hiyo inatumika kwa usafishaji wa dhahabu, pia uchimbaji mkubwa kuna athari ya vumbi, uvujaji wa kemikali, milipuko ya baruti, mchangayiko wa kemikali ambapo baadaye huwa sumu. Inabidi Baraza la Hifadhi la Mazingira (*NEMC*) liwe karibu sana na migodi hiyo ili kuhakikisha yaliyotokea katika Mgodi wa *North Mara* hayatatokea tena na si kwa *North Mara* tu bali kwa migodi yote. Bado, wafanyakazi wa Baraza la Hifadhi la Mazingira ni wachache. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha wanapatikana wafanyakazi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hewa na mazingira, uharibifu wa mazingira nchini si unaleta athari katika ardhi na maji tu lakini pia unachafua hewa na kusababisha madhara makubwa kwa afya ya wanadamu na viumbe vingine hai ambavyo hutegemea hewa safi ili waweze kuendelea kuishi. Uharibifu wa hewa kwenye viwanda vya kawaida na viwanda vya saruji, inaleta athari kwa wananchi kwa uvutaji wa hewa chafu. Hii inaonesha taasisi zinazoshughulikia mazingira zimeshindwa kabisa kuzuia uharibifu huu wa hewa unaosababishwa na viwanda nchini, kwani viwanda vya saruji, kituo cha uchimbaji wa makaa ya mawe Kiwira katika Wilaya ya Tukuyu watu wengi wanaoishi karibu na maeneo haya, afya zao ni za mgogoro kwani viwanda hivi hutoa gesi za *sulphur dioxide*, *nitrogen oxide* na *hydrocarbon* ambazo zina madhara makubwa kwa afya za wakazi hao ambazo huweza kusababisha hata maradhi ya saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaikumbusha Serikali na taasisi zinazohusika kuwa maendeleo ya nchi yoyote hupatikana kwa wananchi kuwa na afya nzuri kwani hii ndio inayoongeza uzalishaji na hatma yake ni kupungua kama si kuondoa kabisa tatizo la njaa na umaskini. Hivyo, Serikali isiangalie zaidi faida wanazopata kutokana na viwanda hivyo bali wajali zaidi afya ya wana jamii ambao ndio walengwa wakubwa wa maendeleo hayo yanayotafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabia nchi, ni mabadiliko yanayotokezea juu ya uso wa dunia kwa kasi na kwa muda mfupi (mfano mafuriko, vimbunga, ukosefu wa mvua mfululizo) ama yanayotokea taratibu na yanayochukuwa muda mrefu ambayo ni ya kudumu kutokana na ongezeko la gesi joto zinazozalishwa na shughuli za binadamu. Kwa ujumla, mabadiliko haya yanarudisha nyuma maendeleo ambayo yamepatikana katika Bara letu la Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi yetu, utafiti uliofanywa nchini kote umeonyesha joto limeongezeka kwa nyuzi joto $0.2^{0}$C na kwa Nyanda za Juu Kusini ni nyuzi joti $0.6^{0}$C. Athari ya mabadiliko ya tabia nchi, yanaanza kuonekana katika nchi yetu kama ifuatavyo:- Malaria sasa iko katika maeneo ya baridi ambapo haikuwepo kabisa; Ziwa Rukwa limerudi ndani kwa kilometa saba; Uyeyukaji wa theluji Mlima Kilimanjaro hadi mwaka 2025 theluji yote katika kilele cha Kibo itakuwa imekwisha

kabisa; maji ya chumvi yanaingia katika visima vya maji baridi katika Ukanda wa Pwani Bagamoyo Pangani na Rufiji; kutoweka kwa Kisiwa cha Maziwe (Pangani) na Fungu la Nyani (Rufiji); Ukuta wa Pangani sasa maji yanapita juu wakati wa maji kujaa na kuhatarisha maisha ya wakazi wa mji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Kilimanjaro, ni urithi mkubwa kwa nchi yetu. Mlima huo una mchango mkubwa kiuchumi kwa kuchangia asilimia kubwa katika pato la nchi hii, vivyo hivyo kwa kuendesha maisha ya wananchi wa Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Serikali yetu lazima iwe na mikakati madhubuti ya kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia nchi, haitoshi kuridhia mkataba wa mabadiliko ya tabia nchi na itifaki ya Kyoto peke yake. Je, Serikali imefanya miradi gani kama nchi kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Siku ya Mazingira Barani Afrika, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Afrika yalifanyika 3/3/2010 Jijini Arusha ilijikita kwa undani kuangalia ni jinsi gani Bara la Afrika, linaweza kutumia njia za asili katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho hayo yalitoa msisitizo kwa kuonyesha madhara ambayo yatatokea kiuchumi na jinsi gani yanaweza kukabiliwa ili kupunguza athari hizo kwa maisha ya kawaida ya mwananchi. Pia yalisisitiza umuhimu wa uhifadhi wa mazingira katika kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo ambayo hutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa. Nchi za Bara la Afrika ndizo zilizomo katika athari kubwa ya matokeo ya Mabadiliko ya Tabia Nchi kwa ujumla kwa kulinganisha na nchi kwenye Mabara mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa, matumizi bora ya mbolea za asili pamoja na usimamizi katika matumizi mazuri ya rasilimali zetu, ndio njia pekee itakayotufanya tukabiliane kikamilifu na mabadiliko ya Tabia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wachangia mpaka sasa wako watano tu nao ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa kwanza katika mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa 2010, Muungano wetu umetimiza miaka 46 tangu ulipoundwa. Tukifuatilia mijadala, tutaona siku zote imetawala na malalamiko yasiyokwisha baina ya pande mbili za Muungano. Mimi nadhani wakati umefika sasa Tanzania na pande mbili za Muungano, Tanganyika na Zanzibar, zibadilishe mtazamo na kutafuta suluhisho la tatizo hili ambalo limekuwepo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kwamba suluhisho la matatizo haya litapatikana kwa njia ya *truth and reconciliation (*ukweli na maridhiano).

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, jina la nchi hizi ni Tanzania na Tanzania Zanzibar, hakuna Tanganyika.

**NAIBU SPIKA:** Hata mimi Msemaji wa Kambi ya Upinzani nilikuwa namshangaa sana, jina Tanganyika kalitoa wapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Jussa endelea.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Zanzibar tunasema jina si mboje, kwa hiyo, si tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema Muungano huu, kwa lugha aliyopendelea rafiki yangu tunayetoka Jimbo moja, wa Tanzania Bara na Zanzibar ingawa Hati ya Muungano ambayo bado ni halali, inatambua hizo pande mbili nilizozitaja awali, umetimiza miaka 46 na tunahitaji tubadilishe mtazamo. Mimi naamini kwamba njia inayofaa kabisa ni njia ya ukweli na mapatano au maridhiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapokuwa na nia njema, kama ilivyosema Hotuba ya Msemaji wa Upinzani, hakuna ambalo haliwezekani. Tumeona katika mfano mzuri sana wa Afrika Kusini walikuwa na mgogoro wa muda mrefu sana wa ubaguzi wa rangi lakini siku walipoamua kukubali na wakaamua kuleta mapatano na maridhiano, sasa hivi Afrika Kusini ubaguzi wa rangi umekuwa ni historia na nchi hiyo inapiga hatua katika Bara la Afrika katika masuala ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wenyewe tumeonyesha mfano kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani pia Zanzibar tunajua sote kumekuwepo na mgogoro wa kisiasa ambao umedumu kwa takribani miaka 50 kwa malumbano yasiyokwisha lakini palipokuja nia njema na dhamira ya dhati, tumeona mwaka jana kupitia maridhiano ambayo yaliasisiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Amani Karume na Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Self Sharif Hamad, sasa hivi suala hilo linaonekana limebadilisha kabisa mtazamo wa kisiasa Zanzibar. Kwa hiyo, ndio kusema kwamba tukitaka, tunaweza mfano uko humu humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunasema, kuna mambo mengi ambayo yanahitaji kutafutiwa ufumbuzi. Tatizo kubwa lililopo katika suala hili ambalo ninavyoamini mimi linapaswa kuwa ndio kiini cha kutafutiwa ufumbuzi, ni kwamba Muungano wetu tangu ulipoasisiwa, msingi wake haukuwa madhubuti. Kwa nini nasema hivyo? Mkataba wa Muungano, rasimu yake iliandaliwa na mgeni anayeitwa Roland Brown ambaye wakati ule alikuwa ni Mwanasheria Mkuu. Nadhani kwa wakati ule tutakubaliana na Mwanasheria Mkuu ilikuwa ikiitwa Tanganyika. Roland Brown imerekodiwa akisema kwamba aliandaa mkataba ule kwa kutazama mahusiano kati ya Uingereza na Ireland ya Kaskazini. Sasa Ireland ya Kaskazini ilikuwa ni *conquered territory*, Zanzibar haikuwa c*onquered territory* na wala mpaka leo siyo hivyo. Kwa hiyo, nasema ule msingi wenyewe aliokuwa ametujengea, wakati ule tulikuwa wachanga wakati tunapata uhuru, haukuwa mzuri lakini nadhani sasa tumefika mahali tunaweza tukapata ufumbuzi kabisa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Roland Brown aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Tanganyika huru lakini haya mambo ambayo Mheshimiwa Mbunge anazungumza kwamba alitoa maoni, haya maoni hatuna. Kwa hiyo, labda Mheshimiwa Mbunge, angeyaonyesha kusudi tuweze kuelewa alisema nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba radhi sana kuingilia wakati Mheshimiwa Mbunge anazungumza lakini nafikiri ni vizuri kuyaweka mambo haya sawa sawa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa, tutaomba kwa muda wa siku mbili, kama utakuwa na hayo maoni ya huyo Mwanasheria uliyemtaja Roland Brown, utuletee.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutaona uharaka wa kulipata suala hilo kwa sababu sikuja na kila rekodi ambayo ninayo nyumbani ya masuala haya ya Muungano lakini nitajitahidi kuliwasilisha ndani ya siku hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba rafiki yangu kidogo awe mvumilivu ili niweze kutoa maoni yangu.

**NAIBU SPIKA:** Ndio uhuru wa humu ndani, humu ndani ndiyo mtindo wenyewe ndio maana ziko kanuni, endelea tu Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa nilichotaka kusema ni kwamba masuala haya yamekuwa yanatusumbua muda mrefu lakini ninachosema tunahitaji kuona mambo haya yanatafutiwa ufumbuzi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mkataba wa Muungano, kuna mambo ya msingi ambayo yamewekwa mle lakini mengi hivi sasa ukitazama tunavyoendesha nchi, hayapo tena. Mfano mdogo, katika Mkataba wa Muungano, moja katika misingi yake ni suala la Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais. Hili lilifanywa makusudi kabisa ili kuweka msingi wa mahusiano baina ya pande hizi mbili lakini hili sasa halipo. Lakini mambo ya Muungano kwa mfano orodha imekuwa inaongezeka kila siku, sina haja ya kurudia aliyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka kusema kwamba ukweli hakuna ambaye haoni umuhimu wa ushirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Tuna historia ambayo tuna-*share* mambo mengi kabisa lakini hiki kitendo cha kuendelea kukaa katika hali ya kutoaminiana na matatizo ambayo kila siku tunaendelea kuyarejea, kinaendelea kuathiri ile hali ya upendo na moyo mmoja ambao ungepaswa kuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapaswa kujifunza kutoka katika historia za wenzetu. Sisi hatuwezi kuwa na mvutano au uhasama ambao ulikuwepo kwa mfano baina ya Marekani na Uingereza karne mbili zilizopita au uliokuwepo baina ya Marekani na Japan baada ya Marekani kuishambulia Japan lakini leo Marekani, Uingereza na Japan ni washirika wakubwa wa uchumi. Wamesahau yale yaliyopita, yamebakia katika historia, wanatafuta namna gani wanaweza wakanufaika na fursa za kiuchumi kwa pamoja na sisi Zanzibar na Tanzania Bara tunapaswa kutafuta mifano kama hiyo. Tumejaaliwa, tuko katika *a very strategic position* katika eneo hili na tukilitumia vizuri, inaweza kuzinufaisha pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Muungano huu tangu mwanzo ninavyoamini mimi ulikuwa una lengo la kutaka kujenga hali nzuri na kunyanyua maisha ya watu wa nchi zetu mbili ambazo zimeungana. Tutafute njia basi ya kuondokana na haya. Njia inaweza ikapatikana ikiwa tutaweza kuheshimiana. Tukitambua kwamba msingi wa Muungano ni yaliyokuwa madola mawili huru, iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika, zikaunda Muungano huu. Kwa hiyo, tukitambua msingi huo, naamini kwamba tunaweza tukakaa pamoja na tukapata suluhisho la dhati la Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, kumekuwa na hisia mara nyingine kwamba Zanzibar imekuwa inalalamika sana lakini tusisahau kwamba Zanzibar ni mshiriki na mbia sawa katika Muungano huu kama ulivyo upande wa pili wa Muungano. Kwa hiyo, ina haki ya kuona kwamba masuala haya inafaidika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimeandikwa kitabu hichi ambacho kimetoka mwaka huu ambacho kinaitwa *"Kwaheri Ukoloni, Kwaheri Uhuru!"*. Kitabu hiki ni cha zaidi ya kurasa 500 kikielezea mambo mengi sana kuhusu historia ya Muungano na Mapinduzi na chimbuko lake. Lakini pia kimesaidia sana katika kutoa mapendekezo ya ufumbuzi wa

wapi tutapaswa kwenda katika kutatua tatizo hili. Ninawaomba sana viongozi wetu na watunga sheria, wakapata kitabu hiki, wakakisoma ili kwa pamoja tushirikiane ili tutakapokuja katika Bunge lijalo, isiwe tena kila siku tunaendelea kuzungumzia kero za Muungano. Lakini tuone vipi tunaweza kuondoka hapa tulipo tukiwa katika moyo wa ushirikiano na kuwa mfano kweli katika Bara la Afrika kutokana na Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Naomba radhi nilikuwa nimeenda kuwapokea wageni wale ambao ulikuwa umetuagiza tuonane nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa muhtasari kabisa, ninapenda kutumia nafasi hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa uwamuzi wake wa kuunda Mkoa wa Njombe. Ni kitendo ambacho kitasaidia sana kuharakisha maendeleo ya eneo lile kwa sababu ya milima na umbali kutoka Makao Makuu. Kwa taarifa yenu, wananchi wamepokea uamuzi huu kwa furaha, kwa shangwe na tutajaribu kutekeleza wajibu wetu ili kukidhi lengo la Serikali la kuunda Mkoa huu na Wilaya ya Wanging'ombe. Tatu, naomba kutumia nafasi hii, kuwashukuru tena wananchi wa Wilaya ya Njombe na Majimbo yake yale matatu, kwa jinsi ambavyo tunashirikiana kujenga nchi yetu Tanzania kupitia Mkoa ule. Salamu hizi vile vile naziwasilisha kwa sababu Naibu Spika hawezi kusema, kwa hiyo, mimi nasema kwa sababu natoka huko na najua mazingira ya kule. Motisha hii, tunathibitisha kutenda mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, ninapenda kwa muhtasari kusema kwamba nchi inaweza ikaagiza chakula, dawa, bia, magari, nguo kutoka nje, lakini haiwezi kuagiza hali nzuri ya hewa, mazingira, maji ya kilimo kutoka nje. Kwa hiyo, tukiangamiza Tanzania, tumejiangamiza wenyewe kwa sababu hatutaweza kuagiza Tanzania kutoka nje. Kwa hiyo, napendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali kwa makusudi ianze kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu madhara ya ongezeko la joto la jua duniani. Kuna wakati Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Batilda alisema, ifikapo mwaka 2050 au 2060 watu wa miaka 30 wataonekana kama miaka 80, maji hayatakuwepo kutokana na vitendo vya binaadamu vya kujiangamiza wenyewe kwa lengo la kutaka kujihami anajikuta anajiangamiza mwenyewe. Hivi sasa kwa mfano, idadi ya watu duniani imefika karibu bilioni saba na rasilimali zinapungua. Huwezi ukaunda dhahabu, mafuta yanapungua, chakula kinapungua, mvua zinapungua, kukua kwetu wenyewe, ongezeko la kujenga majengo, linatufanya tuwe maskini zaidi. Kwa hiyo, hali ya baadaye itakuaje, ni swali gumu sana kulijibu lakini ni vizuri sana tukaanza kujibu sasa, tusipoziba ufa, tutashindwa kujenga ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, tunapita wakati mgumu sana kwa sababu kuna mabadiliko ya tabia nchi, kuna uhaba wa chakula, kuna uharibifu wa mazingira, tunapata tabu kupata hewa safi, maji katika baadhi ya nchi hivi sasa ni nadra kiasi kwamba wanaanza kuagiza kutoka nchi jirani na sisi tulikuwa na bahati ya kuwa na maziwa, tunasikia hata Ziwa Victoria nalo liko hatarini kukauka. Kule kwetu Njombe ambako hii Mito Rufiji, Kilombero ndio chanzo chake, nako hali ya hewa imebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lugha ya mazingira haizungumzwi na tunaendelea na mambo ya kupanga mipango hapa kama vile mambo yote yatakuwa kama yalivyo, nadhani hili ni kosa. Mambo haya watu wa kawaida hawayajui, ni Waziri wa Mazingira na watu wachache wanaofuatilia redio na matangazo ya dunia, ndio wanajua hali yetu ya baadaye itakuwaje. Kuna vitu unaweza ukaumba, vingine haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati nimesema hapa, barabara zote za Tanzania, barabara kuu kutoka Dar es Salaam mpaka Mbeya pembeni pembeni mle unadhani ni mapambo, ni chupa, makaratasi na uchafu wa kila aina. Watu wakipanda mabasi, wanatupa takataka nje kuchafua nchi yetu ili kuweka usalama ndani ya basi, napendekeza hatua zichukuliwe. Mbona mnaweka hatua za kufyekafyeka nyasi kando kando ya barabara? Hizi takataka kwa nini hamuokoti? Kuwe na mkakati na kampeni ya Kitaifa ya barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Arusha, Dar es Salaam mpaka Lindi, Mtwara, Songea, Mbeya, kuwe na watu wanaookota takataka na elimu ianze kufundishwa nini maana ya takataka, watu hawaelewi, takataka maana yake nini? Takataka ni kitu chochote kisichokuwa mahali pake, ndio takataka. Hata ukileta sufuria hapa ukumbini, ni takataka, hata kama ni safi. Usafi maana yake nini, ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa usalama wa mazingira, hifadhi ya vyanzo vya maji imefuzwa? Kwa nini tusianze kulinda vyanzo vya maji kama tunavyolinda hizi mbuga za Taifa? Vyanzo vya maji vyenyewe hatuweki alama za kudumu kwamba chanzo cha mto huu maana yake hii, weka alama za kudumu na sio kusema maneno tu. Chanzo cha maji ni wapi, tupite nchi nzima, tuweke alama, tuwe tunakagua kila mwaka ili kuokoa nchi hii vinginevyo ndugu zangu tusipojenga safina, nchi hii itakumbwa na gharika sisi ndio wahusika katika uongozi. Ni lazima tuamue maamuzi makali sasa kwa lengo la kuhakikisha kwamba kizazi kijacho kinarithi Tanzania yenye sura ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napendekeza tena, matangazo ya usafi na mazingira yawekwe kwenye mabasi na magari yote, mabasi yote yawe na sehemu ya kuweka takataka ndani ya mabasi yenyewe. Kama ni kutoka Iringa- Njombe pawe na mahali pa kutupa takataka pale Iringa, Mufindi, Morogoro, Chalinze kote huko tukaanze kujenga tabia hii ya usafi, hatuelewi maana ya usafi, ni tabia. Tuanze kujenga tabia hii ndani ya mawazo, vichwa, shuleni na kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nchi nyingine zote mambo ya karatasi za nailoni kweli hayapo, ni sisi tu. Unakuta mtu yuko kwenye daladala, amekunywa maji, anarushia barabarani. Mwingine ana gari zuri kabisa, anakula, anarushia barabarani yaani unashangaa hii gari na mtu mwenyewe havifanani, ni vitu vya ajabu kabisa.

Mheshimiwa Mnyaa atazungumzia mambo ya Muungano, halafu atafuatiwa na Dokta Luka Siyame.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniongezea pointi kwa sababu nilikuwa nizungumzie mambo ya mazingira lakini kwa sasa itabidi niliongelee suala la muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kusema kwamba tunapozungumzia masuala hayo ya Muungano, watu wasipate tafsiri mbaya kwa sababu mtu akikukosoa, amekupenda na mkisimama watu wawili mahali popote halafu ukamfinya mwenzako, yule aliyeumia, ndiye atakayepiga kelele. Kwa maana hiyo, *impact* ya Muungano, sisi Wazanzibari tunaona unatuumiza zaidi ndio maana tunataka mambo yaende vizuri kwa faida ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwamba yeye ni wa kwanza kudumisha Muungano, lakini ofisi yake aliyopo, ni ofisi ya Makamu wa Rais, Mambo ya Muungano na Mheshimiwa Spika hapa aliwahi kutuambia kwamba nafasi ile ya Makamu wa Rais, ni moja, iko pale, iliyotolewa kule, mnakumbuka, sasa yeye pale ndio kwa maslahi ya Zanzibar na mambo ya Muungano. Sasa bahati mbaya nasikitika, Waziri wa Mazingira yuko katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo haihusiki na mambo ya Muungano, sasa hayo ndio baadhi ya michanganyiko ya haya mambo, iko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameshazungumzwa na kwa kweli niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Riziki, kuhusu mambo ya Muungano ambayo imemeliza kiasi kwamba sijui hata la kusema lakini labda niongeze kitu kimoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, anayehusika na mambo ya Muungano, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, nafikiri ana wajibu mkubwa. Kwanza, ana uzoefu mkubwa, yupo katika Bunge miaka mingi, ameshughulikia mambo ya Muungano na amefanya kazi pande zote za Jamuhuri. Kwa hiyo, anajua fika kwamba yako masuala mengi ya Muungano hayatekelezeki na yeye ofisi yake ndio ina wajibu wa kurekebisha. Anajua fika katika mambo ya Muungano tangia mwaka 1964 kabla ya hiyo nyongeza lakini hayajatekelezeka kimuungano mpaka hivi leo, mfano Bandari. Bandari ni suala la Muungano lakini upande wa Tanzania Bara inajiendesha kama upande huu na upande wa Zanzibar inajiendesha kivyake, halijaenda kimuungano hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavyozungumzia hapa hizi kasoro, ofisi yako inafaa izishughulikie na haya yote yanaweza yakapatiwa ufumbuzi ikiwa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ambao sio msahafu, imefika *stage* sasa ifanyiwe mabadiliko. Kuna matatizo ambayo hayawezi kutatuka kama Katiba ya Jamuhuri ya Muungano haijafanyiwa mabadiliko. Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, inahusika kikamilifu itakapofanyiwa marekebisho Katiba ya Jamuhuri ya Muungano sasa ni wakati muafaka baada ya miaka 46 ikajumuisha hayo matatizo yote ambayo leo tunayaita kero za Muungano kumbe ni matatizo ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nikutolee mfano wa hapa hapa. Ndani ya Bunge hili, kuna Wabunge wa kuchaguliwa Majimboni, ndani ya Bunge hili kuna Wabunge Viti Maalum, ndani ya Bunge hili kuna Wabuge wa Kuteuliwa na Rais, lakini mtu hawezi kuwa Waziri Mkuu kwa kuwa Mbunge, lazima awe Mbunge wa kuchaguliwa Jimboni, kwa mujibu wa Katiba. Sasa ina maana ndani ya Bunge hili, kwa Katiba iliyopo tuna *class* tofauti na ndio maana hata *CDCF* wakapewa Wabunge wa baadhi ya Majimbo tu, Wabunge wengine hawakupewa. Tukitizama, kuna tatizo la Katiba. Anaweza kuchaguliwa mtu kuwa Waziri Mkuu ikiwa ni Mbunge tu wa kuchaguliwa? Ni kutoka kwa Mbunge anayetokana na Jimbo. Mtu hachaguliwi kuwa Waziri Mkuu kupitia Viti Maalum, hachaguliwi aliyeteuliwa na Rais, hili ni tatizo. Kwa hiyo, imefika wakati wa kubadilisha hata hii Katiba, ndio tutapata ufumbuzi wa matatizo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi hii ya *MANSEP*, *PADEP* na *TASAF*, kwa kweli ni miradi inayotusaidia sana Watanzania, lakini utekelezaji wake unatofautiana katika pande mbili za Jamuhuri ya Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara mpaka sasa hivi Mbunge ni Diwani kwa hivyo anapata taarifa zote za Halmashauri kama kawaida lakini kwa upande wa Tanzania Visiwani haipo hiyo. Kwa hiyo, kuna mambo yanatekelezwa huko, Mbunge hajui lolote, hajui mwanzo wala mwisho. Hii ni kasoro na ofisi ya Mheshimiwa Waziri inabidi iratibu masuala haya vizuri. Kwa hivyo, miradi hii ya *MANSEP*, *PADEP* na *TASAF* mpaka sasa hivi utekelezaji wake kwa upande wa Visiwani, Mbunge anakuwa hana habari na mambo yanayofanyika ndani ya Jimbo lake na ule utaratibu wote unakuwa una matatizo kwa kiasi fulani. Kwa maana hiyo, kama Mbunge aliyechaguliwa na wananchi hana taarifa ya mambo yanayotendeka ndani ya Jimbo lake, hilo ni kosa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri katika miaka ijayo pamoja na kwamba *PADEP* ndio mwisho, mwezi wa Juni ndio mwisho lakini iko haja kwa vitu hivi kufikiriwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa *MANSEP*, upande wa Zanzibar ilipata shilingi bilioni 26 na upande wa Tanzania Bara ikapata shilingi bilioni 50 na kitu. Katika mradi wa *PADEP*, Zanzibar ilipata shilingi bilioni sita na upande wa Tanzania Bara ilipata shilingi bilioni 64. Sasa mimi namtaka Mheshimiwa Waziri baadaye atufafanulie, kwa nini katika *PADEP* tuna asilimia 8.5 na kwa nini katika *MANSEP* tukapata asilimia 39.4. Huu mgawanyo umekuwakuaje? Kwa hivyo, tunajikuta katika miradi ya *PADEP* kidogo mambo yamerudi nyuma lakini katika miradi hii ya *MANSEP*, hoja hapa sio

katika kuhifadhi fukwe na kupanda mikandaa tu,mazingira yanachafuka pamoja na umaskini uliopo kwa maana hiyo miradi ya kukata miti, miradi ya makaa katika nchi hasa Visiwani, miradi mikubwa kama hii inapokuja, ni kuimarisha uvuvi wa kileo, ndio watu utawatoa katika njia nyingine ya kutokuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kwa upande wa Jamhuri nzima ya Tanzania, tunakabiliwa kama hotuba ya *Shadow Minister* wa Mambo ya Mazingira alivyozungumza, kuna ukataji miti wa kiasi cha juu, nishati kubwa inayohitajika hapa ni mkaa, yaani kuni kwa walio wengi. Lakini Wizara hii ya Mazingira haina uhusiano hata kidogo na Nishati na Madini wakati Tanzania leo tuna gesi ya kutosha, wakati Tanzania bado miundombinu ya kuisambaza gesi hiyo haijapatikana, kuna sababu gani ya Wizara hii ya Mazingira isishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini ili gesi hii ikapatikana kwa Watanzania walio wengi? Hapo una-*impose indirectly* kwamba kuni hazitakatwa, mazingira hayataharibika, ni kitu pekee cha kufanya ambacho Wizara hii ni lazima ishirikiane, isibebeshwe Wizara ya Nishati na Madini pekee yake au ikabebeshwa *TPDC* suala la kusambaza gesi, hili ni suala ambalo Wizara hii ya Mazingira ikitaka misitu ipone, ikitaka watu wapunguze matumizi ya mkaa basi ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu kusababisha gesi hii itumike nyumbani, ndio chanzo kikubwa cha nishati, baraka aliyotujalia Mwenyezi Mungu na mazingira yatapona, tafadhali katika Bunge lijalo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kushiriki katika kujadili hoja hii. Awali ya yote, naomba niseme, naunga mkono hoja na baada ya hapo nijikite katika sehemu mbili za mjadala huu. Mosi ni pongezi, napenda kwa niaba ya wananchi wa Mbozi Magharibi, nichukue fursa hii kipekee kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuweza kututunuku Wilaya mpya ya Momba yenye tarafa nne za Kamsamba, Msangano, Ndalambo na Tunduma.

**NAIBU SPIKA:** Ambako ndio Jimbo lako?

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndio lililokuwa Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba pia kipekee kabisa, nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa umahiri wake kwa kushughulikia masuala ya Muungano na masuala ya mazingira Kitaifa na Kimataifa kwa kiwango cha kutukuka. Napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, kwa kweli, kwa uimara wake katika

kushughulikia mambo ya Muungano na hasa hasa kwa kudhihirisha jinsi ambavyo anajadili na kujibu maswali mbalimbali katika Bunge hili ambayo yanahusu Muungano, ambayo yamekuwa yakiulizwa kwa nyakati mbalimbali. Napenda pia kipekee kabisa nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mazingira, Dokta Batilda Buriani ambaye naye niseme kwa hakika katika mambo ya mazingira amejikita katika kuhakikisha uharibifu wa mazingira unaosababishwa na viwanda ambavyo vinajengwa kiholela na hivyo kutofuata sheria na taratibu na kutishia usalama vinafungiwa na pia kwa ujumla katika kuhakikisha mazingira mbalimbali ambayo yameharibika yanarejeshwa katika hali safi.

Ninaamini kabisa haya yote yamewezekana kwa sababu ya utendaji mahiri wa Makatibu Wakuu katika hizo Ofisi mbili za Rais pamoja na Watendaji wote na Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Baada ya kusema hivyo, naomba sasa niingie sehemu ya pili ambayo inasema ni tatizo nalo ni moja tu, nalielekeza kwenye suala la mazingira na hili linahusu Wilaya yangu ya Mbozi. Kuna msitu ama hifadhi ya msitu ijulikanayo kama hifadhi ya akiba ya msitu wa Isalalo ambayo ilianzishwa zaidi ya miaka 50 iliyopita na wakati ule ikapewa jina la *Lady Chatterly's Forest Reserve.* Hifadhi hii iko katika Kata 10 kati ya Kata 30 za Wilaya ya Mbozi. Lakini linalotokea hasa hasa kuanzia msimu wa mvua wa mwaka 2008/2009 hadi hivi sasa ni ukataji holela wa zaidi ya hekta 300 za msitu huu ambao badala yake imepandwa miche ya kahawa pamoja na kwamba taarifa hii mimi binafsi nimekwishaitoa Wilayani kwa maana ya Halmashauri na kwa DC na kujadiliwa hata kwenye Baraza la Madiwani na hata Mkuu wa Wilaya kutoa amri kwamba hawa watu wasimishe ukataji huo na ulimaji huo na hata mimi binafsi kutoa hoja hii kwenye Warsha ama Kongamano la Taifa kuhusu mabadiliko ya tabia nchi mwaka jana. Lakini hadi leo hakuna kitu kilichofanywa.

Sasa kwa kuona hivyo, limeibuka kundi lingine la watu ambao wameanza kukata kiholela na kuvuna mbao za miti ya mninga na mininga miji. Nasikia kwa hivi sasa wakati tuko huku hata ile miti ya miombo nayo baada ya watu hao kupata misumeno ya umeme wameanza kuikata na kupasua mbao. Hivyo basi, ninaomba kwa sababu shughuli hii inafanyika wazi wazi kwenye barabara ya Igamba –Msangano - Utambalila na shughuli hii inafanyika usiku ambapo utaona miali mingi ya moto na taa na misururu ya magari ambayo yanasomba mbao hizi, cha kushangaza kabisa sehemu hizo zina vizuizi vya maliasili, lakini hakuna hata lori moja tunaloona linakamatwa na tunaambiwa kwamba shughuli hii ni mradi wa wakubwa.

Ninaomba, kwa sababu mwaka jana wakati wa Bunge la Bajeti niliongea juu ya suala hili, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kwa kutumia mamlaka aliyopewa awaagize Watendaji wake wafuatilie hilo suala kwa sababu msitu huu ni wa kipekee kabisa, bioanuwai yake ni ya kipekee Mkoani Mbeya na hata ile *ecosystem* yake ni ya kipekee kabisa, nina hakika kama ingekuwa imefanyiwa utafiti maalum ingeweza hata kutangazwa kwamba ni ya kipee kiduniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ndiyo chanzo kikubwa cha maji yaendayo Ziwa Rukwa. Pamoja na kwamba kuna mradi wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia

hifadhi ya kurejesha mazingira ya zamani ya Ziwa Rukwa katika eneo hili, lakini hatuoni hatua inayochukuliwa ili kurudisha mazingira ya hili eneo kama yalivyokuwa miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema, naunga mkono hoja, ila naomba msitu wetu huu uokolewe.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo kuhusu mambo ya hotuba hizi zote mbili ambazo zimepita. Kwanza nimpongeze Waziri wa Nchi, ambaye anashughulikia Muungano na anayeshughulikia mazingira, wote wawili, kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa kweli zimetupanua na kutupatia mwanga wa namna tunavyokwenda. Lakini nilikuwa naomba nijikite zaidi katika mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira kwa kweli ni somo ambalo najua ni kubwa na ni pana, lakini nilikuwa naomba nizungumzie zaidi kwenye sehemu hii ya kutupa takataka. Nikisafiri mara nyingi katika mabasi kutoka Mbeya mpaka Dar es Salaam au mpaka hapa, kwa kweli kila nikiangalia mazingira ya maeneo ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu. Yamejaa makaratasi kila mahali na kila mahali unashangaa kwamba haya makaratasi mwisho wake yatakwenda wapi? Lakini kuna mfano mmoja wa basi moja la Sumry ambao wao unapopanda tu basi wanaanza kukueleza jinsi ya kuzitunza takataka. *(Makofi)*

Basi hili ni kama kwenye ndege unakaa pale unaelekezwa kwamba takataka zote zitatupwa hapa na unapewa *dustbin* mahali ambapo utatupa takataka zako zote. Lakini mabasi mengine mfumo huo haupo. Kila mtu anatupa ovyo na kibaya zaidi mpaka kwenye mbuga za wanyama zimejaa takataka mfano wake haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali labda sheria za kutunza mazingira zimekuwepo lakini hazitekelezwi ipasavyo. Nilikuwa naomba Serikali kama inawezekana sheria hizi zitilie mkazo ili ziwe na nguvu zaidi. Nakumbuka siku moja mimi nilikuwa Uswisi kwenye gari la jamaa amenichukua, nimekula ndizi pale nikatupa ganda. Nilipotupa lile ganda mimi nakwenda sina habari, yule dreva hajui kama mimi nimetupa ganda pale, limeendeshwa gari ametufuata mpaka tulipofika na yeye amesimama pale. Mwisho, anarudisha lile ganda kwetu, bwana umelitupa hili ganda pale. Mpaka leo naona aibu sana kuweza kutupa takataka ovyo ovyo, kwa sababu nafikiri nitakamatwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kama sheria zingekuwa na nguvu zingesaidia sana hali ya mazingira. Lakini kwa sababu sheria zimekuwa finyu, sio ajabu unamkuta mtu anatembea mjini anatupa tu karatasi, kwa sababu haogopi, hakuna kitu kinamshitaki. Nilikuwa naiomba Serikali kutilia mkazo kuhusu sheria hizi, kwa sababu tunakoelekea huko mbele ni kubaya. Kibaya, mtu amepanda kwenye basi, anatapika, anaweka matapishi yake kwenye karatasi au mtu anapenga makamasi anaweka kwenye karatasi halafu anatupa nje, hujui ni nani atakayeokota.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni aibu kubwa sana. Nilikuwa naiomba Serikali ingejitahidi kuweka sheria ziwe na nguvu zaidi. Kuna mfano mmoja, ni juzi juzi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kupitia Halmashauri ya Jiji la Mbeya waliweka sheria wakajaribu ku-*implement* ile sheria ndogo kwamba mtu yeyote lazima ahakikishe kwamba ana mahali ambapo atatunza takataka zake pale nyumbani. Nakwambia kila mahali na kila mtu alikuwa anajaribu kufanya usafi. Kumbe ni kukumbushwa tu. Unajua ni kama sadaka. Sadaka sio kwamba mtu hapendi kutoa, lakini usipomkumbusha hatoi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali hasa Wizara ambayo inashughulikia kwamba tukumbushwe wananchi, tukumbushwe kuhusu kutunza mazingira. Tusipokumbushwa nchi yetu itaharibika na tutaelekea kubaya sana. Yaani makaratasi yaliyojaa humo njiani nashangaa! Hivi hii ndiyo nchi ambayo watu wanaishi! Hiyo ni dhambi kubwa sana. Maana tusiwe tunahubiri mambo mengine tu, lakini haya madogo tunaacha. Kwa nini tusiweze kuyatekeleza? Nilikuwa naiomba Serikali ichukulie maanani iwe *concern* sana na mambo haya, kwa sababu kwa kweli hatujui ni watu wangapi wanaathirika kwa ajili ya kuokota hayo makaratasi? Wanyama wangapi wanaathirika? Kwa hiyo, nilikuwa naomba tujaribu kuweka mkazo ili Sheria hii ya Mazingira ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ilikuwa ni kuhusu upandaji wa miti. Nimeona hapa kwenye hotuba kwamba kuna mipango mingi sana ya upandaji wa miti. Kila Wilaya imeeleza kwamba itapanda miti. Hii ni mipango tu ya kiwalaya. Mimi mwenyewe hapa pamoja na kwamba Wilayani kwangu upo mpango huo, lakini ni watu wachache sana wanajua kwamba kuna kampeni ya kupanda miti. *(Makofi)*

Lakini kumbe kama tungeanza kwenye kaya watu waelezwe, tunakwenda katika kaya kwenye misiba, unashangaa kuona hata mahali pa kujificha jua msibani mnashindwa. Mwenye nyumba anashindwa kupanda mti nyumbani kwake. Kwa nini tusianzie kutoa elimu hii kuanzia kwenye kaya na kuwe na sheria zenye nguvu na uwezekano huo upo? Wala siyo kwamba tunaweza kushindwa, upo kabisa! Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali kwamba tujitihidi kuhakikisha kwamba hii kampeni ya kupanda miti iwe ni kampeni ambayo inashuka chini mpaka kwenye kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba kuna zawadi zitatolewa kwa ajili ya wale ambao wamepanda miti. Lakini ni elimu ndogo sana ambayo imetolewa kwa hapo, iko kwenye makaratasi. Makaratasi watu siku hizi wameshachoka nayo maana yamekuwa mengi mno. Wanataka kuelezwa, kwa sababu kila mahali yamebandikwa makaratasi. Wamechoka! Bahati nzuri *system* ya Serikali yetu kiutawala ni nzuri. Kuna mabalozi, kuna wenyeviti wa Vitongoji, kama wangeeleza wakafundishwa mambo haya wangeweza kuyafanyia kazi vizuri sana na mwisho hatimaye tungeona kwamba mazingira yetu yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi ndogo sana zinatushinda. Nilikuwa Namibia, nimeshangaa jinsi walivyoweza kuutunza mji wao mzuri kabisa na nchi yao ilivyokuwa nzuri. Wala hawatupi hata takataka hovyo, kwa sababu wewe mwenyewe unaogopa. Hili suala ni mtu mwenyewe anajifunza. Lakini kwa kupewa elimu na elimu

hiyo inawezekana kutolewa kwa watu wetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hata ukiangalia kwa mfano kule kwangu Mbeya Vijijini unakuta uharibifu wa mazingira. Ile sehemu yote ambayo ilikuwa inatiririsha maji zamani, siku hizi karibu mito mingi sana imekauka kwa sababu mazingira hayajatiliwa maanani. Kwa sababu misitu yote imefyekwa, nafikiri baada ya miaka michache maji yatakuwa hamna. Tutafanya nini? Nilikuwa naiomba Serikali ingejitahidi kufufua zile sheria ambazo zipo tayari lakini hazifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano tu wa hiyo ambayo nimesema ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuamrisha kwamba watu wote waweke miji iwe safi na kwa kweli hata mimi nilipokwenda pale nyumbani kwangu nikakuta watoto wangu wamefyeka, nikajua kuwa sheria hii wakati mwingine zitiliwe mkazo zaidi. Kwa hiyo, tutengeneze miji yetu iwe safi. Miti ipandwe kwa uhakika na miti ianzie kwenye kaya na hatimaye iende mpaka huko juu. Naomba kuunga hoja kabisa kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuzungumzia kidogo suala lile lile la Muungano, kwa sababu Muungano kama tunavyojua ni mwiba katika nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na ukurasa wa 18. Ukurasa huu unazungumzia suala la kuelimisha umma kuhusu Muungano. Nina wasiwasi kidogo katika suala hili kwamba kweli watu wanaelimishwa kuhusu Muungano? Kwa sababu hata ukitazama takwimu hapa, kuna fulana 300 zilizogawiwa, *covers* 500. Sasa 300 *out of forty million people!* Tanzania sijui kama kuna elimu hasa ya Muungano. Hilo ni moja. Lakini la pili ni kwamba, hawa waelimishaji ni nani ? Kwa sababu sifikirii kama Wanzanzibar wameshirikishwa katika suala hili la kuelimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitatoa mfano mmoja. Nilipomaliza kikao cha Bunge kilichopita, sisi Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria tumepata bahati ya kwenda Morogoro katika semina ya Maadili ya Umma. Pale tulielimishwa sana pamoja na mambo ya Muungano. Lakini muelimishaji mmoja, yaani Mtoa Mada alikuwa ni Profesa Kabudi. Profesa Kabudi tulizungumza naye, sasa wakati tunamwuliza kuhusu *Articles of Union* namna zinavyoheshimiwa, yeye akadiriki kusema kwamba kwa sababu tuna Katiba ya Tanzania, kwa hiyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza na *Articles of Union* ni *subordinate.* Kitu ambacho haiwezekani hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa mwelimishaji mwenyewe ni huyu anayepotosha, mimi nina wasiwasi kwamba *paragraph* hii yote haina maana. Haiwezekani kwamba *Articles of Union* ni *subordina*te kuliko Katiba ya Muungano au Katiba nyingine. Ninavyojua mimi, *Articles of Union* ni *Treaty* baina ya *two equally sovereign partiners.* Sasa ikiwa ni *treaty,* huwezi ukaichezeachezea tu. Sasa anapokuja mtaalam akasema kwamba ni *subordinate,* sio kweli na uelimishaji wa aina hii kwa kweli utapotosha na unapotosha jamii ya Watanzania. Kwa hiyo, ombi langu kwanza Wanzanzibar washirikishwe katika kuelimisha masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili ni kwamba kuna hili suala la mafuta na gesi ambalo lilizungumzwa katika ukurasa wa 15. Hapa nasema kwamba masuala mengine yanaendelea kushughulikiwa ni namna ya kugawana gharama za faida ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.  Sasa hapa najiuliza, hawa Marais wakisema tunawasikiliza au hatuwasikilizi, kwa sababu mimi nilikuweko katika Uwanja Gombani katika Sherehe za Mapinduzi na Mheshemiwa Rais wa Zanzabar alikuweko. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alikuwepo na katika suala hili Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alisema kwamba suala la mafuta limeshapatiwa ufumbuzi kwamba sasa linatoka katika orodha ya Muungno na Rais alikuwepo pale.  Halafu juzi katika Baraza la Wawakilishi, Waziri Kiongozi wa Zanzibar alisema kwamba suala hili kwa sababu ilikuwa ni agizo la Rais ameshapelekewa Waziri Mkuu kwa hatua.

Mimi nilikuwa nafikiria kwamba hatua zenyewe zitakuwa ni suala la kuleta Bungeni, likatolewa suala hilo.  Sio suala la kugawa tena fedha, hamna suala la kugawa fedha.  Mimi naomba nielezwe hili suala lililozungumzwa na Marais: Je, ni kweli au suala lililomo ndani ya kitabu ndiyo kweli? Kwa sababu Muungano siyo suala tu la kuongeza kila kitu katika orodha ya Muungano. Lakini ili kuimarisha Muungano, hata ukitoa kitu ambacho kinaleta matatizo nayo ni kuimarisha Muungano.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naomba pia tuelezewe.  Suala lingine ni suala la mfuko wa pamoja wa fedha.  Suala hili limekuwa likizungumzwa siku nyingi sana. Miaka inafika hata 20 imo katika Katiba.  Sasa kweli mpaka leo hii Kamati ya pamoja miaka 20 haiwezi kulitatua suala hili mpaka lini au tusubiri tena miaka mingine 30 au 40? Itakuwa kweli hiyo ni kuimarisha Muungano au kuudhoofisha Muungano.  Kwa sababu kitu kama hiki ni kitu ambacho kinaleta matatizo. Sasa mimi nafikiri hawa wanaohusika ni wazi wayatazame mambo kama haya. Huwezi kuzungumzia suala la mfuko wa pamoja wa kugawa asilimia 4.5 kwa miaka 20 halijapatiwa ufumbuzi.  Hawa watendaji wanafaa au hawafai, ikiwa *twenty years* hujafanya chochote !

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la mikopo. Suala la mikopo katika ukurasa 17 na 18 pia limeelezewa hapa.  Wanasema kwamba SMZ inaweza ikakopa kwa mikopo ya ndani.  Lakini mikopo ya nje lazima SMT ishirikishwe. Mimi najiuliza, kweli hapa napo tunaimarisha Muungano?  Maana kuna mambo ya SMZ ambayo siyo ya Muungano. Wizara ya Kilimo kwa mfano, hivi kweli kama tunataka kukopa mbolea Korea, tunataka kukopa mbegu ya mpunga Uchina ndiyo mpaka Serikali ya SMT ikubali, maana yake kushirikishwa na sisi tukubali.  Sasa jamani tunakwenda wapi?   Mimi nafikiri kuna mambo ambayo siyo ya Muungano, SMZ haihusiani kabisa na kushirikishwa  na SMT.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakubali kwa upande mmoja kama mtasema kwamba *BoT* kwa sababu kile ndiyo chombo kikubwa cha fedha, wale wanaweza wakatoa *guarantee* kwa SMZ.  Lakini SMT, Waziri wa Fedha wa Muungano ashirikishwe namna gani?  Mimi nafikiri haya ni mambo ambayo lazima tuyatazame ili sote pande mbili Zanzibar na Tanzania Bara tujue kwamba huu ni Muungano ambao unatufaa sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba hii *CDF* ya jimbo, niseme kwamba kuna shilingi bilioni mbili na hii inashughulikiwa na Wizara ya Makamu wa Rais. Lakini kwa Zanzibar, fedha hizi zimepelekwa Wizara ya Fedha. Sasa mimi nataka nijue, *Accounting Officer* atakuwa nani ? Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi lini Serikali itasafisha mazingira ya mji kama Jiji la Dar es Salaam. Jiji kama hili kuwa chafu ni aibu ya nchi nzima ili kupunguza kipindupindu na ndio mji unaoongoza kwa magonjwa. Mitaro sehemu ya jangwani mvua ikinyesha wanafungulia vyoo vyao na mji mzima kutoa harufu. Maziwa pamoja na bahari kuna magugu maji ambayo ni uchafu mkubwa hasa kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008 – 2009 nilichangia kuhusu uchafuzi wa mazingira ya meli kumwaga uchafu karibu na bandari na mpaka sasa wanamwaga pale pale. Masoko kwa mfano hasa ya Dar es Salaam na hata feri inatoa harufu, na Ikulu panakosa heshima kwa ajili ya harufu hiyo. Je, Serikali inasemaje? Ina mikakati gani kupunguza matatizo hayo? Matatizo ya wasafiri pamoja na mabasi yanayotoa vinywaji na vyakula kwenye gari wanatupa uchafu hovyo: Je, kwa nini isitungwe sheria kila basi wakawa wana kifaa cha kutupa uchafu huo kwenye basi humo kuliko kuambiwa tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini pasiwekwe matangazo kwenye magari yote kwamba atakayekiuka anachukuliwa hatua au kufungiwa leseni? Ukataji miti uchomaji mikaa pamoja na kuchoma moto hovyo imekuwa kero: Je, Serikali bila kuwatungia sheria, maneno tu yataweza kusaidia? Haiwezekani! Watu wanakuwa wabishi, madhara yanawapata wasiokuwa na hatia, mito inakauka, wananchi wanakosa maji, walio wachache wanawaharibia walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanaochimba mashimo ya changarawe hasa kutengeneza barabara, wakimaliza, hakuna anayefunika mashimo, wanaacha mmomonyoko, wenyewe wanalipwa wanaondoka. Ukiangalia waliotengeneza barabara ya Mtukula Kagoma pamoja na ujenzi unaoendelea wamechimba hovyo hovyo, matokeo yake watu wanafunikwa na mmomonyoko wanakufa. Ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimba madini hao sasa ndio wamezidi, wanachimba eti wanafanya utafiti, wanawaacha wakiendelea kila shimo wanaliacha hivyo hivyo wananchi wetu wanaingia kujua watatoa chochote, umasikini, wanafunikwa na kufa, wengine hawajulikani. Nashauri Serikali iwe inatenga bajeti kubwa kwenye Wizara hii. Nimekwenda sehemu nyingi za wachimbaji, nimekuta wanajisaidia hovyo hovyo, hawana vyoo, ndio maana wanaugua hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna wawekezaji wanamwaga sumu kwenye mito ya wananchi wanakochota maji na kusababisha madhara makubwa. Nimeona mimi

mwenyewe, Geita wana mabaka wanakuwa na muvi, upele mwili mzima! Wana matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Ali Mohamed Shein - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake uliotukuka katika kushughulikia masuala ya Muungano wa Tanzania na Mazingira katika ngazi ya Taifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze pia pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mohamed Khatibu kwa uimara wake katika kushughulikia masuala ya Muungano, kama alivyodhihirisha katika kujibu maswali tete ambayo yamekuwa yakiulizwa Bungeni kwa nyakati mbalimbali. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Batilda Buriani kwa juhudi kubwa katika kuhakikisha masuala ya uharibifu wa mazingira yanayoshughulikiwa ipasavyo nchini hususan viwanda visivyozingatia sheria na kanuni za utunzaji mazingira yao na urejeshaji wa mazingira pale ambapo uharibifu umekwishatokea sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki hata kidogo kama sitatoa pongezi zangu za dhati kwa Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Masuala ya Muungano na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa kazi kubwa wanayoifanya ili hakikisha yote yamekuwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee suala nililolitolea malalamiko kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ya mwaka 2009/2010 kuhusu ukataji holela wa zaidi ya hekta 300 za miti, hifadhi ya msitu wa akiba wa Isalalo *(Isalalo Forest Reserve)* iliyoko Wilayani Mbozi katika Kata za Isandula, Chiwezi, Msia, Msangano, Itaka, Chitete, Chukulumo, Nambinzo, na Ivuna. Eneo husika likiwa lile lililopo Kata ya Msia, Kijiji cha Isalalo ambako msitu huo umekatiwa kwa makusudi na kupandwa kahawa msimu wa mvua wa mwaka 2009/2010.

Kibaya zaidi ni kwamba pamoja na taarifa hii kufikishwa Wilayani na kujadiliwa kwenye vikao vya Baraza la Madiwani na agizo la kusimamisha shughuli ni kutokana na *DC* na pia kufikishwa kwenye warsha ya Taifa ya Mazingira mbali na Bunge lako Tukufu, bado hakuna hatua iliyochukuliwa na kilimo kinazidi kuendelea ndani ya msitu huo ambao ni wa kihistoria, kwani ulifanywa hifadhi miaka ya 50 na wakoloni wa Kiingereza na kupewa jina la *Lady Chatterly's Forest Reserve*. Msitu huu ndio unatengeneza ukingo wa kaskazini wa Bonde la Ufa la Rukwa ambayo ni sehemu ya Bonde la Ufa la Magharibi na ni hifadhi yenye bioanuwai na *eco-system* ya kipekee kabisa Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamoja na kwamba eneo hili ni sehemu ya vyanzo vikubwa vya maji yaendayo ardhi oevu ya Ziwa Rukwa kwa upande wa Mashariki, uharibifu unaoendelea ndani yake hauelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara na Taasisi zake ichukue hatua za haraka kwani hivi sasa kuna uharibifu mkubwa zaidi unaoendelea wa upasuaji mbao kiholela kutokana na miti ya mninga na mninga maji, nasikia sasa hivi hata kutoka kwenye miombo. Ukataji na usombaji wa mbao hizi hufanywa usiku. Naomba watumishi wa Ofisi ya Rais – Mazingira na wale wa Wizara ya Maliasili na Utalii wapite barabara ya Igamba – Msangano – Utambalila wakati wa usiku ili washuhudie miale ya moto, taa na misururu ya magari yaliyoegeshwa na kusafirisha mbao zinazovunwa na kusafirishwa isivyo halali. Japo karibu na kuingia barabara kuu ya kaskazini *(Great North road)* kuna vizuizi vya Wizara ya Maliasili, lakini hatuoni mbao zozote zinazokamatwa. Inasemekana ni miradi ya wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nazitoa kwa niaba ya wapigakura wote wa Jimbo la Kwimba kwa ushirikiano wa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi chote cha miaka mitano tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani. Shukrani za dhati tunazitoa kutokana na mafanikio tuliyoyapata kutokana na miradi ya *TASAF* katika Wilaya na Jimbo la Kwimba. Kwa bahati nzuri, Wilaya ya Kwimba imekuwa ikifadhiliwa kupitia mradi wa *TASAF* katika awamu zote mbili.

Kutokana na hilo, tunaishukuru sana Serikali kwa kutupatia fursa ya kujipatia uzoefu wa kuibua miradi kutoka chini na jinsi ya kuisimamia. Miradi hii imewapatia wananchi fursa ya kutambua na kumiliki miradi yao. Tunashukuru sana. Tuombacho kupitia Wizara hii na Waziri husika, tunaomba sana viporo vya miradi ya *TASAF* kama barabara ya Chibuji – Bupamwa na ule wa zahanati ya Shilembo jimboni Kwimba ipatiwe fedha mapema na kukamilishwa mapema ili ikabidhiwe Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na *TASAF*, Wilaya ya Kwimba pia ni wadau wa Hifadhi ya Mazingira kutokana na ukame uliokidhiri, mvua zisizotosha na uchungaji usio na mpangilio maalum. Jumla ya hali hiyo inasababisha mazingira yanayoashiria tishio la Wilaya kugeuka kuwa jangwa. Maika ya 80 – 90 kulikuwa na mradi wa *KRP (Kwimba Reafforestration Project)* uliojulikana kwa jina la Mfadhili wa Australia, Brian.

Mradi huu ulihamishiwa Magu katikati ya miaka ya 90 kutokana na watendaji wa mradi huo kutokukubalika sana na uongozi wa Halmashauri ya Kwimba. Sababu hazikuwa za msingi sana ila alikosekana msuluhishi mwenye utashi kwa muda muafaka. Matokeo ya mradi huo ni miti ya mikaratusi mingi na miarubaini mtu aionavyo mara aingiapo Kwimba. Kwa bahati mbaya sana mwendelezo wa mradi huo unazidi kupungua mwaka hadi mwaka. Ombi langu ni kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais ijipange upya, tena kwa nguvu zaidi ili kuja kuendeleza pale mradi huo ulipoishia ili kuinusuru Wilaya hiyo kuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miti muafaka kwa Wilaya hiyo ibainishwe na kupangwa kwa kupandwa vyema. Juhudi hizi zitaokoa uzoefu uliopatikana na ari ya miche ya watu ambao bado wapo wakiendeleza miradi ya miche ya miti kutopotea.

Ombi la pili, nishati mbadala kwa matumizi ya kuni nyingi na mamilioni ya magunia ya mkaa isambazwe mapema hasa katika shule zetu za sekondari, zahanati na hospitalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kukubali kuweka mitambo ya *(biogas)* katika shule tatu za Mwamashimba, Nyamilama na Ngudu katika Jimbo la Kwimba. Mitambo hiyo itasaidia kupunguza malundo ya kuni katika shule hizo na kuwezesha matumizi ya gesi hiyo katika maabara za shule hizo. Ombi langu ni kuwa, miradi hiyo ikifanikiwa iweze kusambazwa kwenye vituo vingine jimboni humo kwa vituo vitumiavyo kuni kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kuchukua fursa hii kuishukuru na kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuendeleza kushughulikia vyema kero mbalimbali za Muungano wetu. Pamoja na kukuru kakara za demokrasia ya vyama vingi, umoja na kuaminiana kati ya wananchi wote wa pande zetu mbili za Muungano vinazidi kuimarika. Ni imani yangu kuwa kero zilizobakia zitaambatana na matokeo ya maendeleo, vitaendelea kushughulikiwa kila muda muafaka utakapokuwa unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ninampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa uadilifu wake mkubwa. Makamu wa Rais ni mtu rahimu sana, hana mgogoro na mtu. Nampongeza sana. Tuige mfano kwake. Nawapongeza sana viongozi na watumishi wake wote waliomo katika Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta kuondolewa kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Siku za hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi imekuwa ikizungumza sana namna ya kuliondoa suala la mafuta kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Zanzibar ni nchi. Hata hivyo, kuanza kuzungumza na kutaka kuliondoa suala la mafuta kwenye orodha ya mambo ya Muungano naona itakuwa kwenda kinyume cha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hofu yangu hapa tutaanza kutengeneza ufa mkubwa sana kwenye Muungano ambao unapigiwa mfano mzuri barani Afrika. Nimesikia kwamba tayari Mheshimiwa Waziri Kiongozi ameshamwandikia Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda kuhusu azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutaka kuliondoa suala la mafuta kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kila upande wa Muungano ukitaka kuondoa mambo muhimu kwenye orodha ya Muungano: Je, Muungano utabaki? Je, huo sio ndio utakuwa mwanzo wa kuvunjika kwa Muungano? Je, kwa Zanzibar kutaka kuliondoa

suala la mafuta kwenye orodha ya mambo ya Muungano si ina maana twende kwenye mchakato wa kubadilisha Katiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kama Zanzibar itafanikiwa katika jambo hili, kesho watakuja na lingine kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kujenga majengo kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na makazi yake. Hatua hii ni nzuri. Hata hivyo, wasi wasi wangu ni namna tunavyotawanya Ofisi na makazi ya viongozi katika maeneo mbalimbali nchini. Naona kama haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwa mfano, pale Tunguu - Zanzibar kumejengwa ofisi nzuri sana ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, matumizi ya Ofisi hiyo ni madogo sana. Inawezekana kabisa hali ikawa kama ilivyo kwa Ofisi ya Bunge, Tunguu ambayo kwa kweli ni kama haitumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri badala ya kuendelea kitumia pesa nyingi za Serikali na walipa kodi wa nchi hii, zitumike Ikulu zilizopo Mikoani na Wilayani kama ilivyo Tanzania Bara kwa ajili ya makazi ya muda kwa viongozi wetu wa kitaifa wanapokuwa Zanzibar/Pemba kwa ziara za kikazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuanzishwa Wizara – Ofisi ya Makamu, inayoshughulikia Mazingira, lakini bado ukataji wa miti bado unaendelea. Ushahidi wa jambo hili ni namna mikaa inavyoingia mijini. Leo ukienda Mikoa yote, utaona idadi kubwa ya mikaa ikiingia mjini kwa baiskeli na magari. Huwa najiuliza: Je, wote hawa wana leseni za kufanya biashara hiyo? Kwa uchunguzi wangu mdogo, wanaojihusisha na biashara hii hawana leseni. Hii ina maana kwamba miti hukatwa hovyo hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kilimo cha tumbaku kinachangia sana ukataji miti, maana ukaushaji wake hutumia kuni sana. Naomba kujua: Je, kuendelea kulima kilimo cha tumbaku sio sawa na kuendelea kuhamasisha ukataji miti hovyo? Hatuoni kwamba kama hali hii ikiiendelea tutaendelea kutengeneza jangwa taratibu? Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira inachukua hatua gani katika kukomesha hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi katika Ofisi ya Rais akiwemo Waziri Batilda Buriani na wasaidizi wake. Urithi wa nchi duniani pote ni kuwa na miti mingi ili kuendeleza maisha duniani. Kwa bahati mbaya, nchi yetu ya Tanzania bado haijaliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miti mingi bado inakatwa ovyo. Pamoja jitihada zote zlizoelekezwa kwa wananchi toka Serikalini, imeshindikana kupunguza ukataji ovyo wa miti. Serikali hufanya kazi ya ziada katika kuelimisha wananchi kukagua mapori mbalimbali Mikoani. Kwa hiyo, nashauri kwamba jitihada za kutoa elimu ziongezwe kukagua mapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchomaji moto umekithiri pia katika maeneo mengi, hali inayokimbiza viumbe hai wakiwemo wadudu, wanyamapori na mimea asilia, ambayo baadhi ya mimea hiyo ni dawa asilia ambayo ni tegemeo letu la baadaye katika madawa asilia nchini. Tuzingatie kuwa dawa asilia inategemea sana ulimwenguni kutoka Afrika na Asia. Katika hali hii uoto unapotea na ukame ndio unatawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yenye uoto zaidi katika Mikoa na hasa milimani na mabondeni ni lazima Serikali iyalinde binadamu wasiweze kuyafikia ni lazima yaachwe huru. Aidha, maeneo ya kutumika kwa ajili ya maendeleo kama vile katika kuleta umeme kwa kutengeneza mabawa na kutumia mito, nashauri tahadhari kubwa zichukuliwe katika kuhakikisha kuwa ujenzi huo unaendana na uhifadhi wa mazingira katika kulinda makazi ya viumbe hao kwa mfano vyura, konokono, samaki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba viumbe katika misitu wahifadhiwe. Msitu wa Vikindu kati ya Dar es Salaam na Pwani, msitu huo umekatwa kabisa wote. Vinyonga wenye pembe tatu pekee wanapatikana hapa katika msitu huu na hamna popote duniani wanapatikana kwa wingi. Ni ajabu sana kuona kuna wizi wa maliasili na Serikali imefunga macho mpaka kuachilia msitu huo kuteketea kabisa. Je, viumbe hao, vinyonga wa pembe tatu wamekwenda wapi? Inasikitisha sana. Jambo hili mlitilie maanani.

Mhesimiwa Naibu spika, naunga mkono hoja, lakini okoeni viumbe vya asilia vya Mwenyezi Mungu.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na ambayo inaimarisha Muungano wetu ambao sasa una zaidi ya miaka 46 na ni mfano katika Bara la Afrika na unaendelea kuimarika siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana ushirikiano wa kiuchumi na kijamii ambao Zanzibar inapata kupitia Muungano huo. Aidha, naipongeza Serikali ya Muungano kwa kutoa fedha za Barabara ya Amani hadi Mtoni jumla ya Sh.1,600,000,000/=. Kwa ujenzi wa barabara hiyo mimi binafsi kama Mbunge wa Jimbo la Mtoni kwa njia ya Maswali Bungeni niliuliza maswali karibu matatu kuhusu barabara hiyo. Naomba kujua wakati wa kufanya majumuisho, ujenzi kwa ajili ya barabara hiyo utaanza lini hasa ukizingatia kuwa fedha zipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na.16, ya mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo imeshapitishwa na nalipongeza Bunge la Jamhuri wa Tanzania kwa kupitisha sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge kutoka Zanzibar bado mpaka leo hatujapata pesa hizo kupitia Halmashauri zetu. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho kujua ni kwa nini Wabunge kutoka Tanzania Bara wameshapata fedha zao na Wabunge kutoka Zanzibar bado fedha hazijapatikana?

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara yake kwa bajeti hii. Pili, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) - Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Buriani kwa ziara aliyoifanya jimboni kwangu hasa maeneo ya Nyamongo ambapo kuna mgodi wa *North Mara* pamoja na maeneo yanayozunguka mgodi yaliyopata maafa makubwa kutokana uchanjaji wa mto Tigite na kujionea madhara makubwa waliyopata wananchi pamoja na wanyama kama ng'ombe, mbuzi, kondoo hali ambayo ilipelekea wananchi kupoteza maisha kwa kutumia maji yenye sumu ya mto Tigite. Ziara hiyo ilikuwa na ujumbe mkubwa wa Serikali ambao ulikuwa na Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Makatibu wa Wizara husika, wataalam mbalimbali kwa lengio la kulitatua tatizo la *North Mara.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana wananchi kulipwa fidia mapema ili kuhama maeneo ambayo shughuli za migodi zinatarajia kujengwa ili kuepuka madhara ambayo hutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwamba Baraza la Hifadhi la Mazingira *(NEMS)* kufanya kazi kwa karibu sana na mgodi wa *North Mara* na Watumishi wa *(NEMC)* wawe ni watumishi ambao ni Wazalendo. Mara nyingi kuna baadhi ya wafanyakazi ambao husaliti wananchi (Watanzania) na kukumbatia wageni *(Investor).* Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwa na ratiba ya kutembelea miradi ya migodi mara kwa mara ili kugundua kasoro ili kuepuka madhara kama yaliyotokea katika maeneo ya kata za Kibasuka, Nyamwaga, Nyarokuba, Kemambo na Matongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu kama wananchi waliopata madhara pamoja na wanyama hata kupoteza maisha wamelipwa fidia? Ni mpango gani wa muda mfupi, muda wa kati na wa muda mrefu wametekelezwa kwa kupunguza madhara ambayo yamewapata wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa wananchi katika maeneo yanayozunguka mgodi wanachi wanaendelea kupata madhara yanayotokana na Mto Tigite, akina mama wanaendelea kupata madhara makubwa ya mimba kuharibika magonjwa ya ngozi, mifugo kama vile ng'ombe mbuzi, kondoo na punda, zinaendelea kufa. Napenda kuishauri Serikali kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa migodi yote hapa nchini. Namwomba Waziri wa Mazingira atembelee tena mgodi wa *North Mara* ili uweze kubaini kasoro ambazo hazijarekebishwa na kampuni ya mgodi wa *North Mara*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, miji yetu ni michafu sana katika viwanda, gereji, shughuli zote hizo zinafanywa katika makazi ya watu, takataka zinatupwa ovyo ovyo barabarani, uvutaji wa sigara ni moja ya tatizo kubwa kwa watumiaji na wasiovuta kwa vile huvuta sigara hadharani. Tunaomba Muswada wa Sheria kuhusu uvutaji wa sigara hadharni uletwe ili kuwepo sheria ya kuzuia uvutaji sigara hadharani.

Pamoja na hayo, napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo langu la Tarime kwa Ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote tangu nichaguliwe kwa uchaguzi mdogo wa mwezi Oktoba, 2008 baada ya kufiwa na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe. Mungu iweke roho ya Marehemu Peponi. Natambua juhudi zilizofanywa na wananchi na kuweza kushinda kwa kishindo chaguzi ndogo zilizofanyika hapa nchini, yaani Kiteto, Busanda, Biharamuro na Mbeya, ni Tarmie tu tuliweza kushiriki kwa upande wa upinzani. Hii ni heshima kubwa kwangu pamoja na chama changu cha CHADEMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Batilda Buriani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Katibu Mkuu wake Ruth Mollel pamoja na Wakurugenzi wao kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kupanga na kusimamia program za hifadhi ya mazingira nchini wakishirikiana kwa karibu sana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeshiriki katika program mbalimbali kinchi na Kimataifa zinazosaidia marekebisho ya athari za mabadiliko ya tabia za nchi, jambo ambalo linapaswa kuendelezwa ili kuzuia maafa mbalimbali yanayotokea hapa duniani Tanzania ikiwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba mazingira ni suala mtambuka, ni muhimu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kuwa na mawasiliano ya karibu sana na Tawala za Mikoa (TAMISEMI) katika kutekeleza sheria ya mazingira (2004) kwa masuala yanayowahusu ikiwa ni pamoja na mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Ma-Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya ndizo zinazopaswa kusimamia na kudhibiti masuala yanayohusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla, lakini kwa hali halisi mamlaka hizo hazitoi umuhimu unaotakiwa hasa kwa maeneo yafuatayo:-

(a) Uchomaji wa moto ovyo wa misitu, mapori na mbuga umekuwa ni tishio kubwa kwa viumbe vingi na mimea ya asili kwa ujumla hapa nchini. Ukizunguka nchi nzima hasa wakati wa kiangazi unajionea jinsi mioto inavyochomwa ovyo utafikiri hakuna msimamizi hasa katika Mikoa ya Rukwa, Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Singida, Pwani na Lindi. Hivi sasa hata miti ya kupandwa huchomwa moto. Ni tishio kubwa.

(b) Uchafu katika Miji pia ni tatizo kubwa. Kwa kuwa uchafu ni tabia na hali ya sasa inaelekea tabia hii ya uchafu imejijenga kwa watu wengi, watu wanatupa taka ovyo, miundombinu ya maji taka haipo kiasi ambacho si kitu kigeni kuona maji machafu yakitiririka ovyo hata barabarani kiasi ambacho hata watoto hucheza humo. Utaratibu huo ni hatari sana hasa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendeza kulipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa kazi nzuri wanayofanya hasa kwa kuweka utaratibu wa kuwa karibu na wadau mbalimbali wa mazingira kwa utoaji wa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na elimu kuhusu sheria ya mazingira ya mwaka 2004. Kutokana na kazi nzuri wanayofanya kuwa umuhimu wa kuwaongezea fedha ya kutosha katika bajeti yao ambayo itawasaidia pia kuziimarisha Ofisi za Kanda zilizofunguliwa ambazo zinafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kushauri kwamba ni vizuri Baraza la Mazingira (*NEMC*) nalo pia lifahamike kwa jina kama nchi nyingine za Afrika ya Mashariki ambako taasisi kama hii hufahamika kuwa ni *Authority* badala ya *Council*. Hii itasaidia kuwa na *Uniformity* katika nchi zote. Itapendeza likiitwa NEMA badala ya NEMC.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika siku hii ya leo na kupata fursa ya kuchangia hoja hii ingawa ni kwa maandishi. Hata hivyo, nategemea kuwa maoni yangu haya yatazingatiwa na kuchukuliwa hatua za kufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningelipenda kuchangia ni kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama tunavyoelewa kuwa kumekuwa na mmonyonyoko mkubwa wa ardhi unaosababishwa na ongezeko la kina cha maji ya bahari na kusababisha mawimbi makubwa ya bahari hasa katika fukwe za bahari ya Hindi na kuathiri sana miundombinu pamoja na makazi ya watu wanaoishi karibu na fukwe hizo kama vile vijiji vya fukwe za Pwani ya Kusini Mashariki ya Kisiwa cha Unguja vya Jambiani, Paje, Bwejuu na Dongwe (Michamvi)

Mheshimiwa Naibu Spika, athari hizo ni pamoja na fukwe za maeneo ya Kigamboni Tanzania Bara katika pwani ya Chuo cha Taasisi ya Mwalimu Nyerere, suala ambalo nimekuwa nalizungumzia mara nyingi katika Bunge lako hili Tukufu kuwa linaweza likasababisha hasara kubwa kama hatua za kufaa hazikuchukuliwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali kulizingatia suala hili na kulitafutia ufumbuzi wa kufaa. Kama hapana pesa za kutosha zilizopangwa katika bajeti hii, basi naishauri Serikali kutafuta pesa na kulichukulia suala hili kuwa la dharura na kukiokoa chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia katika maoni yangu haya ya Wizara hii ya Makamu wa Rais ni suala la Mfuko wa kuendeleza Maendeleo ya Jimbo (*CDCF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kupitisha sheria ya mfuko huu wa kuendeleza maendeleo ya Jimbo na kuanza kutekelezwa kwa kutolewa fedha na kuanza kutumika kwa awamu mbili za bajeti ya 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, fedha hizo zimeshaingizwa katika Benki lakini utaratibu wa upatikanaji wa fedha hizo kule Zanzibar si wa kuridhisha, kumekuwa na urasimu wa upatikanaji wa fedha hizo ambazo kwa utaratibu huo uliopo umesababisha kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha hizo kwa kutumika katika Majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuzingatia utaratibu wa kuzipitisha fedha hizo kupitia aidha, Ofisi ya Bunge moja kwa moja au kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ambayo natumai itasaidia sana kupunguza urasimu uliopo hivi sasa ambao kwa upande mwingine kwa upande wa Zanzibar unakwenda kinyume na sheria iliyounda mfuko huo hasa katika upande wa watu wa kutia saini cheki za Mfuko huo katika Majimbo ya Zanzibar, naomba sheria hii izingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri wangu huu, nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Muungano; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mazingira na watendaji wote wa Wizara hii na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kuhusu utunzaji wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza msisitizo zaidi uwekwe kwenye Halmashauri zote nchini kusimamia kwa karibu suala zima la utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya miji yanakusanya takataka nyingi sana za kila aina, lakini hakuna utaratibu mzuri wa kuzikusanya wala kuziangamiza au kuziharibu badala yake wanakwenda kuzibwaga eneo lingine na kufanya madampoo hatari mijini. Naishauri Serikali ijipange kwa miji yote nchini, takataka ziharibiwe badala ya kuzihamishia wanakodhani ni mbali na wakazi wengi. Aidha, Serikali izitenge takataka kwa aina zake kwa ku-*recycle* katika vifaa vingine.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napendekeza Halmashauri zinunue vifaa vya taka na kuvisambaza maeneo yote katika *Council* inayohusika (au mamlaka husika).

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya matumizi au utunzaji bora wa mazingira itolewe na ikibidi kuwe na vikundi vinavyosimamia hili ili tuondokane na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za vifaa vya usafi wa mazingira mfano, dawa za vyoo, kung'arisha kuta na sakafu za vyooni, mabafuni na majiko vipunguzwe bei ili wananchi wavimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vijijini, sheria izingatiwe. Ukaguzi wa majumbani urejewe kwa nguvu sana. Siyo siri, bado kuna wananchi hawana vyoo, sielewi tusemeje wanapotaka kwenda faragha wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, hapo kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira yanayopelekea pia maradhi ya matumbo kama homa za matumbo, kipindupindu na kuhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi uangalie vyoo, mashimo ya taka na mahali pa kupikia chakula (majiko). Hali kadhalika ukaguzi uzingatie mahali wanapopata maji ya kunywa na kupikia. Mito yetu ya asili haitunzwi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuzingatia kwa kushirikiana na Wizara zingine na wadau wengine, maeneo ya Maziwa (*Lakes*) yaangaliwe kipekee. Kuna utiririshaji wa maji machafu Ziwani. Pia watu wanaendelea kujenga karibu na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liende pamoja na Jiji la Mwanza waache kutiririsha maji machafu ziwani. Mtaro mkubwa ulio Jijini Mwanza unaopeleka maji ziwani ni hatari kwa mazingira na afya. Aidha, wakazi wa milimani, Jijini Mwanza watafutiwe makazi mengine hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na afya na kuweza kunipa wasaa wa kuchangia hotuba hizi zilizokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda sana kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuliendesha Bunge hili bila ya upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri wa Wizara hizi pamoja na wadau wote wanaohusika na Wizara hizi kwa hotuba zao. Shukrani za pekee ziwaendee Mawaziri Vivuli wa Wizara hizi ambazo zimejaa hekima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira, Serikali inapiga sana kelele kuhusu ukataji wa miti lakini la kushangaza hakuna nishati mbadala kwani wananchi wengi wanatumia kuni na mkaa, kwa hiyo, kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweke mipango kabambe ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata nishati mbadala ili wanusuru mazingira yetu.

Huwezi kuyanusuru mazingira kama hajapanga mipango mikakati na kutoa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanapata athari kubwa kutokana na wawekezaji wa madini kutochukua tahadhari ya kulinda mazingira. Kwa hiyo, Serikali iwachukulie hatua kali wale wawekezaji wanaozunguka makazi ya watu na kuchafua mazingira na kusababishia madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali haijaweka mikakati kwa wananchi wanaosafiri na magari au mabasi ya abiria kutupa chupa au uchafu njiani, je, Serikali inawachukulia hatua gani wale ambao wanagundulika kufanya hivyo au sheria tunazozitunga zinabakia kwenye makaratasi tu, hawaeleweshwi wananchi umuhimu wa usafi katika nchi yao? Tunaiomba Serikali iwaelimishe wananchi namna ya kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kufanya jitihada kubwa ya kutatua kero za muungano, bado Serikali inakwenda taratibu sana, hasa ukizingatia miaka yote hiyo imetatua kero mbili tu. Naiomba Serikali ijitahidi sana kwenda kwa kasi ili hizi kero ziweze kuondoka na kuuweka Muungano wetu katika hali nzuri na kuondoa manung’uniko kutoka kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2008 tulishuhudia kamati hizi za fedha kukamilisha kazi yake, lakini la kushangaza na kusikitisha mpaka leo Serikali hii ya Muungano imeshindwa kutatua kero hii ya asilimia 4.5, kwa nini Serikali hii ina kigugumizi cha jambo hili hasa ukizingatia tangu tumeingia mpaka leo tunamaliza kipindi cha miaka mitano kumetatuliwa kero mbili tu na itachukua miaka mingapi kumaliza kero zilizobakia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii inaonesha Serikali haina nia ya dhati au tuseme wanaona hakuna umuhimu wa mambo haya? Mwisho na kwa umuhimu mkubwa nampongeza Mheshimiwa Dr. Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kusisitiza maridhiano ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuonesha nia ya kuleta maridhiano ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Nakushukuru sana. Ahsante.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanazozifanya katika ofisi hii ambayo ndio uti wa mgongo wa Muungano wetu. Utendaji wao mzuri ndio uliotufikishia kuwa Muungano wetu ufikie umri huu mrefu (miaka 46).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo ya hotuba ya Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Muungano, mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF* II) bado lipo tatizo la uchangiaji wa miradi hii kwa jamii ambapo jamii inaendelea kushindwa kuchangia kiasi cha asilimia iliyowekwa na Serikali pamoja na kuwa asilimia hiyo ya uchangiaji wa jamii kwa miradi ya maendeleo ilipunguzwa kutoka asilimia 20 hadi 15%. Hata hivyo wananchi wameshindwa kutoa michango yao kwa asilimia hiyo (15%) na hivyo miradi hiyo kutomalizika kwa muda uliopangwa kwa Mbunge na Mwakilishi na hata Diwani wao ndio limelemewa na mzigo huo (kwa kuchangia asilimia 15).

Naiomba Serikali ipunguze tena asilimia ya uchangiaji kwa jamii kwenye miradi ya maendeleo (ujenzi wa shule, zahanati, soko na kadhalika), nishauri mchango huo uwe asilimia tano (5%), ili kuwapunguzia mzigo Waheshimiwa Wabunge au Wawakilishi na Madiwani ambao ndio wachangiaji wakuu wa asilimia hiyo. Aidha, miradi hiyo itakamilika kwa muda muafaka tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua kama *TASAF II* itakuwepo au ndio hapatakuwa tena na miradi ya *TASAF* maana Mheshimiwa Waziri hajataja katika hotuba yake ya mwendelezo wa miradi ya *TASAF*. Hali kadhalika naiomba Serikali iongeze fedha ya miradi hiyo kwa vile Tshs.36,000,000/- haitoshi kwa mradi wa ujenzi hasa wa madarasa ya shule kutokana na kupanda kwa gharama ya vifaa vya ujenzi. Nashauri *ceilling budget* kwa miradi ya ujenzi usipungue milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MACEMP*, kutokana na mabadiliko ya hali za nchi duniani visiwa vingi vimeendelea kuathirika sana kutokana na mimomonyoko ambayo huvimega visiwa hivyo, jambo ambalo kama hatua za makusudi hazijachukuliwa visiwa hivyo vitatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi inazozichukua Serikali ya kuboresha usimamizi wa mazingira ya pwani, lakini bado kunahitajika juhudi zaidi ya kuvinusuru visiwa vyetu kwani kasi ya mimomonyoko ni kubwa na hasa Kisiwa cha Unguja moja ya maeneo yanayomomonyoka kwa kasi ni maeneo ya Marukubi na Kibweni na sioni juhudi zozote za kuzuia mimomonyoko hiyo zikichukuliwa na Serikali pamoja na kuwa bilioni 26 zilipelekwa Tanzania Zanzibar. Naiomba Serikali iyafanyie kazi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. Naipongeza Serikali kwa kulipatia ufumbuzi suala hili, hata hivyo bado utekelezaji wake unasuasua kwa watendaji wa mamlaka ya mapato Tanzania hasa kwenye masuala yahusuyo uingizaji wa magari Tanzania Bara kutoka Zanzibar. Bado kuna ukiritimba hapo bandarini (Dar es Salaam) ambapo gari linapofika bandarini hapo, ni lazima likae japo kwa siku tatu kwa uchache pamoja na kwa taratibu zote mteja (mwenye gari) atakuwa amezikamilisha, kitu ambacho humlazimisha mwenye gari kutozwa tozo la ghala (*storage charge*).

Ni vyema *TRA* ikaweka utaratibu mzuri zaidi hapo bandarini wa kuwa na *one stop centre* ambapo kutapunguza ukiritimba uliopo sasa ambapo mteja humlazimisha kutembea zaidi ya mita zipatazo 300 kufuatilia nyaraka kutoka *strong room* kwenda ndani ya bandari (nitakuwa nimeeleweka) ambako kunatolewa nyaraka za kuruhusu kutoa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sula la mafuta na gesi asilia, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano katika hotuba yake alitaja suala la mafuta na gesi asilia Serikali inaangalia utaratibu wa mgawanyo wa mafuta (kama nilisikia vinginevyo atanisahihisha) lakini kwenye kitabu chake cha hotuba sijaona kipengele hicho. Hata hivyo, kwa mujibu wa vyombo vya habari inasemekana kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeshawasilisha rasmi suala hili kwa SMT ambapo SMZ imeamua kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia kwenye mambo ya Muungano. Je, ukweli wa jambo hili ukoje na je, hakuna masuala mengine ambayo baadaye SMZ ikitaka kuyaondoa kwenye Katiba yanayohusiana na mambo ya muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuitengea fedha barabara ya Mtoni – Aman (Benjamini Mkapa *Road*) ambayo ilikuwa ni ahadi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na ndiyo maana ilipewa jina lake wakati akiifungua. Naomba SMT izitoe fedha hizo kidhati na kwa wakati ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kama alivyoahidi Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ambayo alisema bila kukamilika kwa ujenzi huo isingependeza hata kidogo barabara hiyo ikapewa jina lake. Ni imani yangu kuwa SMT chini ya uongozi wa CCM ni sikivu na itatekeleza ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira, bado kuna changamoto kubwa wa uhifadhi wa mazingira ambapo kwa kiasi kikubwa wakulima hasa wa Tumbaku hukata miti kwa wingi bila kupanda mingine kwa ajili ya upanuzi wa kilimo hicho na ukaushaji wa tumbaku. Ni vizuri Serikali ikachukua hatua za makusudi za kuona ni jinsi gani inaweza kuwasaidia wakulima hao kupunguza au kuondoa kabisa uharibifu mkubwa wa ukataji miti kwa kuwapatia nishati mbadala ya kisasa hasa ile ya ukaushaji wa tumbaku badala ya kuendelea kuwahamasisha kuendelea kuongeza kilimo cha tumbaku na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa siitendei haki Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mafanikio makubwa iliyoyafanya kwa upande wa Tanzania Zanzibar ambayo kwa orodha ni mengi, lakini nitaorodhesha mafanikio machache tu ambayo ni pamoja na ujenzi wa Tawi la Benki Kuu (*BOT*), Ofisi Ndogo ya Bunge, Ofisi Ndogo ya Makamu wa Rais, miradi ya *TASAF* miradi ya *MACEMP, PADEP*, miradi ya ujenzi wa hospitali ya kisasa JWTZ – Bububu, ujenzi wa nyumba za Polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa hotuba nzuri ya Bajeti, tulizungumza mimi na Mheshimiwa Waziri ili utembelee eneo langu la Keko na ukanikubalia. Eneo hilo lina mmomonyoko wa ardhi na pia mfereji wa Serengeti ambao umeharibu mazingira maeneo

ya Chang'ombe, Keko na Miburani. Nimeona niweke kwa maandishi ili upate kunikumbuka Mheshimiwa Waziri Dada yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Makamu wa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, nimpongeze pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika kuandaa hotuba hii ya Bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni na ushauri kuwa kuwe na kitengo kitakachoratibu utaratibu mzima unaohusiana na upandaji wa miti usimamizi wa mazingira na usafi, pia kuwe na watu makini ambao wanaguswa sana katika suala la uhifadhi wa mazingira, wapatiwe mafunzo hata kwa kwenda nchini China kujifunza juu ya kusimamia upandaji wa miti kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa miti wa umri wa mimea hiyo na kisha kuja kutafsiri kwa vitendo hapa nchini kwetu.

Pia kuwepo na fungu la fedha ambaloo litaweza kuwasaidia vijana ambao wanajihusisha na uuzaji wa miti na maua hasa katika Jiji la Dar es Salaam hali ambayo itasaidia vijana hawa kuitunza miti hiyo mpaka ikue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na kodi itakayotokana na kutoza ada ndogo katika mashine na vyombo vya moto kama magari, treni, meli, ndege, viwanda na kadhalika ambavyo huzalisha moshi mwingi ambao huharibu mazingira *(Carbon Tax)* itasaidia Serikali kupata kiasi kikubwa cha fedha ambacho kitasaidia eneo hili la uhifadhi na upandishaji kodi hiyo hiyo itaweza kusaidia katika sekta nyingine za kijamii. Tozo la shilingi 10,000/= kwa gari dogo kwa mwaka ni shilingi 50,000/=, viwanda na mitambo mingine kwa idadi kubwa ya mitambo hiyo hali itaweza kubadilisha sura halisi na itakuwa chanzo kipya cha kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wakazi wa Mji wa Moshi na Mji wa Mwanza kwa kuweka miji yao katika hali ya usafi. Mazingira ni uhai kwani yasipotunzwa twaweza kupata maradhi na kadhalika hivyo basi tuyatunze na tuyalinde. Pia Sheria ndogo za kila halmashauri na miji zisimamie usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mji wa Dar es Salaam wazoa taka na magari ya kuzolea taka wamekuwa na tabia za kitapeli kwani michango hutolewa kwa kila kaya au kila nyumba kwa ajili ya uzoaji wa takataka lakini waweza kukaa zaidi ya wiki mbili na gari la taka usilione.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za mijini mara nyingi hazina nafasi ya kuchimba mashimo ya taka. Hatma ya yote inabidi uwape taka vijana ambao hupita na

mikokoteni. Vijana hawa huzitupa wapi taka hizo? Na kama wanazitupa sehemu ambayo si sahihi wanafanywa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi wa kawaida ana mamlaka gani juu ya huyu anayetupa taka ovyo? Pale mvua zinaponyesha sisi wananchi hatuwaoni wale wanaofungulia mitaro ya maji machafu ya vyooni na karoni? Tunafanya nini pindi tuonapo hayo? Hatua gani zinachukuliwa dhidi ya watu hao? Ni wangapi wanafanya kazi hii ya ulinzi wa uharibifua wa mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri majibu ya maswali haya ndiyo uwezekano wa kuweza kutunza mazingira yetu na kutokomeza uchafu uliokithiri katika miji yetu. Ahsante na kazi njema.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 99 katika ukurasa wa 62 *"Strange the thing management effectiveness in National Parks Systems"* inahusisha milima ya Livingstone na Ludewa, naomba ufafanuzi kwani eneo hili bado si hifadhi ya Taifa.

Kifungu 127 katika ukurasa wa 78 kwa vile usipoziba ufa hutajenga ukuta na kwa kuwa miradi ya Liganga na Mchuchuma imeanza na kwa kuwa miradi hii itavuta watu wengi sana na kusababisha athari kubwa za mazingira. Wizara hii inajihusisha vipi kuzuia hili hususani kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mioto nchini linaloleta uharibifu mkubwa wa mazingira na binadamu linashughulikiwa kana kwamba liko sawa nchi nzima. Kwa nini isitengenezwe ramani ya maeneo yanayoathirika na mioto kutegemeana na ukubwa wa athari na vyanzo vyake ili kupata mbinu za kupambana na mioto hiyo kwa mbinu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafuta ya moto poa ambayo ni nishati mbadala yameishia wapi hususani kuhusiana na ufanisi na tija kama mbadala wa mkaa na kuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inafadhiliwa asilimia 100 na wahisani? Je, Serikali haithamini mabadiliko ya tabia nchi na athari zake kiasi kwamba tunaona hakuna haja ya kuwekeza katika sekta hii? Je, kweli uhifadhi huu utakuwa endelevu kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inawasaidia vipi wananchi wa Ludewa wanaoishi kando kando ya Ziwa Nyasa katika kuwapa mbadala wa kulima kwenye miteremko ya milima ya Livigstone kwa ajili ya kujikimu.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuiandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira uchimbaji wa madini, katika nchi yetu hivi sasa kuna uchimbaji mkubwa na mdogo wa madini katika maeneo mbalimbali. Tanzania ni nchi ya pili inayozalisha dhahabu na nchi yetu inazalish madini tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchimbaji huo wa madini unaleta athari kubwa kwa mazingira na athari kubwa kwa maji yanayosafishiwa dhahabu katika makazi ya binadamu kutokana na maji hayo kuwa na kemikali na milipuko ya baruti na baadae kuwa sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaiomba Serikali kupitia Baraza la Hifadhi la Mazingira iwe na wafanyakazi wa kutosha ili kudhibiti yale yaliyotokea *North Mara* yasiweze kutokea tena na wahusika wa uchimbaji wa madini waweze kuwasimamia wachimbaji na kutoa tahadhari pale maporomoko ya ardhi yanapokaa katika hali ya hatari waweze kuzuiwa waondoke katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira ya uchimbaji mchanga, kunajitokeza uchimbaji wa mchanga kiholela kwa ajili ya kujengea, hii ni hatari kubwa kwa sababu sehemu kubwa ya ardhi huleta maporomoko na miti mingi huanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haitengi maeneo maalum ya kuteka mchanga? Na ikiwa Serikali imetenga maeneo hayo na wananchi wanateka maeneo mengine kwa nini hawachukuliwi hatua ili kupunguza maporomoko hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maridhiano tunaomba Mwenyezi Mungu ayajalie yawe ya kweli na amani na yale yaliyokusudiwa yatekelezwe ili nchi yetu iwe na imani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni lazima tuwapongeze viongozi wetu wawili Rais Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Maalimu Seif Sharrif Hamad kwa kukaa pamoja na kuona katika nchi yetu sote ni ndugu, hakuna haja kukaa kwa kufarakana na kugombea mara zote kwa matatizo ya kisiasa, hii ni dalili njema ya kujenga Zanzibar mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu nawatakia kila la kheri watendaji wote kwa hotuba hii. Ahsanteni sana.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima niseme *Alhamdulillah.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hotuba husika ni dhahiri kwamba Serikali inafanya kazi kwa nguvu zake zote kuiweka nchi katika mazingira mazuri. Pamoja na nia hiyo nami natoa mawazo yangu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia niupongeze Muungano wetu kwa mara ya kwanza kufanikisha Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo kwetu Zanzibar, kitendo hiki ndio chachu ya maendeleo katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani Watanzania wengi wanatumia kuni na mkaa kwa kupikia chakula, kuni na mkaa inapatikana na miti kwa kutegemea nishati hiyo inaleta uharibifu mkubwa wa mazingira kwani miti inakatwa kwa wingi hatimaye itatokea ukosefu wa mvua. Je, Serikali imejiandaaje kunusuru hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, miti hunusuru mmomonyoko wa ardhi. Hali ya maziwa yetu na mito imepungua sana kina chake kutokana na mmomonyoko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tumepewa rasilimali kubwa na Mwenyezi Mungu. Eneo hili ni lile la madini kwani madini ni hazina inayopatikana ndani ya ardhi kwa njia ya kuchimba. Uchimbaji mkubwa ama mdogo huleta uharibifu wa mazingira kama vile vumbi, uvujaji wa kemikali na ulipuaji wa baruti. Mambo haya yote kwa muda fulani huwa sumu ambayo hatimaye inakuwa ni hasara kwa jamii ili tunusuru haya Serikali iiandae vizuri *NEMC* ili iwe karibu na maeneo ya wachimbaji wa migodi ili kunusuru maisha ya Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau yaliyotokea katika mgodi wa *North Mara*, chombo kinachosimamia mazingira nchini *(NEMC)* ni wazi kwamba kina uhaba wa wataalamu wake, hivyo ni kiasi gani Serikali imejiandaa kuhakikisha wataalamu hao wapo na wanakidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muungano, kwa kuwa Serikali zetu mbili zimekithiri kuwepo kwa dosari katika Muungano wetu pamoja na Serikali zetu kukaa pamoja ili kuondoa dosari hizi. Napata wasiwasi mkubwa kuona hakuna sababu ya kuchukua muda mrefu kutatua dosari hizi. Kwa nini tuchukue muda mrefu ilihali kasoro zimeonekana? Naiomba Serikali isimamie ili kuondoa kasoro hizi. Hii itaondoa dhana mbaya kuwa Muungano ndio unaoiondolea Zanzibar uchumi wake. Kufanikisha haya ni kuisadia Zanzibar. Mungu ubariki Muungano. Ahsante.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mawasilisho yake ya hotuba ya Bajeti ambayo ni nzuri na yenye kuleta matumaini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa usimamizi wake makini wa masuala ya mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashauri Waheshimiwa, Mawaziri wote wawili mambo yafuatayo, kwanza Mradi wa *MACEMP* unahitaji kufanyiwa mapitio ili mapungufu yake yasawazishwe kwa wakati. Ushahidi wa ushauri huu unatokana na malalamiko ya wavuvi wengi wa Zanzibar wanalalamika kuwa nyavu wanazopewa ni

ndogo sana na haziwezi kuleta tija. Aidha boti nazo hazina uwezo wa kwenda bahari za mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya uchomaji moto misitu bado zipo na zinatisha kwani zinaathiri mazingira kama sheria zilizopo ni nyepesi basi ziangaliwe zaidi ili ziboreshwe na ziweze kukidhi haja ya udhibiti wa mazingira na kama sheria zinatosha basi usimamizi unahitaji kuwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo zaidi uwekwe kwa Waheshimiwa Mawaziri, kuhudhuria kikamilifu vikao vya kuzungumzia kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Serikali ya mwaka huu nilichangia kuhusu 4.5% ya Mapato ya Muungano ambayo inapatiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la muda mrefu kila siku Wabunge tunaotoka Zanzibar tunaulizia kuhusu suala hili na tunapata majibu ya kuwa tuvute subira. Suala hili linashughulikiwa na Serikali zote mbili lakini kila Bajeti inayokuja huwa majibu ni yale yale yanafanana. Je, ni lini suala hili litafika mwisho, ili kila siku tusiendelee kuulizia suala hili

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya Mazingira nitazungumzia kuhusu suala la uchafu ambao upo katika masoko yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko yetu yote yanapata taka nyingi kutoka vijijini kunakotoka mazao. Sasa hivi Serikali kwanini haiwafahamishi wanaoleta mazao haya wapunguze kuleta majani mengi yanayosababisha taka nyingi katika masoko yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia mmomonyoko wa ardhi kwenye kingo za bahari. Kwa kweli bahari inakula sana ardhi yetu lakini kuhusu hili hatuna la kufanya isipokuwa nikuangalia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la muda mrefu kila siku Wabunge tunaotoka Zanzibar tunaulizia kuhusu suala hili na tunapata majibu ya kuwa tuvute subira. Suala hili linashughulikiwa na Serikali zote mbili lakini kila Bajeti inayokuja huwa majibu ni yale yale yanafanana. Je, ni lini suala hili litafika mwisho, ili kila siku tusiendelee kuulizia suala hili

**MHE. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza kwa kuzungumzia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF II)* kama ifuatavyo:-

(a) Kama ilivyofanyika katika utekelezaji wa awamu ya kwanza hatua za utekelezaji zinafanyika kwa pole pole mno. Baadhi ya miradi haikukamilika kama ilivyotarajiwa hasa miradi ya maji pamoja na ile ya Zahanati. Nashauri *speed* ingesisitizwa.

(b)Vifaa vinavyowekwa kwenye uchimbaji wa visima huwa havina viwango imara. Kwa mfano robo tatu ya mashine za maji kwenye vina vimeharibika chini ya mwaka.

Wilaya ya Chunya mashimo mengi yameachwa wazi baada ya kuokota dhahabu hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo. Je, Serikali ina mpango wowote wa kufunika?

Hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo wanahitaji elimu ya uhifadhi mazingira.

Wapo wachimbaji hasa wale wadogo wadogo wa madini ya dhahabu ambao hawatoi kodi ya aina yoyote isipokuwa kwa wale wachache wakati wa kupata kiwanja utaratibu ungefanyika wa kila anaeamua kuchimba dhahabu kwa kiwango kidogo atoe chochote Serikalini.

Kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira katika Bonde la Ziwa Rukwa unaosababishwa na kilimo, ufugaji usio endelevu na uvuvi haramu matokeo ya uchafuzi huo ni kupungua kina cha maji, kupungua rasilimali ya maliasili ya samaki na Ziwa kukauka kwa mfano katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ziwa Rukwa limeendelea kukauka umbali wa kilomita tisa.

Ni maoni yangu kwamba Serikali ingechukua hatua za makusudi za kulinusuru Ziwa hili lisikauke au kuchafuliwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika napenda kupongeza hotuba ya Waziri kwa kuelezea kwa ufasaha juu ya mazingira. Mazingira ni somo pana na ni muhimu sana kwani pasipo mazingira mazuri nchini hali ya maendeleo au uhai itazorota.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara kwa kutoa elimu kwa jamii na semina mbalimbali za kutoa miongozo na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uharibifu wa mazingira unaofanyika maeneo mengi kwa kuchoma misitu huku Serikali inakaa kimya misitu ikiteketea na Bainowai ya nchi kuharibika. Uchomaji wa mkaa jambo hili linaendelea kwa kasi na miti mikubwa

imekatwa na kuchomwa Serikali inaona mkaa unachomwa na mkaa upo barabarani hakuna hatua inayochukuliwa kwa uharibifu wa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali inakataa makusudi kuelewa kwamba biashara ya mkaa imeharibu mazingira, huku wakieleza uharibifu wa mazingira inatokana na mifugo mingi nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia juu ya Ziwa Natron, Hifadhi ya *Lake Natron* ni muhimu kwa kulinda ndege *Flamingo* na maeneo chepechepe inayozunguka Ziwa hilo. Naomba Serikali itoe Elimu ya kuhifadhi Ziwa hilo kwa jamii ya wafugaji wanaozunguka mlima Lengai na Ziwa Natron. Bila wananchi hao mazingira ya Ziwa yangeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaelezea kuweka kiwanda cha magadi Ziwa Natron lakini mpaka sasa hatujui wazo hili limeshindikana au bado lipo. Baada ya wananchi wa Wilaya ya Longido kusikia kwamba Serikali inapendekeza kuwapa wawekezaji kujenga kiwanda hicho *Lake Natron* wakaenda ziara Kenya kuangalia Kiwanda cha Magadi Ziwa Lake Magadi. Walikuta kwamba bado Flamingo wapo, hakuna uharibifu wa mazingira yaliyotokea, wananchi waliozunguka eneo hilo wamefaidi, Halmashauri imeendeleza na Serikali kwa ujumla imepata mafanikio mengi. Naomba Serikalii ipime hasara na faida itakayopatikana endepo kiwanda kitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali waanzishe miradi ya kimaendeleo kwenye vijiji vinavyozunguka Ziwa Natron. Kama Serikali itakuwa na nia ya kuifadhi Ziwa hilo ni afdhali Elimu itolewe kwa jamii na kuwasaidia kuliko kutambua Flamingo kwamba ni muhimu zaii kuliko watu na wanyama wengine wanaouzunguka ziwa hilo. Serikali iwe karibu na wanandhi hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe pongezi za dhati kwa Makamu wa Rais mwenyewe, Waheshimiwa Mawaziri, Katibu Mkuu na wahusika watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri na utendaji baada ya kusema hayo, ninaomba kuuliza,

Kwa kuwa baadhi ya changamoto zilizoorodheshwa, ni pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira, je, Serikali imejipanga vipi kuendelea kutoa semina/elimu kwa Umma wakiwemo wale wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro waishio vijijini na kulima kwenye maporomoko ya Milima? Je, elimu hiyo inaweza kutolewa, Kiwilaya, Tarafa, Kata na Vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza uwepo mradi wa elimu ya mazingira kwa Umma katika ngazi ya Kata. Zaidi sana ikiwezekana elimu hiyo ifundishwe mashuleni namna ya utoaji walimu wa sasa kwa kutumia msafara wa mwenge au siku ya mazingira duniani bado haitoshelezi kabisa kwani wanaofikiwa ni wachache sana ambao wako kwenye mikusanyiko hiyo.

Pendekezo la pili ni:- kuhusu Wizara yenyewe isimamie/ijitegemee kwani kuwa kwenye mwavuli wa Ofisi ya Makamu wa Rais inafunikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwani hata Bajeti iliyotolewa ni ndogo kulingana na shughuli husika. Je, inaweza kuundwa Wizara ya mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Kilimanjaro umezungumziwa muda mrefu kuhusu theluji kuyeyuka. Lakini sijawahi kusikia ufumbuzi wake. Je leo hapa mtoa hoja anatueleza nini katika kudhibiti kuyeyuka kwa theluji hiyo? Ninaomba ufafanuzi na majibu ya kina.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, naomba kukumbusha suala la *Environmental Impact Assessment (EIA)* kuhusu barabara itakayojengwa kutoka MLALO hadi MBARAMO itakayopitia msitu wa SHAGHAYU kwa KM zisizozidi 16. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi hiyo wakati alipofanya ziara katika Wilaya ya Lushoto mwezi Julai, 2008 kuwa Barabara hiyo lazima ijengwe kabla ya uchaguzi wa 2010.

*NEMC* iliitaka Halmashauri ya Lushoto itenge T.shs. 60 millioni kwa ajili ya gharama ya kutayarisha *EIA* hiyo lakini Halmashauri imeshindwa kutenga kiasi hicho cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hiyo ni muhimu sana kwa wananchi wa Kata ya Mbaromo kwa sababu itapunguza umbali wa kufika Makao Makuu ya Wilaya ya Lushoto kwa kilomita 120. Hivi sasa inawalazimu Wananchi hao kuteremka kwa miguu kilomita 13 hadi Mnazi ndipo wapate gari kwenda Mkomazi, Mombo (Wilaya ya Korogwe halafu wapande gari lingine la kuwapandisha kwenda Lushoto.

Kwa ujumla, Kata ya Mbaramo haina barabara ya kuwezesha mabasi na magari ya mizigo kuwahudumia. Barabara ya Mlalo – Mbaramo ndio itakuwa mkombozi wa Wananchi wa Kata ya Mbaramo – yenye wakazi wapatao 12,000 (Elfu kumi na mbili).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli ya Serikali kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kutekeleza ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Baada ya hapo napenda kushauri kuwa uchafu umekithiri sana katika Jiji la Dar es Salaam. Mifereji mingi sasa imeziba na imejaa maji meusi na machafu sana, hii ni hatari sana kwa afya za watu. Vile vile hamna magari ya kuzoa taka, tafadhali tuwe na magari ya kuzoa taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna bustani nyingi sana kandokando ya barabara za Jiji la Dar es Salaam. Hizi bustani zinazuia maji ya mvua kutiririka hadi kwenye mifereji. Chukua hatua, pata sehemu za kulima Bustani za maua na zuia vibaka wasiweke bustani kando ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam ni chafu sana na inatia aibu, hatua za haraka zichukuliwe kusafisha Jiji hili.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Babati imekuwa ikikumbwa na mafuriko kwa miaka mingi tangu miaka ya sitini, sabini, themanini, tisini na sasa miaka ya 2000 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi mbalimbali zimefanyika kulinda Mazingira ya Ziwa Babati na misitu yote inayozunguka Wilaya ya Babati. Hata hivyo mwelekeo umeonyesha kuwa bado Serikali haijafanikiwa kuhifadhi mazingira na Babati inaendelea kupata mafuriko kwa kasi kubwa kutokana na Ziwa kujazwa tope na makorongo yote yanayoelekea Ziwani. Kwa hali ilivyo matatizo yaliyopo ni vigumu kuyadhibiti kwa Bajeti ya Halmashauri peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa ushauri ufuatao:-

1. Ni muhimu kuweka *register* ya uharibifu unaotokea kila mwaka Babati.

2. Ni muhimu kuielekeza Wilaya ili ifanye yaliyo katika uwezo wake.

3. Iainishwe mambo gani yatakayofanywa na Taifa kuhusiana na mafuriko na utunzaji wa Mazingira.

4. Wizara hii isome na kuchukua hatua kwa taarifa pekee na ya mfano iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuishia Machi, 2010 iliyohusu Ukaguzi wa Ufanisi Sura ya Sita, Ukurasa wa 79 mpaka 95. Menejimenti ya kuzuia na kupunguza maafa yapatikanayo na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawatakia kila la heri katika kazi zenu muhimu sana kwa Taifa letu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwana mazingira, napenda sana kupanda miti, najua faida ya kuwa na miti. Naomba niulize ile sheria ya ukataji miti ovyo tumeshaifuta? Kama bado kwa nini haitekelezwi? Udhaifu wa utekelezaji uko wapi kwa utaratibu huu wa kazi ya ukataji miti tukijipa miaka 10 ijayo nchi yetu itakuwa jangwa. Ni vizuri tukasimamia sheria kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miti inakatwa ovyo kwa ajili ya mkaa, Dar es Salaam ikielimishwa wakaachana na kutumia mkaa badala yake watumie gesi. Dar es Salaam ni watumiaji wakubwa wa mkaa, magari yaliyobeba mkaa peke yake kutoka bara huleta katika Jiji la Dar es Salaam sheria ni vizuri ikatumika. Serikali iache kigugumizi cha kusimamia sheria vinginevyo miti yote itakwisha.

Upandaji miti hapo awali ilikuwa kila mwaka ilitengwa siku moja ya kupanda miti naomba niulize kazi ya upandaji miti ni sawa na kazi ya ukataji miti?

Kama kasi ya upandaji imepungua Serikali ina utaratibu gani wa kuongeza kasi ya upandaji miti kwa nchi nzima na kama kasi ya ukataji imeongezeka Serikali ina utaratibu gani wa kuondokana na kazi ya ukataji miti.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri ya kuhifadhi mazingira na vile vile kudumisha Muungano. “Msemo wa Kero za Muungano” sikubaliani nao. Muungano sio kero. Kero zilizoko ni za utekelezaji. Muungano hauwezi kuwa kero.

Tatizo letu kubwa la mazingira ni la uelewa mdogo wa Watanzania kwa sababu hiyo nchi inatuharibikia mikononi mwetu. Hivyo tuna kazi kubwa ya kuwaachia watoto na wajukuu wetu Tanzania yenye mazingira bora na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, Ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake. Nikushukuru wewe binafsi na Ofisi yako kwa umakini.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba hii iliyoandaliwa na Watendaji kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika hotuba, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kutembelea Bukombe na kuzindua mradi wa Maji Tarafa ya Mbogwe – Bwelwa masikitiko yako kwa nini Mheshimiwa Makamu wa Rais tangu 2008 alipoahidi T.shs. 1,500,000/= kwenye kikundi cha watumia maji hadi leo hawajapewa? Mheshimiwa Waziri unataka kuwaambia wananchi wa Mbogwe Serikali imeshindwa kutoa ahadi hiyo? Au ni lini fedha hiyo itatolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hifadhi ya mazingira kwa wachimbaji wadogo wadogo wasaidiwe. Kwanini miradi ya akina mama ya kuwabadilisha toka matumizi ya mkaa kwenda matumizi ya gesi Bukombe haipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba miradi hii ya wanawake wa Bukombe wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kauchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii akiwepo yule wa masuala ya Muungano na yule wa Mazingira. Pia Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya Bajeti imelenga kuendelea kuimarisha Muungano wetu pia kutunza Mazingira yaliyotuzunguka nchini Tanzania, kwa maslahi yetu na vizazi vyetu vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vitambulisho, kwa upande wa Zanzibar wapo baadhi ya wananchi hasa kutoka vyama vingine vya upinzani wanalalamika kuwa hawakuandikishwa kama walivyoandikishwa kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba sasa hivi upo mlundikano wa vitambulisho katika ofisi husika na hadi leo hii vitambulisho hivyo havijachukuliwa. Hii imetokana na kwamba kipindi hicho walijitokeza wageni au wasio wakaazi wa Zanzibar kwa kipindi kirefu, kujitokeza kuandikishwa na kupiga kura kinyume na utaratibu kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada tu ya kupiga kura katika kipindi hicho waliondoka na kurudi wanakoishi bila kusubiri vitambulisho vyao na kuvichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki serikali imejikita katika suala zima la kuzingatia sheria na kufanya uhakiki wa wakaazi waliopo Zanzibar ndio wanaandikishwa kisheria tofauti na makosa yaliyofanyika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tume ya uchaguzi *NEC* na *ZEC* kwa upande wa Zanzibar *ZEC* imekuwa na utaratibu wa uandikishaji wananchi wa Zanzibar kwa mujibu wa sheria za uandikishaji.

Mheshimiwa Spika, walioandikishwa Zanzibar watamchagua Rais wa Zanzibar, Rais wa Muungano, Mbunge na Mwakilishi, kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, na *NEC* kwa upande wa Zanzibar katika kipindi hiki inafanaya kazi ya kuandikisha wale ambao hawapaswi kuchagua mbunge, mwakilishi wala Rais wa Zanzibar na sasa wao watamchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atapofanya majumuisho aliweke sawa ili wenzetu wasiofahamu suala hili waweze kujibiwa ili wasiendelee kupotosha wananchi na kufahamu kwamba Tume ya Uchaguzi *NEC* haifanyi majukumu yake kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza serikali kwa kushirikiana na serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wao na kuweza kushughulikia kero za Muungano na kufikia hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza kwa kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar, ukarabati mkubwa wa Ikulu Ndogo ya Muungano kule Wete Pemba.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali baada ya ukarabati huo na baada ya kupitishwa Bajeti ya Wizara katika kipindi hiki cha mwaka 2010/2011, kukamilisha ajira za watumishi wakiwemo watendaji katika Ofisi ya Makamo wa Rais, pamoja na Ikulu ya Jamuhuri ya Muungano iliyopo Wete Pemba.

Mheshimiwa Spika, hili litaweza kuleta msukumo zaidi na utekelezaji wa shughuli mbali mbali katika maeneo haya niliyoyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Nadhani Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais watapata muda wa kupitia hoja mlizotoa waweze kutoa majibu mara tutakapoingia saa 11.00.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, Wasemaji wote niliokuwanao katika orodha walikuwa wameshachangia. Kwa hiyo, ninaingia katika nafasi ya kuomba watoa hoja waanze mmoja mmoja kuweza kujibu. Tutaanza na Waziri wa Nchi, anayehusika na Mazingira.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona Ukumbi huu, kipindi hiki cha Bunge hili la mwisho, nimeshawaandikia wale wa upande wa waliokuwa wameniandikia ki-*note*, kubwa linalotakiwa zaidi ya yote ni ile bajeti. Ile ilihitaji kabisa *strictly quorum* ndio maana tuliita kwa majina. Lakini mkisema muingie hapa kwa majina, tena kikubwa ni bajeti. Sasa tunaelezea utekelezaji wa Wizara mbalimbali, kwa hiyo, *quorum* iliyopo hapa tunaiacha hivi ilivyo. Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola Muumba wa Dahari na Zama, Muumba wa Nchi, Bahari na Viumbe, Mola mtoa Riziki na Mpangaji Kagar, Mfalme na Mtimizaji ahadi na asiyeshindwa wala kukatizwa na chochote kwa kutupa uhai na kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya njema katika kuchangia hii bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba kutoa pole kwa wafiwa na ndugu na jamaa wote. Pole nyingi kwa jamaa na viongozi wote waliotangulia mbele za haki. Aidha, natoa pole nyingi kwa Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuondokewa na mume wake; Mwenyezi Mungu, amjalie moyo wa Subira. Mwisho, naomba kutoa pole kwa familia ya Marehemu mzee Suedi Masumai, aliyekuwa Mwenyekiti wa *BAKWATA*, Wilaya ya Arusha Mjini na muasisi wa chama, aliyefariki na kuzikwa jana mjini Arusha. Naomba Mwenyezi Mungu aipe subira familia yake na amlaze Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kubwa kwangu na kunipa majukumu mbalimbali katika kipindi cha miaka mitano. Nafasi hizo ni pamoja na kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge na Uratibu na sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Nina imani nimetumikia nafasi hizi zote kwa bidii na ubunifu na kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unaosema: "Imani Huzaa Imani." Nami namwombea kwa Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais wetu na Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, samahani kidogo tu-*clarify* jambo fulani. Hizi Wizara ni *Vote* mbili tofauti. Kwa hiyo, wewe unazo dakika 30 na Mheshimiwa Waziri anazo dakika 30. Tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unaosema, "Imani Huzaa Imani." Nami ninamwombea kwa Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, inshallah amjalie afya njema, maisha marefu na amjalie ushindi wa kishindo. Wananchi wa Tanzania bado tunampenda na bado tuna imani kubwa na uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa uongozi wake kwa ujumla na hususan kwa kuniongoza na kunielekeza katika kutekeleza majukumu yangu katika Ofisi yake ya kusimamia masuala ya mazingira. Kwa ujumla nimefarijika sana, nimejifunza mambo mengi sana kutoka kwake. Nami ninamwombea kwa Rabuka, amjalie apate kile anachokusudia na amfanyie wepesi yale yote yaliyo magumu. Shukrani zangu za dhati ni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Penda, kwa uongozi wake na mwongozo na ushirikiano mkubwa ambao amekuwa akinipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri. Nawatakia kila la heri kwa yote. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Mwenyekiti wangu wa Kamati - Mheshimiwa Job Ndugai na Kamati yetu ya Mazingira, Maliasili na Ardhi pamoja na Wabunge wote, watumishi wa Bunge na watumishi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Mwenyezi Mungu, atawalipa kwa kuwajibu maombi yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia kwa kuishukuru familia yangu, watoto wangu na mume wangu mpendwa Bwana Othman Soud, kwa ushirikiano mkubwa na kwa mapenzi anayonipatia. Mwenyezi Mungu, azidi kumtia nguvu na awapatie subira kwa ustahimilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru viongozi wangu wa dini, Masheikh wangu kwa elimu yao ya dini, dua zao na maelekezo. Aidha, nawashukuru sana viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali, Maaskofu, Mapadri na Wachungaji, kwa elimu na huduma na maombi ambayo wamekuwa wakiniombea. Ni kupitia dua na maombi yenu, naamini Mwenyezi Mungu amezidi kunitia nguvu na kuniongoza katika maisha yangu hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza humu Bungeni na kwa njia ya maandishi. Natambua pia Waheshimiwa Wabunge, wote waliochangia masuala ya mazingira katika bajeti zilizotangulia. Ni wazi kuwa dunia hii sasa inakabiliwa na changamoto kubwa ya kimazingira. Aidha, uelewa na ufahamu wa wananchi juu ya matatizo haya na jinsi yanavyoathiri afya na uharibifu wa mazingira umeendelea kujengeka ingawa bado mwamko ni mdogo. Jambo ambalo halijabadilika sana ni kasi ya

jitihada za wananchi katika kubadili tabia na kuwa na mwamko zaidi katika kuzingatia usafi wa mazingira na kutotupa taka ovyo au uadilifu wa kutumia nishati na kutumia nishati mbadala pale inapowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa kisera kuhusu changamoto ya mabadiliko ya tabia ya nchi umekuwa ukibadilika kila mara. Awali, changamoto hii ilionekana kama ni suala la mazingira, lakini sasa imekuwa ni suala la kiuchumi na kiuongozi. Ikitathminiwa athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi, inakadiriwa kwamba takribani 3% ya pato la Afrika, Tanzania ni moja ya nchi zilizoathirika sana kwa ukame na mafuriko, kuongezeka kwa kina cha bahari na kukauka kwa vyanzo vya maji. Bajeti ya kukabiliana na athari hizi kwa Tanzania, inakadiriwa kufikia dola bilioni moja kuanzia sasa hadi mwaka 2020. Kupata fedha kama hizi kunahitaji mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Hivyo basi, sasa hivi suala tunalolifanya ni utafiti wa kufahamu athari za kiuchumi kwa Tanzania ili kuweza kuangalia yafuatayo:-

Kwanza, ni kutathmini athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi kwenye Sekta za Kilimo, Nishati na Utalii na pia Afya. Lakini vile vile kuhakikisha ushiriki wa sekta binafsi ya jamii na hatua za kutekeleza mipango ya programu ya kuhimili mabdiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia michango mbalimbali iliyowasilishwa humu Bungeni, inaonesha kuwa ile dhana iliyojengeka huko nyuma ya kuona kwamba mazingira ni usimamiaji wa taka na upandaji miti tu, imeboreka zaidi na hivyo mtazamo mpana zaidi kuhusu mazingira umejengeka miongoni mwa wananchi. Naomba nitumie fursa hii kujaribu kuzijibu hoja mbalimbali ambazo zimewasilishwa humu Bungeni, na kwa wale ambao nitashindwa kuwataja kutokana na muda, nitaomba sana mniwie radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa hoja ambazo zimewasilishwa na Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Ninaishukuru sana Kamati kwa kazi kubwa na maelekezo ambayo wamekuwa wakitupatia. Katika hoja ambazo zimewasilishwa hapa ni kuhusu umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais kuongeza kasi zaidi katika kutengeneza na kumalizia kanuni na miongozo ambayo ilikuwa imebakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema tunapokea ushauri. Kanuni tutazitengeneza zaidi na tumepanga kwa kipindi hiki kutengeneza kanuni saba pamoja na miongozo mitatu na hivyo kufikia Kanuni 29 na miongozo 19. Aidha, kuhusu upungufu wa watumishi, tunajielekeza zaidi katika kuongeza watumishi hasa katika Wilaya. Sasa hivi katika Wilaya ambazo zina Maafisa mazingira, ni asilmia 90 tu ya Wilaya zote. Tunataka tufikie lengo la asilimia 100 ama kupata watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na *NEMC.* Jitihada zipo za kuweza kuendelea kupata watumishi katika Ofisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilizungumzia utunzaji wa mazingira na kutoa kipaumbele na hasa kuzitaka Serikali za Mitaa, kuongeza kasi na usimamiaji na kutoa kipaumbele katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tunaona kwamba ni chachu ya mabadiliko. Kama tunataka kuwa na mabadiliko katika usafi na usimamizi wa mazingira, basi juhudi kubwa zitaweza kufanyika katika Halmashauri za Mji na Halmashauri zetu za Manispaa na Wilaya. Tumeanza kwa kutoa mafunzo kwa kupitia Kamati za Ushauri za Mikoa, lakini na sisi viongozi tushirikiane kuhakikisha kwamba wote tunaweka msukumo mkubwa katika ngazi za Halmashauri zetu. Tunazo Kamati za Mazingira za kuanzia Kata mpaka Vijiji. Tuhakikishe kwamba zile Kamati zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala zima la nishati, na umuhimu wa sekta za nishati kwa matumizi yao ya maji na sekta zile zinazotumia maji kuweza kuchangia gharama za wale wanaotunza vile vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona hili ni wazo zuri. Limeanza katika ngazi ndogo kwa kupitia taasisi mbalimbali za kijamii katika maeneo ya Morogogo na maeneo ya Lushoto, tutaweka msukumo zaidi ili kuona kwamba mfumo huu wa kutoza kutokana na huduma hii ya maliasili kwa taasisi zinazofaidika na huduma hizi za maliasili, zinachangia huduma hii ili mazingira yaboreke zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilitoa msukumo zaidi kuhusu elimu ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeupokea ushauri na tutajielekeza zaidi katika kuongeza njia mbalimbali na ubunifu mkubwa katika kutoa elimu ili wananchi katika ngazi zote waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeambiwa kwamba elimu ya mabadiliko ya tabia ya nchi bado haijawafikia wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na ushauri huo na tunasema kwamba elimu tutaiwakilisha na tuhakikisha kwamba tunatumia vyombo mbalimbali. Sasa hivi tumeanza kwa kutunga wimbo kwa kutumia vijana wetu wa kizazi kipya na tunaamini kwamba wimbo huu umeanza kuenea. Tunatumia bendi na ngoma za kienyeji, lakini vilevile kutumia taswira na utaalam mbalimbali ili elimu hii iweze kuyafikia makundi mbalimbali ya kijamii ambayo kwa ujumla ndio waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitushauri kwamba zaidi ya mabonde yale ambayo tunajielekeza, yaani bonde la Ziwa Viktoria, bonde la Ziwa Tanganyika na bonde la Ziwa Nyasa, hebu tuongeze kasi sasa katika mabonde yote ya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na ushauri huo na tumeanza kwa kutengeneza mkakati unaosimamia hifadhi ya fukwe zetu, bahari, maziwa, mabwawa na mito. Kwa kupitia mkakati huo, tuna uhakika tutayafikia mabonde yetu yote na kuweza kujielekeza. Na sasa hivi kikubwa tulichokiweka ni kufikia Ziwa Rukwa ambalo asilimia kubwa ya maji kama mnavyojua kilometa zaidi ya saba za maji, yameingia ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na tatizo zima la utupaji wa taka na usimamizi wa taka mijini. Hili Waheshimiwa Wabunge wengi wamelielezea na tumelipokea na tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitoa maagizo maalum kwa Wizara yetu, kwamba ni vizuri *NEMC* ikashirikiana na Mamlaka ya Ngorongoro ili kuona kwamba ile miradi ya kijamii ambayo inafanyika, basi kusiwe na kikwazo kikubwa kwa ajili ya kutengeneza tathmini ya athari za kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeupokea ushauri na tutafanya kazi kwa pamoja ili kuona kwamba tathmini ya athari ya kimazingira haikwamishi miradi ya kijamii katika maeneo yale ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kambi ya Upinzani ilitoa maelezo yao kwa ufasaha kabisa na mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Waziri Kivuli, Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kwa kweli ameelezea katika hotuba yake kwa kina kabisa masuala muhimu na ya msingi sana. Suala zima la mabadiliko ya tabia ya nchi na umuhimu wa kujielekeza katika elimu hiyo, jinsi gani athari za mabadiliko ya tabia ya nchi zinaathiri fukwe zetu. Lakini uharibifu wa *bio-anuwai* katika maeneo mbalimbali. Lakini pia alielezea masuala mazima ya uchimbaji holela wa madini katika maeneo yetu na jinsi gani tunatakiwa tusimamie na kuona kwamba uzoefu tulioupata katika mgodi wa *North Mara*, hautajielekeza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote tumeyaona, tumeyazingatia na mikakati mahsusi tumeiweka. Sasa hivi kinachofanyika kule *North Mara* ni kuona kwamba ufuatiliaji kama tulivyoupanga unaendelea, lakini kama tulivyoeleza, timu ya wataalamu wa afya wanafanya utafiti ili kuona ile athari iliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliochangia katika hoja hii kwa kuongea walikuwa wachangiaji watatu. Nianze na Mheshimiwa Mbunge, Jackson Makwetta, ambaye yeye alielezea suala zima la elimu kuhusu mabadiliko ya tabia ya nchi. Nianze kwa kumpongeza sana Mzee wangu Mheshimiwa Jackson Makwetta - Mbunge wa Njombe Kaskazini. Kwa kweli huyu amekuwa ni mwanaharakati mkubwa wa mazingira na amekuwa balozi wetu. Mheshimiwa Jackson Makwetta, ameweza kutengeneza kijarida kuhusu athari ya mabadiliko ya tabia nchi na akakipa jina la *"Gharika Linakuja Tujengeni Safina"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu hiki tumekichukua sisi Ofisi ya Makamu wa Rais na tutakichapisha na tunachofanya sasa hivi ni kuweka vibonzo, vikatuni, ili kiweze kueleweka kwa lugha rahisi na nyepesi na wananchi wakapata elimu hiyo. Mimi niseme tu, kama nilivyomuahidi, hii kazi aliyoifanya, hii jitihada tutaitunza na nina imani kwamba wananchi wa Jimbo la Njombe Kaskazini na wenyewe watamtunza kutokana na hii kazi nzuri anayoifanya ya kuangalia mustakabali wa nchi yatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa alizungumzia suala zima la tatizo la utupati wa taka ovyo pembeni mwa barabara. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa. Kama mtakumbuka, mimi na Mheshimiwa Celina Kombani, tulizindua mkakati huu pale kituo cha mabasi cha Ubungo, tukatoa elimu kwa waendeshaji wote wa mabasi, tukawaeleza umuhimu wa kuwa na vile vyombo vya kuweka taka ndani. Lakini inaonesha kasi ya kubadilika tabia kwa watu wetu ni ngumu na bado tutaendeleza elimu hiyo. Tutashirikiana sote kwa pamoja. Ninamshukuru sana Mheshimiwa kwa michango yake yote na ninasema kwamba bado tutapeleka elimu kwa sababu kasi ya kubadilika tabia ni kazi ambayo itachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucas Siyame, pia alizungumzia kwa kirefu tatizo la hifadhi ya msitu wa Isalalu katika Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hatuna sababu ya kujitetea hapa pamoja na kwamba misitu iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini bado tuna jukumu la sisi kushirikiana katika uratibu wa msitu huu. Nami nieleze tu kwa sababu msitu huu ni msitu wa jamii, na kupitia sheria ile kuna sheria ambyo inajielekeza katika usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii, mimi niseme tu kwamba suala hili tutalifuatilia na kwa vile tuna Ofisi ya *NEMC* pale kanda ya Mbeya, tutafuatilia kuona kwamba tatizo liko wapi na ni kwanini maamuzi katika ngazi ya Wilaya yanashindwa kufuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia inatoa tu mafunzo kwamba tufanye nini sasa ili misitu yetu ibaki, tuweze kuisimamia vipi hii misitu ikiwa katika sekta nyingine na mapolisi wako katika sekta nyingine. Tunatakiwa tuwe na uratibu gani na kuwe na ushirikishaji gani, hasa ukizingatia kwamba sheria zipo, sheria ya misitu ya mwaka 2002

lakini na sheria yetu ya mazingira ya mwaka 2005 na zote ni kali na zote zinatoa adhabu; ni kwanini bado kunakuwa na hali kama hii? Namwomba Mheshimiwa Mbunge, wananchi wake wajue tu kwamba hili amelieleza na tutalifanyia kazi na nina uhakika tukishirikiana wote tutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale - Mbunge wa Mbeya Vijijini, naye alieleza matatizo haya yote ya uchafu katika maeneo yetu ya Miji, lakini vile vile akaeleza sasa tatizo ni nini? Ni sheria? Na kama sheria ipo ni kwa nini bado kunakuwa na taizo hilo? Lakini vilevile akaeleza kwamba kuna mabasi yanayofanya vizuri, akataja basi la Sumri ambalo linafanya vizuri na wanatoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, elimu tumetoa kwa mabasi yote, lakini bado. Sisi tunashirikiana na *SUMATRA* ili kuhakikisha kwamba wale ambao hawafuati yale maelekezo, basi watafungiwa leseni au watapewa adhabu na kulipishwa faini kutokana na kuendelea kuchafua mazingira. Naomba wananchi wote wawe askari. Mimi nina uhakika mwananchi atakayekuwa ndani ya basi akimwona mwenzake anatupa taka nje, akimsimamia na kumwambia kwamba usifanye jambo hilo, kweli suala hili litabadilika. Tushirikiane wote, tusimwachie mtu fulani ndiye yeye awe mkatazaji. Sisi sote tuwe ni maaskari wa kuamua kwamba suala hili halitakiwi liendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala zima la usafi wa mazingira na usimamizi wa taka katika miji. Suala hili limezungumziwa na Wabunge wengi sana ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotaja, Mheshimiwa Jackson Makwetta amelizungumzia suala hili, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, Mheshimiwa Siyame, lakini vilevile Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Janet Masaburi, Mheshimiwa Hadija Al-Qassmy na Mheshimiwa Anna Abdallah, wote wamezungumzia kwa hisia kubwa kabisa kwamba tatizo la uchafu wa mazingira katika nchi yetu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema kweli tunakiri kwamba kweli tatizo hilo lipo, kama Ofisi ya Makamu ya Rais, tumetengeneza mkakati wa usimamizi wa taka ambao umekwishaandaliwa na umeshasambazwa katika maeneo yote. Serikali vilevile imeandaa mpango wa kuboresha mazingira katika miji yetu kama tulivyoeleza tunaanza na jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha kuwa na *environmental master planning*, sio *Cities, ni environmental master planning* ambayo itaangalia matatizo mazima ya kimazingira.

Lakini vilevile tumeona tusaidie Jiji la Dare es Salaam tuweze kutoa huo uchafu hasa katika mito yetu. Katika mto Msimbazi, tumeandaa mradi kushirikiana na *UNEP* na tunategemea huo mradi tutashirikisha mgambo hao hao wa mji na ikibidi tutashirikisha hata JKT ili kusafisha taka zote ambazo zipo na kuweza kuona kama hali hiyo itarudi kama ilivyokuwa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mkakati ule wa Tanzania *Strategic Cities* na katika moja ya mambo pamoja na miundombinu itakayowekwa ni kusimamia masuala hayo ya usafi.

Wabunge wengi wamezungumzia masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi, nao ni Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, vilevile Mheshimiwa Janeth Massaburi na hawa wote walichozungumzia ni kwamba tunafanya nini na miradi gani ipo? Lakini vilevile Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Ali Khamis Seif amezungumzia mikakati gani ipo?

Mimi nimweleze tu kwamba mikakati iliyopo sasa hivi, tuna mikakati mikubwa ambayo kwanza ni kuhusisha suala zima ya mabadiliko ya tabia ya nchi katika sekta zetu zote. Tuna fedha za kutoka Japan ambayo kazi kubwa ni kuhakikisha kwamba kila sekta inajitathimini kuangalia athari ya tabia ya mabadiliko ya tabia nchi itaiathiri vipi na mikakati gani itafanywa. Zaidi pia ni kuangalia katika kitengo kinachoshughulikia maafa.

Mheshimiwa Omari Kwaangw' alizungumzia uzoefu wake wa Jimbo la Babati, maafa ya mara kwa mara yalivyotokea tunajifunza nini kutokana na ripoti ile ya Mkaguzi Mkuu? Sisi tunachosema tunataka kujifunza kwa kuangalia jinsi gani tutaweza kuimarisha kitengo chetu kinachoshughulikia uratibu wa maafa, lakini kupata tathimini za awali ili kujiepusha na maafa kabla hayajatokea. Kwa hiyo, hilo ni moja, tumeimarisha vituo vyetu ili kuweza hata kupata utabiri wa kutosha.

Lakini Mheshimiwa Mbunge wa Pangani leo hayupo, lakini nimthibitishie tu kwamba suala la ukuta ule wa Pangani ni historia. Sasa hivi fedha zimeshakuwepo, mtaalam mwelekezi ameshapatikana, tunasubiri tu aje aanze kazi na angekuja kama sio suala hili la bajeti kupita na wataalam walikuwa *busy* kutengeneza hii bajeti, basi angekuja mwezi huu. Lakini tunategemea mwezi ujao mapema atakuja ili kazi ianze.

Mheshimiwa Janeth Massaburi, aliomba kuwa na *carbon tax* na hili tumeshalifanyia kazi, tumeshapendekeza maeneo ambayo tunaweza tukaweka ushuru hasa katika maeneo yale ya magari ambayo yanatoa uchafu na maeneo mengine ambapo sasa hivi Wizara yetu ya Fedha inaangalia baadhi ya maeneo ya kodi ambayo tumeyaweka.

Lakini vilevile kuna mradi unaoangalia masuala ya Pwani, ambayo itakwenda mpaka maeneo ya Zanzibar hasa katika zile fukwe ambazo zimeathirika sana. Sasa hii pia itashughulikia maeneo kama ya Chuo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, maeneo ya Kigamboni ambayo Mbunge wa Kigamboni amelielezea kwa hisia kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala misitu, ukataji misitu na uchomaji wa miti hovyo, limezungumziwa kwa kirefu sana. Mheshimiwa Shemeji yangu Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Rajabu Ahmed Juma, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Ali Khamis Self, Mheshimiwa Lucas Siyame, Mheshimiwa Khadija, wote wamelizungumzia kwamba tunafanyaje kuondokana

na tatizo hili la ukataji wa miti hovyo? Sheria zipo na kwanini hazifuatiliwi? Hili tumelieleza kama nilivyoeleza hapo awali, elimu itaendelea kutolewa ili kuona kwamba ulinzi shirikishi wa misitu ya jamii inarudi.

Kulikuwa na suala la kilimo cha tumbaku na jinsi kinavyoathiri misitu yetu. Mheshimiwa Cosmas Masolwa - Mbunge wa Bububu na Mheshimiwa Godfrey Zambi, wote walilielezea hili suala na kusema kwamba tunafanya nini? Mimi nadhani kwa maana ya ofisi ya mazingira, tumeanza kwa kutoa elimu kwa wakulima wanaolima hili zao la tumbaku kutumia matanuru ya kisasa ambayo yanaitwa *rocket burn. Rocket burn* hii ina uwezo wa kupunguza kiasi cha kuni kinachotumika kutoka tani tisa mpaka tani 4.5. Hii bado haituridhishi. Sisi tumejiunga katika mtandao wa kitaifa wa nishati mbadala ambayo Makao Makuu yake yako Uarabuni na tunategemea kwamba kupitia nishati mbadala tutapata teknolojia nzuri zaidi ambayo haitatumia kuni na mkaa ambayo itaweza kusaidia katika ukaushaji wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya mazingira na kukuza weledi, ni suala limezungumziwa karibu na Wabunge wote waliochangia hapo, kwamba kunahitajika kuwe na elimu yenye unafuu kuongeza zaidi kasi ya elimu. Mimi nazidi kusema kwamba napongeza sana Taasisi ambazo zimeshirikiana na ofisi yetu kutoa elimu. Niwapongeze sana wenzetu wa *JET* - Chama cha Waandishi wa Habari ya Mazingira, niwapongeze Chama cha Wanasheria wanaotetea masuala ya mazingira.

Nizipongeze na Taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikiangalia masuala ya mazingira kama *TATEDO* kwa maana ya kutoa ubunifu wa majiko ya sanifu, wa akina mama wale wanaotumia nishati ya takataka zile za makaa ya mawe kwa ajili ya kutengeneza mkaa na brikate zile na wote ambao wameshiriki kwa kweli tunawapongeza na tutaendelea kushirikiana katika kutoa elimu.

Matumizi ya nishati jadilifu, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, amelizungumzia hili, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Ahmed Mohamed Hamid na yeye alizungumzia hili na sisi tunasema kwamba sasa hivi tunachotaka ni kuangalia jinsi gani tutaweza kutoka kwenye kutumia kuni na mkaa hasa katika miji kama Dar es Salaam na kutumia gesi hasa gesi asilia. Tumeanza kwa kushawishi makampuni ya Serikali na makampuni binafsi kukopesha watumishi wao ili waweze kupata magesi. Kama nilivyosema asubuhi, kwamba kampuni ya *Orxy* imekuwa msitari wa mbele na imeshaanza kuingia mikataba na makampuni mbalimbali ili kuweza kuwakopesha watumishi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala zima la eneo la Temeke, Mheshimiwa Abbas Mtemvu - Mbunge wa Jimbo la Temeke alitueleza kwamba kulikuwa kuna maji yanatiririka katika kiwanda cha Serengeti, lakini vilevile kulikuwa na eneo la Keko ambalo lilikuwa lina mmomonyoko mkubwa wa ardhi na akaniomba nikatembelee eneo lile.

Nasema kwamba, eneo lile nitatembelea lakini hata kabla ya mimi kwenda, wataalam wangu walikwenda wiki iliyopita na wakakagua eneo lile la mferejei na wakaona kwamba ule mfereji ulikuwa umejengwa na Manispaa na kwamba mfereji huo ulikuwa unatumiwa kinyume na Kampuni ile ya Bia na wale waliambiwa kwamba waache kutumia mfereji huo na tayari *notice* imeshatolewa kwa kiwanda kile. Pia Baraza limezuia watu wote wanaotiririsha maji katika mfereji ule kuweza kuacha. Niseme tu kwamba tutapanga muda ambao tutakwenda bila kuwa na *notice* ili tuweze kuona kwamba hali hiyo kama inarejea au imebadilika.

Lakini vilevile kulikuwa kuna maoni ya Kambi ya Upinzani kwenye masuala yetu ya *NEMC* hasa katika masuala ya jinsi gani tunaangalia viwanda na kipaumbele katika uwekezaji ili usiathiri afya za wananchi. Niseme tu kwamba kuna viwanda vingi kama saruji ambavyo vinatumia teknolojia isiyokuwa na athari, kwa mfano, kwa vumbi inayozalishwa kwa kiwandani.

Lakini vilevile Baraza limekuwa likikagua, kuna viwanda vilevile ambavyo kama Tanga, Wazo, Mbeya ambavyo vimekwishaanza kutekeleza agizo hilo la kubadilisha teknolojia ili kuwa na viwanda ambavyo havitatoa vumbi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine za Wabunge zinazohusu mazingira zinazojitokeza wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa ni suala zima la Serikali inafuatilia vipi na kuchukua hatua Halmashauri za Serikali za Mitaa zinazoshindwa kusimamia usafi wa mazingira. Hata hivyo, Serikali kupitia Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imekuwa ikitoa ushauri wa karibu kwa Halmashauri hizo.

Kwa vile tayari tunatoa tuzo kwa wale wanaofanya vizuri, hivi sasa ofisi yetu itapendekeza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kuona sasa tunaweza tukatoa *list* ya wale ambao wanafanya vibaya ili kipindi kijacho wakaweza kuboresha jitihada za usimamizi wa masuala haya ya taka na kuweka kipaumbele  na tuna hakika kwamba hali hii inaweza ikaleta mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum Kagera, na yeye alizungumzia suala zima la uchafu katika maeneo ya Mwanza, akazungumzia masuala ya uchafu katika maeneo ya Ziwa Victoria na maeneo mengine. Mimi niseme tu kupitia ule mkakati wetu wa hifadhi wa fukwe zetu, bahari, maziwa mito na mabwawa tutajielekeza katika matatizo yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikalini pia kulikuwa kuna suala zima la Mheshimiwa Mbunge wa Mwera ambaye alizungumzia kuhusu North Mara. Nimwambie tu kwamba suala kama tulivyofuatilia kwa pamoja aliliona, sasa hivi tunachosubiri ni taarifa ya Wizara ya Afya ili kuona kama kuna uhitaji wowote wa fidia au vipi.

Mheshimiwa Brg. Hassan Ngwilizi - Mbunge wa Mlalo, alizungumzia suala zima, Serikali itasaidia vipi jimbo lake liweze likajenga barabara iliyo katika ahadi ya Chama cha Mapinduzi ambayo imeshindwa kujengwa kutokana na kutokuwa na tathimini ya athari kwa mazingira? Sisi tunamwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokana na kilio hiki cha muda mrefu na kwa sababu ni ahadi ya Serikali na imekuwa ya muda mrefu, baraza limekubali kwamba suala hili sisi tutalichukua na ninyi kupitia Halmashauri yako ifuatilie kwa Baraza la Hifadhi ya Mazingira ili tathmini hii ikafanywe kwa gharama za ofisi yetu na barabara hiyo ya Mlalo mpaka Mbaramo, kupitia msitu wa hifadhi ya Shangio iweze ikajengwa. Nakupongeza sana Mheshimiwa kwa ufuatiliaji wako.

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer pia alizungumzia suala la maeneo ya Longido na kuona kwamba wananchi wapewe elimu kuhusu bioanuwai hasa katika ziwa la *Natron.* Nampongeza na tutaendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Jadi Kadika naye alizungumzia masuala mazima hayo ya tathmini, ujenzi holela, uchimbaji na yote hayo tumeyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha, naomba uniruhusu nitoe ufafanuzi kidogo kufuatia taarifa ambazo zimekuwa zikiwachanganya wananchi wengi. Nimekuwa nikipokea simu na ujumbe mfupi wa maneno kutoka kwa baadhi ya wakazi wa Arusha wakinilaumu kuwa kwa nini naondoa nia yangu ya kugombea jimbo la Arusha Mjini? Naomba kutumia fursa hii kwa ruksa yako kuwaambia ndugu zangu wa Arusha kuwa jamani nia yangu ya kugombea jimbo la Arusha bado iko pale pale, hivyo msidanganyike na taarifa zisizo na usahihi wowote mimi nipo imara na ni kweli hamnioni huko jimboni kama mnavyowaona wenzangu kwani ninafanya kazi mliyonituma ya kuwawakilisha humu Bungeni. Hivyo basi, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitaomba ushirikiano wenu muda utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huu, naomba kumaliza kwa kushukuru sana akinamama wa Mkoa wa Arusha kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kipindi chote cha miaka kumi kama Mbunge wao wa Viti Maalum. Nina imani uzoefu huu nilioupata utakuwa ni nguzo muhimu kuweza kuniwezesha kuhimili vyema kazi yangu ya Ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini nikipata ridhaa ya wakazi wa Arusha kama nilivyotangaza nia yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kumalizia nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu ya Rais na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano wao mkubwa. Kwa hiyo, napenda kuwashukuru sana washiriki wetu wa maendeleo, Taasisi na makampuni binafsi kwa michango yao na kunisaidia katika jitihada mbalimbali kuendeleza kampeni za kutuza na kulinda mazingira. Naomba kutaja baadhi ya mashirika na makampuni ambayo ni pamoja na Serikali ya Norway, Umoja wa

Ulaya, *TANAPA, Twiga Cement, Oryx gas, CRDB, Cargo Star, Tigo, Stanbink, Eco Bank, Zain, Diamond Trust Bank* na Benki Kuu ya Tanzania.

Naomba pia kuvipongeza vyombo vyote vya habari na wana habari ambao wamekuwa mstari wa mbele kufuatilia masuala ya mazingira. Aidha, kipekee nawapongeza waandishi wa habari walioshinda tuzo ya Ubalozi wa Uingereza katika masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabia ambayo ni Deogratus Mfungale, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mazingira *JET*, Lukas Liganga, Mwandishi wa *The Citizen* na Timoth Kitundu - Mwandishi wa *The Express*. *(Makofi)*

Vilevile napenda kuwashukuru wasanii walitunga na kuimba nyimbo za mazingira kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira ya Afrika iliyofanyika tarehe 3 huko Arusha ambao ni Mrisho Mpoto, Bushoke, Keisha, Baby Madaha, Feruzi, Juma Nature, *Rich One* na Ismael. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tumesikia ya kwamba umeshatangaza nia hadharani, sasa naomba nimwite mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii leo jioni kuhitimisha hoja ambayo asubuhi tumeizungumza. Naomba kwanza nitaje wale wote ambao walishiriki katika kuchangia hoja hii kwa kuzungumza ambao wako 11. Nao ni Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mheshimiwa Ali Khamis Self, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Lucas Siyame, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Abbakar Khamis Bakar na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. Hawa ndio waliozungumza.*(Makofi)*

Walioandika ni Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Gen. Hassan Athuman Ngwilizi, Mheshimiwa Lucy Brasio Msafiri, Mheshimiwa Dk. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy na Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw’, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa,

Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyacha, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Ussi Ame Pandu. Naomba samahani kama jina nimetamka vibaya, majina mengine unajua ni taabu kutamka naomba mnisamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru wewe sana na Mheshimiwa Rais kwa kunipa heshima hii kunipa heshima hii ya kunipa kazi hii ya Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, namshukuru sana kwa imani yake na namuombea afanikiwe katika safari yake ndefu ya kuomba urais mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa msaada wake wa kikazi anaonipa mara kwa mara, namshukuru pia Makamu wa Rais ambaye sasa hivi naye yuko katika mchakato, namtakia heri fanaka katika jambo lake.

Mwisho, nawashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Uzini kwa kunivumilia muda mrefu, siko jimboni kwa shughuli hizi za kikazi ambazo ni muhimu pia kwa Taifa letu. Naomba wanisamehe sana endapo muda mrefu siko Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja moja baada ya nyingine. Naanza kujibu hoja ya Mheshimiwa Maida ambaye yeye alizungumzia juu ya mlundikano wa vile vipande vya kupiga kura ambavyo viko vingi sana akasema kwamba ile ni kwa sababu watu wengi walipandikizwa na kwa hivyo anaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu mpya ambao unasaidia kupunguza mapandikizi katika majimbo.

MwIngine alikuwa Mheshimiwa Anna Abdallah yeye anasema anakerwa sana na neno kero za Muungano. Neno hili halifai kutumika katika daftari letu, na mimi nakubaliana naye kabisa, tutafute jina lingine zuri ambalo tutatumia, lenye kuonesha zaidi *positive* kuliko *negative*. Moja kwa moja ni changamoto na wengine tutatoa nafasi watu watoe maoni yao jina gani tutumie badala ya neno kero ambalo yeye linamkera sana. Mimi pia linanikera, sina la kufanya tu.

Mheshimiwa Zambi amezungumzia kwamba yeye anaona kwamba utaratibu huu wa kupunguza mambo ya Muungano katika orodha ya Muungano unaweza baadaye ukadhooifisha Muungano wetu na ile nia njema ya viongozi wetu wa Marehemu Karume na Mwalimu Nyerere ukapotea kabisa. Mimi nadhani kwamba inategemea nia gani, kama nia ni njema sio mbaya nategemea nia ya kuongeza au kupunguza jambo lenyewe lote lile.

Muungano huu ni Muungano wa ridhaa za nchi mbili, zilikuwa huru kabisa. Kwa hiyo, kuongeza au kupunguza ni muhimu. Jambo baya ni dhamira mbaya, lugha mbaya na matusi. Kwa hiyo, nashauri kwamba Mheshimiwa Zambi tukubaliane kwamba kwa sababu Muungano huu ni wa hiari tukubaliane katika jambo jema tufanye tu tusiwe na taabu yoyote. Kama ilivyoingizwa, pia inaweza kupunguzwa lakini utaratibu mzuri ufuatwe.

Pia lingine amesema kwamba kuna Serikali inajenga majengo mbalimbali kwa mfano Zanzibar kule majengo ya Serikali ya Ikulu na kadhalika, anaona kama ni gharama. Sio gharama kwa sababu nchi mbili hizi zote ni ndugu pamoja na viongozi, wakienda Zanzibar lazima wakae nyumba nzuri kabisa. Kwa hiyo, hili jambo sio baya kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Tuendelee nalo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rajabu Hamad yeye anashauri kwamba vilevile vikao vya Muungano, vinakwenda pole pole sana kwamba anashauri tuhimize, tuharakishe ili maridhiano yapatikane. Ni jambo jema sana. Mimi nafikiri hili jambo la maana sana. Lakini pia analalamika kwamba ule mradi wa *MACEMP* ambao unasaidia wavuvi kwamba bado vile vifaa vya kuvulia maboti na majahazi ni madogo sana, yanafaa ili uende bahari kuu kule waweze kupata faida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri suala hili tutawaarifu wanaohusika kwamba misaada hii ya *MACEMP* ya maboti ni vyema maboti haya yawe makubwa zaidi na nyavu nzuri zaidi ili wananchi wafaidike zaidi kuliko kupewa maboti madogo madogo ambayo hayafiki mbali kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji yeye pia alilalamikia juu ya mfuko wa *CDF* kwa Zanzibar, hili ni jambo jema na zuri na kama mlivyoona katika Bajeti yangu Serikali ya Muungano imetoa shilingi bilioni 1.2, ni hela nyingi sana kwa kila mwaka, mimi naamini kwa Zanzibar kwa muda wa miaka kumi ijayo fedha hizo zitakuwa nyingi sana na zitatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini anayolalamikia yeye ni kwamba urasimu ni mkubwa sana wa kupata fedha na kweli hata mimi Jimboni kwangu pia wanalalamika kwamba hawapati, lakini nafikiri tutajitahidi ili kipindi kijacho tuharakishe. Nia yetu ni kwamba Wabunge wapate fedha mapema ili ziwasaidie katika jukumu lao la kuimarisha maendeleo ya nchi yetu na mimi naamini kwamba fedha hizi zitapatikana kabla ya Bunge kuvunjwa ili Wabunge nao wasimamie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nitoe wito na inaonekana kwamba baadhi ya viongozi wa Halmashauri za Zanzibar hawakuelewa madhumuni ya mfuko huu, mara nyingi wanadhani kwamba wao ndiyo wana mamlaka ya mifuko hii. Mifuko hii mwenyewe ni Mbunge na ndiye Mwenyekiti na mwenye maamuzi ya mwisho. Kwa hiyo, natoa wito kwa viongozi wa Halmashauri ambao hawaelewi kwamba mifuko ya Bunge ya *CDF Zanzibar*, Mwenyekiti wake ni Mbunge na ni Mfuko wa Bunge, yeye ndiye anaamua apewe nani na kwa kiasi gani na kwa kazi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaomba kwamba nao pia wasaidie wafanikishe jambo hili kwa sababu nasikia mpaka sasa hivi baadhi ya Wabunge hawajapata fedha hizi, naomba Serikali ya Zanzibar nayo itusaidie kuharakisha fedha hizi ili wananchi wazipate. Kwa hiyo, nasema hili la Mfuko wa Jimbo tunafikiri kwamba wenzetu watatuelewa na watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kutoa ushauri kwa Wabunge wa Zanzibar kwamba nilipata malalamiko baadhi ya Wabunge wengine wao wenyewe wanachukua *cheque* kwenda kununua mabati na saruji, ni mbaya hiyo, tutafungwa bure, tuache hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri wewe usimamie tu, usichukue *cheque* wala kununua saruji, milango wala madirishi na baadaye tutafika hapa nusu ya Wabunge tutafungwa. Kwa hiyo, ushauri wa bure huo na wala hauna gharama yoyote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy pia amezungumzia juu ya kuharakishwa kwa mchakato huu wa kuondoa usumbufu na matatizo ya Muungano na mimi naunga mkono katika hili.

Mheshimiwa swahiba wangu Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu ameongea mengi lakini kwanza amesema kwamba kipindi hiki ni kipindi cha maridhiano na ni ukweli. Mimi nakubali kwani ni jambo jema sana hilo, lakini kwa mfano na matendo yaani matendo yetu na lugha zetu zifanane basi, tunataka kujenga jamii mpya, jamii ya umoja na mshikamano lakini hazitoshi, sisi wenyewe mazungumzo yetu yakatofautiana. Ukiangalia hotuba ya leo ya Dada yangu Mheshimiwa Riziki Omar Juma ni tofauti na maneno anayoyasema Bwana Jussa, hakuna maridhiano wala nini. Kwa hiyo, nafikiri njia nzuri ni kwamba kauli zetu pia zionyeshe kwamba tunabadilika kabisa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu amezungumza pia juu ya nafasi ya Makamu wa Rais, mara nyingi tumezungumza hapa sijui kama hatuelewani kwamba hii nafasi ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais kuondolewa. Hili jambo limekwenda kwa mujibu wa Katiba yetu na kulikuwa na maridhiano kati ya SMZ na SMT, kuna maridhiano ndani ya Chama cha Mapinduzi yaani Chama Tawala na ikaondolewa na ikionekana kuna haja basi mchakato huo kwani uchomeako ndiko utokeako. Kwa hiyo, nashauri kwamba Ndugu Jussa tusaidiane kuambizana kwamba tupunguze basi jazba na maneno makali makali ili tujenge hiyo jamii mpya tunayoitaka. Mimi safari hii nimepunguza, hakuna jazba hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa amezungumza kwamba ni muhimu mambo ambayo yako katika Katiba ambayo hayafai tuyaondoe, ametoa mfano wa bandari. Ni kweli na nimejibu swali moja kwamba tangu nchi hii ilipoanzisha Muungano huu bandari si jambo la Muungano. Lakini tuna mchakato wa Kamati wetu tutaangalia yale mambo yote ambayo tunaona kwamba hayana faida basi tutayaondoa tu, kuna mambo ya bandari, takwimu ambayo haina umuhimu wowote ukiacha takwimu ya sensa. Kwa hiyo, kuna mambo mengine si muhimu lakini tutakwenda vizuri ili tuweze kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia kuhusu miradi ya *MACEMP*, tofauti hii ipo kwa sababu tukubaliane kwamba idadi ya watu wa Zanzibar na Tanzania Bara ni tofauti, ukubwa wa nchi ni tofauti na kwamba haiwezi kuwa sawasawa.

Ukiangalia mwambao wa Zanzibar ni mdogo kuliko mwambao wa Tanzania Bara, kwa hiyo, wakati mwingine hizi asilimia kubwa ni kwa sababu tu ya mazingira ya ukubwa wetu. Lakini zaidi pia inategemea na wale ambao wanatoa fedha hizi na masharti yao ambayo yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Shoka Khamis Juma amezungumza juu ya *TFC* yaani Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo pia imezungumzwa na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary. Ni kweli kwamba ni miaka mingi lakini ni jambo jema kwamba angalau sasa hivi jambo hili lipo katika mchakato, tayari Tume hii ya Pamoja ya Fedha imekutana, imefanya utafiti, imekwenda nchi mbalimbali, imepeleka taarifa yake kwa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, sasa hivi angalau tuko katika mchakato mkubwa na ninaamini kabisa kwa wakati wa Bunge lijalo jipya kwa watakaokuwepo hapa bila shaka jambo hili litakuwa tayari limeshamalizika, tupeni subira ili tuweze kusubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed pia amezungumza juu ya dosari ndogo, kwa hiyo nasema hayo ni mambo ambayo ni ya msingi ambayo tumezungumza.

Mheshimiwa Bujiku Sakila amesema kwamba yeye anaamini kwamba Watanzania wana subira juu ya Muungano wetu huu na Muungano huu ni wa binadamu wala siyo wa malaika kwa hiyo, utakuwa na makosa na dosari kwa hiyo tuvumiliane na baadaye tutafanikiwa tu. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ametoa pongezi nyingi sana kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwamba ni mtu muungwana na mtaratibu, anayeheshimu Sheria na anapenda watu, bila shaka anampigia debe kwa mambo yake ambayo yanakuja huko Zanzibar. Nakushukuru sana Mheshimiwa Bujiku na nitapeleka salamu zako kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, anakumbushia juu ya mfuko ule wa *CDF*, pia amezungumzia juu ya tatizo hili la kuchelewa kwa fedha hizi na mimi nakubali na kama nilivyowasihi ni kwamba tuwe na subira bila shaka baada ya Bajeti yangu tutafuatilia tuone hatua gani tumefikia kwani na mimi pia nahitaji fedha hizi zinisaidie katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, yeye anakumbusha ziara ya Makamu wa Rais alipotembelea Jimboni kwake Bukombe mwaka 2008 na alitoa ahadi kwamba angesaidia mradi wa maji na tumezungumza na Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Faragha wamesema kwamba fedha hizo ambazo aliwaahidi ameshazitoa na amezitoa tarehe 01 Septemba, 2009 na namba yake ya *cheque* hiyo ilikuwa ni 254638 kapewa *RAS*. Kwa hiyo, fuatilia fedha hii tayari Makamu wa Rais halazi damu yeye akiambiwa hapo hapo anatoa, hakuna wasiwasi wowote kwa hiyo fuatilia kwa *RAS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary amezungumza mengi kidogo lakini labda niseme tu kwamba mimi si Mwanasheria lakini mimi ni msanii na mshauri. Ndiyo ni

msanii, nayo pia ni kazi, Shakes Spear ni msanii pia, Shaaban Robert ni msanii pia, kila mtu na fani yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi si Mwanasheria lakini kuna mambo yamezungumzwa hapa lakini nafikiri nataka niyaseme na baadaye Mwanasheria yupo atanisaidia kwamba kwanza nizungumze habari ya fulana, fulana hizi ni kidogo za kuwapa wananchi, ni kweli ni kidogo lakini hatuwezi kuwa na fulana shilingi milioni 40 tukawapa watu kwani hatuna uwezo huo wa kutoa fulani 40 za Muungano na kila mtu akavaa. Lakini tunajitahidi kwa yale ambayo tunaweza, mojawapo ikiwa ni kutumia *radio* na *television* ndiyo mambo ya muhimu sana na tunajitahidi na ni lazima uelewe kwamba Watanzania wengi sasa hivi wamezaliwa baada ya Muungano, kwa hiyo, mengi hawayajui, ukiacha baadhi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema bado tuna kazi kubwa ya kuelimishana na ni wajibu wetu na ni kazi ya kila mtu, kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Abubakar tusaidiane kwamba tutumie vyombo vyetu hivi vya habari tutasaidia kuwaelimisha watu juu ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimestaajabu kwamba amezungumza yeye na Mwanasheria mwenzako Dr. Kabudi hawakuelewana juu ya tafsiri ya Hati za Muungano na mimi siyo Jaji hapa siwezi kuhukumu lakini nitasema kwa maoni yangu mimi nafikiri Hati za Muungano zilikuwa muhimu sana kabla ya kuanzishwa kwa Muungano kwa sababu ndiyo hati za msingi za makubaliano.

Lakini baada ya Muungano kuanzishwa ikatungwa Sheria na Katiba na Hati za Muungano zimekaa kama kumbukumbu tu, lakini nchi inakwenda *dynamic*, lazima Sheria zitabadilika na mambo yataongezeka kwa hiyo, hayawezi kuwa yale yale 11 ya mwaka 1964, hayawezi kuwa! Na kama yangekuwa mambo yale yale 11 leo Ndugu yangu Mnyaa usingekuwa humu ndani kwa sababu yapo 22 na vyama vingi vya siasa vimeingizwa katika orodha ya Muungano. Kwa hiyo, mabadiliko haya pia yanatusaidia sisi kuwepo humu ndani bila hivyo tusingekuwepo humu ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema Hati za Muungano zina umuhimu wake katika wakati wake lakini sasa hivi imekuwa sehemu ya historia yetu na kumbukumbu tu lakini haziwezi kuwa hizo hizo, hazibadiliki mara kwa mara. Lakini yuko Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama nimekosea naomba anisaidie, lakini mimi nafikiri hilo ndilo jambo la msingi kwamba hati hizi haziwezi kuwa hivyo hivyo, tunafuata sheria na taratibu basi zinabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jambo ambalo linafanywa basi linafanywa kutokana na mabadiliko katika nchi yetu na linafuata taratibu na kanuni kwani hii nchi ni ya kidemokraasia kwa mfano jambo likianzishwa labda linaanza kwenye Serikali, kwenye Baraza la Mawaziri, kwenye Bunge hapa inapigwa kura na kwa sheria linaorodheshwa. Kwa hiyo, nasema hili sidhani kama ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia suala la Rais Mheshimiwa Amani Abeid Karume kule Pemba na mimi nilikuwepo na mimi niko karibu zaidi kuliko yeye yaani mimi niko karibu zaidi na Rais Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuliko yeye

Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, nimemsikia Rais Mheshimiwa Amani Abeid Karume akisema kwamba mambo haya nimeyaongea na mwenzangu na tumekubaliana, lakini bahati mbaya Mheshimiwa Jakaya Kikwete hakusema, akasema ndiyoo! Sikumsikia mimi na nilikuwepo pale siku ile.

Kwa hiyo, nasema jambo hili ni jema na zuri lakini twende kwa utaratibu wake kwa sababu nchi yetu haiendeshwi kwa *decree* kwamba Rais akisema inakuwa, hapana! Anatamka kwenye vikao vyake anavyokwenda halafu litakuja tu hapa maana jambo jema litakuja hapa, lakini tupeni muda Serikali ya Muungano ijadili halafu baadaye litakuja hapa, nani hataki mafuta? Hata mimi wa kutoka Uzini nataka mafuta na nitapata hela nyingi sana, lakini tufanye taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kwamba kweli Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume alisema na Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Jakaya Kikwete amesema kwamba jambo si gumu linazungumzika, lakini basi halimalizikii hapo ni lazima liende kwa taratibu zilezile za Kikatiba na Kisheria, lije hapa Bungeni, Wabunge waulizwe, *two thirds* ya Zanzibar na Bara ili tuikubali au tuitoe na mimi naamini kuwa Watanzana na hekima zao watalikubali tu hakuna gumu hata moja lakini tupeni nafasi tulimalize hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia kuhusu suala la mikopo kwamba kwa nini Serikali ya Zanzibar inapokopa nje ni lazima ipate dhamana ya Serikali ya Muungano. Siyo lazima, inategemea na anayekopesha, kama kuna nchi ambayo iko tayari kuikopesha Zanzibar bila dhamana ruksa haizuiliwi kwa sababu ina mamlaka yake yenyewe. Lakini unaposema kwamba lazima ipate dhamana basi bila shaka dhamana hiyo ni jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano la Kikatiba si la kupenda kwamba Serikali ya Muungano ndiyo wenye dhamana ya kudhamini mikopo yote ya Serikali ya Zanzibar kwa wale ambao wanataka mikopo hiyo yenye dhamana. Kwa hiyo, hili jambo si gumu nafikiri na sheria ipo lakini bahati mbaya siijui ni sheria gani lakini sheria hiyo ipo ambayo inatoa nafasi kwa Serikali ya Muungano kutoa dhamana. Kwa hiyo, hili si jambo gumu sana hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha nashukuru kwamba imefikia hatua nzuri sasa hivi, tunazungumza vizuri, hakuna shida yoyote na tutaelewana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa alizungumza juu ya gharama kubwa za kulipia mchango wa awali wa miradi ya *TASAF* na *MANCEP*. Hili jambo halipo kwetu sisi bali lipo katika Wizara ya Utawala Bora na ninaamini kwamba tutawaarifu wahusika ili waone kama kuna uwezekano wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu amesema mengi sana ndiyo maana nasema hotuba yake ilikuwa na mambo sana lakini moja ambalo lilikuwa zito sana anasema kwamba kwa muda wa miaka mitano Serikali hii ya Tanzania haikufanya chochote. Amezungumza weeee, lakini tumetia pamba sikioni! Sidhani, kwangu mimi

ukiangalia pamba hakuna na kila kitu nakisikia lakini mambo kwa utaratibu wake yanakwenda.

Kwa hiyo, la kwanza amezungumza kuhusu mabadiliko ya Katiba ile ambayo ilizungumzwa ya Makamu wa Rais kwamba imekwenda kwa taratibu zake maalum mwaka 1994 na Wabunge wakaulizwa hapa wakapiga kura likapita. Jambo la pili amezungumza kuhusu jina la Tanzania limeletwa kuvungwa vungwa tu hivi, lakini ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya Kwanza nafikiri inazungumzia juu ya jina kamili la Muungano na siyo Tanganyika na Zanzibar bali Tanzania na hili lilipitishwa pia na Bunge hili na kwa bahati nzuri jina hili pia wakati fulani wananchi walitakiwa watoe maoni yao na walete majina likakubaliwa.

Kwa hiyo, jina hili ni kwa mujibu wa Katiba na hata Katiba ya Zanzibar ukiangalia inazungumzia jina hilo hilo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, nafikiri hili jambo ni halali kuitwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuhusu mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki amesema, kunakuwa na vikao vya ndani kwanza kati ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano kabla ya kwenda Afrika Mashariki na kwa hiyo, nakubaliana ni vya kuzungumza na kadhalika. Lakini nafikiri mimi vikao vyote vile vya viongozi wakuu wa Afrika Mashariki, Rais wa Zanzibar anakuwepo ili kuonyesha *independency* yake katika jambo lile kubwa sana.

Kwa hiyo, sidhani kama Serikali ya Zanzibar inatupwa nyuma haishirikishwa, inashirikishwa na mimi sioni ajabu kwa mambo ambayo si ya Muungano kama Serikali ya Kenya na Zanzibar wanataka kusaidiana kuhusu kilimo, Serikali ya Tanzania haiwezi kuzuia, kwa nini? Au Kenya, Rwanda au Burundi kwa nini? Hakuna matatizo yoyote kwa hiyo kuna mambo ni ya Muungano kama ulinzi na usalama lakini mengine hayana kitu lakini muhimu ni kujenga mahusiano mazuri na wajibu wa Serikali ya Muungano ni kuisaidia Tanzania Zanzibar ili ifanikiwe katika mambo ya nchi za nje, wao ndiyo wajibu wao mkubwa sana kwa sababu wao hawana Serikali ya mambo ya nchi za nje kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali ya Tanzania kufanya hivyo wala si hisani, ni lazima wafanye hivyo na ninaamini kwamba Serikali ya Muungano itafanya hivyo kwa ajili ya mambo mbalimbali.

Lakini jambo lingine ambalo kidogo limenistua ni pale aliposema kwamba Muungano wetu umedhoofika zaidi katika miaka mitano iliyopita. Hili kidogo limenistua sana na bahati mbaya Muungano si kama binadamu huu ni mwembamba sana kama wembamba wake lakini unafikirika tu. Sasa mimi sioni kuna kitu gani. Kwanza kipindi cha miaka mitano nchi yetu imekuwa na amani mtu hanisuti hapa! Amani kubwa sana na ni jambo la kujivunia tumekaa watu zaidi ya milioni 40 tena na makabila mbalimbali na tabia zao, kwa hiyo, hili jambo si vizuri kulisema hadharani kwamba tumedhoofika, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeimarika kwanza kwa jambo la amani ambalo ndiyo mtaji mkubwa popote duniani, watu wanatamani amani lakini hawapati, sisi tunatembea usiku na magari Mawaziri hata hatuna habari kabisa hii ni nchi ya amani kabisa, hii ni pepo ya dunia kwa amani. Kwa hiyo, nasema mambo haya ni lazima tuyatunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, miaka mitano hii tumejenga umoja imara zaidi pamoja na maridhiano ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu hapa, ni umoja mkubwa sana ambao ni watu hawa wa makabila tofauti tunajenga umoja mzuri sana, haya ni lazima tuyathamini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pia tumekuwa na ushirikiano mkubwa sana kati ya SMT na SMZ, nimesema asubuhi hapa kuna miradi michache na mikubwa ambayo imesaidiwa, sisemi kwa sababu nasumbuliwa bali nasema kwa sababu ni wajibu, yaani wajibu wa mkubwa kumsaidia mdogo, hapana kusumbuliana hapa, ni wajibu wa mkubwa kusaidia mdogo, mama kumsaidia mwanawe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakati Serikali ya Zanzibar ina matatizo basi Serikali ya Muungano ina wajibu kuisaidia Serikali ya Zanzibar kufanya hivyo na inafanya hivyo. Kwa hiyo, kwa mfano mradi ule wa Pangani tumetaja idadi ya fedha ambazo Serikali ya Tanzania imelipa ili wenzetu wa Pemba wapate umeme wa kudumu na wa uhakika na kuleta maendeleo ndiyo maana ya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza juu ya barabara ile ya Amani, tumezungumza juu ya Mfuko wa Jimbo, tunazungumza jinsi Serikali ya Muungano inavyojenga majengo mengi sana Zanzibar na ni makubwa ya kisasa kabisa ambayo ndiyo inaleta thamani ya fedha kwa Zanzibar yenyewe. Jengo kubwa na zuri kabisa Zanzibar ni jengo la *BOT*, ni mali ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunguu pale ukienda jengo zuri na la kisasa ni la Muungano la Makamu wa Rais, Uhamiaji na Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jirani pale kuna majengo ya Bunge na kadhalika, kwa hiyo, nasema si vizuri kusema sana mambo haya tukajaribu kuwavunja moyo watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, lakini lingine ambalo nafikiri ni la muhimu ndugu zangu ni kwamba tuna fursa nyingi sana na mara nyingi nasema jambo hili kwa ndugu zangu wa Zanzibar, tuna fursa nyingi sana hatuzitumii, tunalalamika tu. Zanzibar tuna ekari tatu, humo kuna ng’ombe, mbuzi, kuku, minazi na kila kitu mchanganyiko lakini leo hapa kuna mtu amepata ekari 1,000 au 10,000 usinung’unike njoo ukae huku upate na wewe, huulizwi kibali, hata huku Bara kuna kila aina ya madini, njoo na jembe lako chimba tu huulizwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kufuga ng'ombe, kule Zanzibar ng'ombe anafungwa kamba, huku ni ajabu ng'ombe hafungwi kamba anaachiwa tu, ardhi kubwa ipo. Kwa hiyo, ombi langu ndugu zangu ni kwamba tusilalamike, tuchukue fursa hii ambayo ni muhimu kwa ajili ya Taifa letu na mimi nafikiri tusilalamike, tuchukue nafasi sasa tuje hapa tupate nafasi yetu kwa sababu hupati mahali popote nafasi kama hii kwamba wewe unatoka asubuhi na jembe lako unachimba tu madini, una ng'ombe wako na mbuzi wako huulizwi chochote na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tuna bahati Muungano wetu ni mzuri sana, Muungano ambao umedumu kwa miaka mingi, zipo nchi ambazo zimejaribu kuungana lakini zimeshindwa. Mwaka 1972, Misri na Libya wameshindwa, mwaka 1975 Mali na Togo wameshindwa, mwaka 1958 Misri na Syria wameshindwa, mwaka 1959 Mali na Senegal wameshindwa, mwaka 1958 Ghana, Guinea na Mali wameshindwa, kwa hivyo sisi tuna bahati sana na ni mfano katika Afrika ya Mashariki na duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ndugu zangu tuendelee kujenga umoja, amani, uzalendo, demokrasia na tuendelee kujenga Taifa kubwa ambalo ndiyo nguzo kabisa na kuleta upendo na mshikamano ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru baadhi ya watu ambao niliwasahau hapa. Nimesahau kumtaja Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula wa Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, hoja hii imeungwa mkono. Mimi nakwambia huu Muungano nyie muuache kama ulivyo, kwa sababu wale wanaosema Zanzibar waingie *East Africa* kama wao, sasa mgogoro ulioko ndani ya Afrika Mashariki si ardhi? Kule kwetu sisi Wazanzibar wanalima vitunguu, hata vile vitunguu swaumu wako kule hatuwaulizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule katika Jimbo la Njombe Kaskazini, wengine wamegombea Uenyeviti wa Mitaa na Vitongoji na wamechaguliwa, wala hatujawauliza tunasema ni wenyeji. Kwa hiyo, jamani viongozi sisi ndiyo wenye matatizo wala siyo wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Waheshimiwa Wabunge wakati mjadala unaendelea Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu alikuwa amesema kuhusu Mwanasheria Mkuu ambaye alikuwa Mwanasheria wa kwanza na kwamba alishiriki katika kutengeneza zile *Articles of Union*, tukamuagiza kwamba atuletee *document* hiyo katika muda wa siku mbili, ameandika barua kwa Spika, kuomba muda uongezwe kwa sababu *CUF* wana Mkutano Mkuu hivi karibuni na yeye ana nafasi kubwa katika chama hicho

kuandaa mkutano huo. Kwa hiyo, ameomba kuongezewa muda na sisi tumejadiliana tumeafikiana tarehe 5, Julai, 2010 alete taarifa hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya hapo nimesema hoja hii imeungwa mkono sasa nitamuita Katibu kwa hatua zinazofuata. Katibu kwa vifungu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26- Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General*……sh. 4,542,109,000/=

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekti, nakushukuru sana. Programu ya 10, *sub-vote 1001*, kifungu kidogo cha 220700, *Rental Expenses*. Ukiangalia gharama za kupangisha inaonekana katika mwaka wa fedha 2008/2009 zilikuwa ni kama shilingi milioni 200 lakini, katika Bajeti ya mwaka unaokuja tunakwenda kwenye shilingi bilioni 1.003, sasa mimi nataka kujua ni kwa nini Serikali inaondoka katika utaratibu wa kujenga majengo yake yenyewe na kuendelea kupanga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu katika kukodi hakihusiki tu na majengo, zaidi ni kukodisha ndege kwa ajili ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, ndiyo maana fedha ni nyingi, hivyo, ni gharama za usafiri.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Programme 10, Subvote 1001, Basic Salaries –Pensionable Posts,* Mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, pia hapo hakuna mshahara wa Waziri, ni Ofisi rasmi ya Makamu wa Rais, kwa hiyo hakuna mshahara.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ndiyo huo huo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hamna hamna, haiingii humu ndani utamhoji vipi, tunahoji hawa waliomo humu ndani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General*……sh. 1,800,993,400/=

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimpongeza Waziri kwa kupeleka pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Amani - Mtoni ambayo ilikuwa ni ahadi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa na katika hotuba yake amesema amepeleka zaidi shilingi 1,000,600,000/= sasa ninataka kujua tu hizo pesa zilipelekwa lini na ni nani waliyempelekea kwa sababu sioni kazi yoyote inayofanyika huko, ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Serikali ya Muungano wajibu wetu ni kutekeleza ahadi ambayo Rais ameitoa ya kupeleka pesa kule Zanzibar na fedha imefika zaidi ya miezi mitatu iliyopita. Kwa hiyo, wajibu wetu tumeshaufanya wa kupeleka fedha hizi. Nimejaribu kuwapigia simu wahusika wa Zanzibar, lakini bahati mbaya simu zao sikuzipata. Kwa hivyo, nafikiri Mheshimiwa Mbunge afanye subira lakini wajibu wetu sisi tumeufanya, kupeleka fedha kule Zanzibar kwa ajili ya barabara ya Mtoni – Amani. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi katika *vote* hiyo hiyo ya 31 Programu ya 10, *sub-vote 1001* kifungu kidogo 210,000, *Basic Salaries – Pensionable Posts*.

Mheshimiwa Waziri, ninaomba msaada wako sasa hivi Kibaha kuna kitovu cha mji, katika kitovu cha mji kuna kiwanda ambacho …

**MWENYEKITI:** Kuna nini, Kibaha kuna kitu gani?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitovu cha mji ambako kuna kiwanda kinachotoa harufu. Masuala ya mazingira tumekuja ofisini kwako Mheshimiwa Waziri, umesema utashughulikia na tayari kuna viwanja vingine vinajitokeza hata bila ya kuandaliwa ramani na vinajengwa. Hakuna *environmental assessment or impact*, sasa mimi ninaomba unisaidie kile kiwanda cha ngozi ambacho tumeshakuja ofisini kwako na nimeshakueleza, kinachukuliwa hatua gani na sasa hivi pale patakuwa kitovu cha mji na kuna hoteli za kitalii zinataka kujengwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru na kumpongeza sana Dada yangu, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kwa jinsi alivyokuwa mfuatiliaji mkubwa wa masuala haya ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alinieleza kuhusu kiwanda hiki cha ngozi cha Kibaha na mimi na wataalam wangu tulikwenda na tukakagua eneo lile la kiwanda na kwa wakati ule kiwanda kilikuwa hakifanyi kazi na tulikuta hali ambayo ilikuwa inaridhisha na hata harufu ile hatukuisikia. Sasa kama kiwanda kimeanza kufanyakazi, itakuwa ni jambo ambalo ni jipya na ninamuomba dada yangu, Mheshimiwa Dr. Zainab

Gama basi aache tulifuatilie hilo suala ili tuweze kuona kwamba kama wanafanya uchafuzi basi hatua zichukuliwe na kama hawawezi kutumia teknolojia ambayo italeta hali nzuri basi tunaweza tukachukua hatua za kinidhamu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, lakini wewe hukuonekana. Haya, basi!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 31,* Programu ya 10, *sub-vote 1001,* kifungu kidogo 210,000 *Basic Salaries – Pensionable Posts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko ya mara kwa mara hasa kutoka Tanzania Zanzibar kuhusu mgawanyo wa fedha za misaada kutoka nchi za nje. Je, ukigawanya fedha zinazopelekwa Tanzania Zanzibar kwa idadi ya Wanzanzibar na pia ukagawanya zile zinazobaki Tanzania Bara kwa idadi ya Watanzania Bara, ni upande upi wa Muungano ambao unapata fedha nyingi *per capita?* Naomba nisaidiwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Muungano hazigaiwi kwa namna hiyo, kwa Zanzibar. Utaratibu ni kwamba kuna mgao wa fedha kutoka kwa wafadhili ambao wanapeleka Zanzibar na mgao huo kwa *formula* ya muda ni 4.5% tukisubiri matokeo ya Tume ya Fedha ya Pamoja.

Kwa hiyo, hivi sasa hatuangalii idadi ya watu, tunaangalia maamuzi ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano kwamba kwa sasa hivi fedha zote za msaada wa Zanzibar kutoka nje, zile ambazo hazihusiani na Tanzania Bara basi 4.5% ziende Zanzibar. Huo ndiyo mgawanyo rasmi ambao uko kwa muda, baadae utabadilika kwa mujibu wa maelekezo ya Tume ya Fedha ya Pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katika makubaliano tuliyofikia kwamba ukishauliza ndiyo umemaliza ingawa siyo nzuri sana, zamani tulikuwa tunasema unaweza kurudia, lakini naona makubaliano tuliyoafikiana wakati tunaanza yalikiukwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*……………… sh. 232,274,900/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *sub-vote 1002,* kifungu kidogo 221300, *Educational Material, Supplies and Services*. Tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri hapa kwamba elimu kwa wananchi wetu kuhusu masuala ya mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi ni ndogo na lazima kuwe na juhudi kubwa sana za kuendelea kutoa elimu.

Sasa nilipokuwa nasoma hapa nilidhani lazima tutaona kuna fedha nyingi sana kwa ajili ya vipeperushi, mabango, sijui na nini na vijitabu. Sasa naona huku kwenye Bajeti ni *zero,* nilitaka maelezo sasa hiyo elimu itatolewa kwa utaratibu upi?

**MWENYEKITI:** Hilo hata Naibu Spika, anaweza kukujibu, kwa sababu hii hapa ukisoma, hiyo *sub-vote 1002* ni *Finance and Accounts*, si hayo unayozungumza. Hayo unayozungumza yako mbele huko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit* ……………..sh. 666,399,200/=
Kifungu 1004 - *Information, Education and Communication*…......................................................sh. 264,926,100/=
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit* …………………… sh. 161,187,000/=
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*…..................................…………sh. 176,646,900/=
Kifungu 2001 - *Union Secretariat* ...........……......sh. 34,124,650,500/=
Kifungu 5001 - *Environment*……………………….. sh. 4,115,351,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001- *Administration and General*..……sh. 4,767,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………sh. 231,250,000/=
Kifungu 2001 - *Union Secretariat*.…………………..sh. 133,861,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Environment*..……………………..sh. 18,336,904,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 5001 kifungu kidogo cha 6506 *Lower Kihansi Environment Management Project.* Huko nyuma tumewahi kuambiwa kwamba tulikuwa tunatunza vyura walioondolewa Kihansi kule Marekani na kwamba, Serikali ilikuwa inatumia pesa nyingi kwa ajili ya kuwatunza. Lakini ili kukwepa hizo gharama tulishaambiwa kwamba Serikali ilikuwa kwenye *process* za kurudisha vyura hao hapa Tanzania, kwa maana ya kuwapeleka kwenye maeneo yao kule Kihansi ili Serikali iondokane na mzigo wa kutumia hela nyingi kwa ajili ya kutunza vyura nje ya nchi.

Je, hatua ipi imefikiwa sasa katika kuhakikisha kwamba tunaondokana na gharama hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali zuri la Mheshimiwa Zambi. Nadhani kama tutakavyoona katika mradi huu fedha zinazotoka nje kupitia Mfuko wa Mazingira wa Dunia, ni shilingi bilioni 1.9 na sisi kwa maana ya fedha za kwetu za ndani ni shilingi milioni 120. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa hivi ni kwamba wataalam wetu walikwenda Marekani na kuweza kuangalia mazingira ya wale vyura yalivyo na kuja kuangalia huku kwetu watawezaje kurudishwa na hilo ndilo zoezi linaloendelea hivi sasa, kuweza kuweka mazingira ya hali ile iliyoko kule na ujoto joto na mvuke mvuke huku ili wale vyura waweze kurejeshwa. Kwa hiyo, kwa maana ya vyura hao ni fedha za nje, ambazo zinatumika za Mfuko wa Mazingira wa Dunia, ili kuweza kuwarudisha na kuwatunza bioanuai hiyo ambayo ni ya kipekee duniani. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *vote* hiyo ya 31, *sub-vote* 5001, kifungu kidogo cha 6569 kinahusiana na *Lake Tanganyika Environment Management Project*. Katika fungu hili sioni *project* yoyote kuhusiana na mazingira ya Ziwa Victoria sasa nilitaka nijue kama nini wazo la Serikali kuhusiana na mazingira ya *Lake Victoria*, kwa sababu kuna uchafuzi mkubwa katika Ziwa hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la Ziwa Victoria halijaonyeshwa hapa kwa sababu hapo awali lilikuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais lakini sasa hivi liko chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwa hivyo, hilo litajitokeza wakati Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya akiweza kujibu hoja yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya ingawa sikukuona mwanzo labda sababu inaeleweka. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 6571 ambacho kinaendana kabisa na kifungu cha *NEMC* cha nyuma nilikuwa naomba nifahamu kwamba katika mpango huu ulioko hapa utahusisha na suala la kuangalia uwezekano wa kuwa na kijinjia kinachofikisha kwenye chanzo cha Mto Ruvuma kwa sababu kupitia MKUKUTA watu huwa siku ya Makumbusho ya Vita vya Majimaji wanakwenda kuanglia ule mto na kiasi kwamba uteremkaji wa kufika kwenye kile chanzo inakuwa ni mgumu kiasi cha kuharibu mazingira. Je, katika mpango huu na sehemu hiyo itazingatiwa?

**MWENYEKITI:** Sijui Waziri unakijua hicho kinjia, naomba ujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unahusisha suala zima la kuzingatia na kuhuisha Sheria ile ya Mazingira. Kwa hivyo, kwa maana ya huko Ruvuma na elimu nzima ya masuala ya mazingira pia itahusishwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji. Wabunge wote wameafiki, kwa hiyo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais yamepitishwa rasmi na Bunge hili.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba niwapongeze Waheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wote wawili kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa utulivu kabisa jambo ambalo sikutegemea. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ndugu yangu Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, zamani alikuwa anahamaki kweli kweli, siku hizi amekua na amejibu kwa utulivu kabisa.

Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa sababu swali la kuhoji na kujadili ni wajibu wetu na kupewa majibu mazuri pia ni haki yetu. Kwa hiyo, naridhika kabisa kwamba tumefanya kazi vizuri na kwa sababu hatuna matangazo mengine naomba niwatakie jioni njema na muwahi sana kwenye mpira lakini unapoangalia mpira kila siku mkumbuke kazi ya Bunge ipo, kwa hiyo, msipotee kabisa. *(Makofi)*

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 22 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*